**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Nne – Tarehe 18 Juni, 2007**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Orodha ya Shughuli za leo kuna jambo muhimu ambalo lilisahauliwa na imetulazimu turekebishe Orodha ya Shughuli za leo, kwa sababu zipo Hati za kuwasilisha mezani ambazo hazikuyatangulia maswali. Kwa hiyo, Nyongeza ya Orodha ya Shughuli za leo imetawanywa sasa hivi ni badiliko ambalo litahusu shughuli hizo. Kwa hiyo, sasa nitamwita Katibu kwa kutuongoza katika shughuli hizo.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:-**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2006. Mpango na Maendeleo kwa mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/2008.

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:-**

Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kuhusiana na Hali ya Uchumi wa Taifa na mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na mfumo wa matumizi ya Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:-**

Taarifa na Mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kwa Bajeti ya mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 30

**Semina ya Viongozi Iliyofanyika Ngurdoto**

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara tu baada ya Viongozi Watendaji kama vile Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuteuliwa walipewa Mafunzo ya kazi katika semina iliyofanyika Ngurdoto Arusha:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika katika kugharimia semina hiyo na vyanzo vya fedha hizo ni vipi?

(b) Je, semina hiyo ilisaidia kwa kiasi gani katika utendaji wa kazi zao za kila siku?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, ilipata ushindi wa kishindo kwa nafasi ya Urais kwa asilimia 80.28 pamoja na Ubunge ikilinganishwa na Vyama vingine vilivyoshiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Ushindi huo peke yake ni changamoto kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Matarajio ya wannachi ni makubwa kutokana na malengo yaliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwani yaliwapa watu matumaini na hivyo wakaamua kutoa ushindi huo mkubwa. Katika kutekeleza majukumu yake kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Rais alilazimika kupanga safu ya Viongozi wa kumsaidia ambapo Mawaziri wapya 19 kati ya 30, Manaibu Mawaziri wapya 26 kati ya 31, Wakuu Mikoa Wapya 15 kati ya 21 na Wakuu wapya wa Wilaya 47 kati ya Wakuu wa Wilaya 113 waliokuwepo katika Awamu ya Tatu waliteuliwa. Hivyo, ili kujibu matarajio makubwa ya jamii iliyotoa ushindi mkubwa kwa CCM ilikuwa ni muhimu kwa kuanzia kwa Viongozi hawa kukutana pamoja ili wawe na uelewa wa pamoja katika kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005 kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa kupitia Semina Elekezi ya Ngurdoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Semina Elekezi ya Ngurdoto iliyofanyika tarehe 22 – 27 Agosti, 2006 jumla ya Sh.1,602,000,000/= zilitumika. Vyanzo vya fedha hizo ni kutoka sehemu zifuatazo:-

(i) Mfuko wa Kuboresha Utendaji (*Performance Improvement Fund (PIF)* – Shilingi milioni 500,000,000. Unaoratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

(ii) Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa (*Local Government Reform Programme (LGRP)* shilingi milioni 300,000,000.

(iii) Programu ya kuzisaidia Serikali za Mitaa (*Local Government Support Programme (LGSP*) shilingi 200,000,000/=.

(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa shilingi 602,000,000/=. Hivyo kufanya jumla ya matumizi kufikia shilingi 1,602,000,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi hapo juu, Semina Elekezi ya Ngurdoto ilikuwa ni sehemu ya kujenga uwezo kwa Viongozi ili kusaidia kuimarisha utendaji kazi Serikalini. Mafanikio katika utendaji yanaonekana wazi. Tutakubaliana wote kuwa mafanikio hayo hayakutokana na Semina Elekezi ya Ngurdoto pekee. Baada ya semina hiyo zilifuatia semina nyingine pamoja na mafunzo mbalimbali. Madhumuni makubwa ni kutekeleza kazi za Serikali kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Semina hiyo imewasaidia Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu wa Tawala za Mikoa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika utendaji kazi wao. Mada zilizowasilishwa zililenga katika utawala bora, mikakati ya kuboresha utendaji kazi Serikalini na ukuzaji wa uchumi na maendeleo ya jamii. Hivyo, Semina hivyo ilisaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha uongozi wa pamoja, usimamizi wa utendaji, uwajibikaji na udhibiti wa raslimali ndani ya Serikali kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake katika ngazi zote ili kuzidi kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Ni dhahiri kwamba mafunzo yoyote yana gharama, lakini kikubwa ni kuhakikisha mafunzo hayo yanachochea maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilivyokuwa nafahamu mimi ni kwamba Wabunge wa CCM ni asilimia 69 na siyo asilimia 80. Naomba sasa niulize swali langu.

(a) Licha ya Semina hiyo Elekezi ya Ngurdoto bado Semina Elekezi, Warsha na Kongamano yanaendelea na hata juzi tu swali kama hili liliulizwa. Kwa hiyo, ni fedha nyingi sana zinatumika ambazo zingeweza kufanyia mambo mengine. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba Semina Elekezi hiyo ya Ngurdoto haikuwa na tija yoyote ndiyo maana mpaka leo Semina na Warsha zinaendelea?

(b) Kwa nini Serikali isipunguze warsha hizo na semina badala yake iweke utaratibu maalum wa mafunzo yenye tija ambayo yanaweza kusaidia utendaji kazi kuliko ilivyo hivi sasa warsha na kongamano imekuwa ni kero? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nia ya Semina ya Ngurdoto ilikuwa ni kutoa dira na mwelekeo wa Serikali ya Awamu Nne, na tuelewe kwamba mwajiri yeyote anapomwajiri mtu anataka tija katika Shirika lake au Taasisi yake. Kwa hiyo, hata Serikali ya Awamu ya Nne ilitoa Semina Elekezi ili kutoa mwelekeo na dira; na hata kwenye ajira unapomwajiri mtumishi unatoa *Introduction course, orientation* ili huyo mwajiriwa afuate matakwa ya shirika lako au Taasisi yako. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais aliona ni vyema kutoa Semina Elekezi ili kutoa mwelekeo na dira kwa Awamu ya Nne ya uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu (b) kero kwa upande wa semina na kongamano. Waheshimiwa Wabunge, ni ukweli usiyofichika kwamba semina na kongamano hazitolewi kiholela tu zinakuwa na mada maalum na zinakuwa na malengo maalum.

Kwa hiyo, semina hizo kama semina za UKIMWI na Semina za Waheshimiwa Wabunge kujua mwelekeo wa Serikali zote zinaleta tija na siyo kubomoa. Mimi ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tusiziponde sana hizo semina bali tuelewa kwamba ni nia nzuri ya Serikali katika kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani inatosha, tunahamia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Na. 31

**Kuwaendeleza Vijana Kimichezo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kuimarisha na kuongeza viwango vya michezo nchini kama vile mpira wa miguu, mpira wa pete *(netball)*, riadha, kareti, mpira wa kikapu n.k.; na kwa kuwa, vijana wengi wenye vipaji vya michezo wako Mikoani, Wilayani na Vijijini:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwatafuta vijana hao na kuendeleza vipaji vya michezo walivyo navyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa makofi mazuri ya kuashiria mambo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, kwa ruhusa yako nikuombe uniruhusu nitoe salam ama nitoe tamko la kuishukuru timu yetu ya Taifa kwa kubeba bendera vizuri katika kutetea Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, mtakumbuka tarehe 14 Juni, 2007 kwa niaba ya Serikali aliwakabidhi vijana bendera ya nchi ili waendelee katika kutafuta nafasi ya kushiriki katika finali za Kombe la Mataifa Uhuru ya Afrika kule Burkinafaso. Vijana hao wamefanya kazi nzuri, nyie wote ni mashahidi wameweza kutupatia ushindi wa goli moja bila na kutuweka katika mazingira mazuri ya kuweza kuendelea katika mashindano hayo.

Naomba nitoe salamu hizo kwa niaba ya Waziri wangu na kwa niaba ya Serikali tuwapongeze kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri ya kulitetea Taifa na kuiletea heshima nchi yetu. Naomba tuwaunge mkono tuwachangie ili waweze kufanya vizuri katika mechi ya mwisho tarehe 2 Septemba, 2007 tuwakungute Msumbiji magoli mengi ili tu-*qualify* kwenda Ghana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kuendeleza na kuimarisha vipaji na kukuza viwango vya michezo yote hapa nchini. Kwa sasa Wizara yangu inaendelea na kutoa mafunzo mbalimbali kwa viongozi wa michezo katika kutambua vipaji kwa vijana nchini kote.

Mheshimiwa Spika, ni vema ieleweke kuwa kukuza michezo kwa kuendeleza vipaji vya vijana ni njia mojawapo tu katika kuimarisha michezo. Zipo njia nyingine kama vile ujenzi wa viwanja, upatikanaji wa vifaa vya michezo na walimu wa michezo ambao ni nyenzo muhimu katika kuendeleza michezo.

Mheshimiwa Spika, mikakati ambayo Serikali inatekeleza kuwatafuta vijana katika kuendeleza vipaji vya michezo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kushirikiana na vyama vya michezo na taasisi mbalimbali katika kuhakikisha kwamba klabu za michezo zinakuwa na timu za vijana.

(ii) Kufufua na kuendeleza michezo ya shule za msingi (*UMISHUMTA*), shule za sekondari (*UMISETA*) na mashindano ya vyuo.

(iii) Vyama vya michezo nchini kuwa na *programme* maalum za muda mfupi, muda wa kati na mrefu katika kuendeleza vijana.

(iv) Kuwa na shule maalum za michepuo ya michezo hapa nchini.

(v) Serikali Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na watu binafsi kuanzisha vituo maalum vya kufundisha michezo *(sports academic)*

(vi) Kusaidia *Tanzania Association of Youth Soka Academies (TAYSA)* ambacho ni chombo kinachosimamia maendeleo ya kuendeleza vipaji vya vijana na kuandaa mafunzo na mashindano mbalimbali hapa nchini.

(vii) Lipo shindano la *Copa Coke cola* ambalo hushindanisha vijana wa chini ya umri wa miaka kumi na saba (17) katika mpira wa miguu kwa Mikoa yote nchini Tanzania. Shindano hili linadhaminiwa na Kampuni ya *Coca cola* na kusimamiwa na *TFF* na wataanza tarehe 20 Juni, 2007 na vijana 700 watakusanyika wote Dar es Salaam.

(viii) Serikali kwa kutambua umuhimu wa vipaji vya michezo ya vijana imemwajiri kocha wa mpira wa miguu (vijana) toka Brazil, na Serikali itaendelea kufanya hivyo kwa michezo mingine yote hapa nchini.

(ix) Aidha, Serikali inacho Chuo cha Maendeleo ya Michezo katika Mkoani Mwanza, Malya kinachotoa mafunzo mbalimbali ya michezo ikiwemo Stashahada maalum ya utambuzi wa vipaji vya vijana katika michezo mbalimbali.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa. Vilevile naomba niipongeze *Taifa Stars* kwa ushindi mzuri walioupata na kuonyesha umahiri wao ingawa kocha alipata kadi nyekundu pamoja na mchezaji mwingine. Lakini vilevile walionyesha umahiri wao na wakafunga goli. Kutokana na hali ya kocha alivyokuwa mzuri na mahiri. Je, Serikali ina mkakati gani kuchukua makocha kutoka Mikoani na Wilayani ili waweze kuja kufundishwa na kocha huyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli alichozungumza, Chama cha Mpira *TFF* kinayo programu maalum kabisa ya kumtumia kocha huyo. Kocha Maximo atakuwa anatumika katika ufundishaji Timu ya Taifa na pia kufundisha makocha katika nchi yetu. Wanayo programu ambao wameiandaa kwa kocha huyo kufanya kozi mbalimbali. Kozi ya awali *preliminary*, kozi ya kati *intermediate*, kozi ya juu *advanced* na kozi nyingine na atakuwa anatembea Mikoa mbalimbali kuhakikisha kwamba angalau kila timu inapata kocha ambaye anastahili na mwenye sifa. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vipaji vya vijana vinavyoonekana hasa wanapokuwa katika shule za msingi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvitambua na kuviendeleza vipaji hivyo katika shule za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi ni kwamba Serikali kwa kutambua kwamba vipaji vinaanzia kwenye umri wa utoto na kuna usemi unaosema samaki mkunje angali mbichi. Serikali inalitambua hilo na Serikali imeamua kufufua mashindano ambayo yalikuwa yamekufa katika shule za msingi, shule za Sekondari na katika Vyuo. Hiyo ni ishara ya kuonyesha kwamba Serikali inajali na kutambua vipaji na ndiyo maana tumekuwa na kocha huyo ambaye naye atapita katika mashindano hayo yatakayofanyika. Wale vijana ambao watakuwa na vipaji vimejionyesha watachaguliwa ili kuwa na timu ambayo ni ya Taifa ya Vijana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED R. SOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante**.** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vijana tunaowatumia ni vijana ambao wengi wanajishughulisha na shughuli zao tu za kimaisha. Inaonaje Wizara hivi sasa ikawaajiri ili kuweza kuwatumia vizuri kwa *time* yoyote wanapowataka badala ya kuvunja kambi na kurudisha kambi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli alichokizungumza ni kwamba sisi katika Tanzania mpaka sasa hivi tuna *practice* mpira wa kulipwa *semi professional* na pia tuna *amateur* wachezaji ambao wanafanya shughuli nyingine na wanacheza michezo; na vijana wetu hawa wengi wao wameajiriwa katika Makampuni yao na wengine hawajaajiriwa. Ni nia yetu sisi kama Serikali kuhamasisha na kuona kwamba michezo inakuwa sehemu ya ajira. Kwa hiyo, tunajaribu kuyahamasisha Makampuni mbalimbali yaweze kuwaajiri wachezaji wetu hao na sisi kama Serikali tuna utaratibu wa kufanya kuhakikisha kwamba mwenye uwezo na kipaji chake na mwenye uwezo wa kufanya kazi mahali basi tuweze kumsaidia apate ajira ili aweze kulitumikia Taifa vizuri.

Na. 32

**Tatizo la Maji Sikonge**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa kasi ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kufikia asilimia 65 (65%) ya huduma ya maji na malengo ambapo kwa sasa ni asilimia 11 (11%) kwa Sikonge:-

(a) Je, juhudi gani zitafanyika hasa katika Kata ya Kipiri, Kitunda, Kiloli na Mji wa Sikonge ili kuwapunguzia shida ya maji ambayo ni kero kubwa wakati wa kiangazi?

(b) Je, Serikali ina jitihada gani za kupandisha kiwango cha asilimia ya upatikanaji wa maji safi na salama katika Wilaya zilizopo chini sana ya kiwango kama Sikonge?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wilaya ya Sikonge ina Tarafa mbili za Sikonge na Kiwele. Hadi mwezi Machi 2007, kati ya watu 132,733 wanaoishi Wilayani Sikonge ni asilimia 11.5 ndiyo wanaopata huduma ya maji. Aidha, katika mji wa Sikonge ni asilimia 24 ya wakazi wote ndiyo wanapata huduma ya maji. Hivyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kuelekeza miradi ya maji katika Tarafa ya Kiwele. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali ilijenga visima vinne katika vijiji vya Majojoro 1, Mwitiko 1 na Mgambo 2. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya imejenga visima sita kwenye Kata ya Kipiri katika vijiji vya Kilumbi vimejengwa visima 3, Zugimlole visima 2 na kisima 1 kilijengwa katika kijiji cha Mgambo (Kata ya Kitunda). Aidha, mradi wa maji wa Ipole unaohudumia vijiji vya Ipole na Udongo katika Kata ya Ipole ulikarabatiwa kwa gharama ya shilingi milioni 30. Juhudi hizo zimepunguza shida ya maji katika maeneo niliyotaja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imetenga shilingi milioni 12 kwa ajili ya uchimbaji wa visima vifupi 4 katika Sekondari za Sikonge 1, sekondari ya Igigwa Kisima 1, sekondari ya Malampaka kisima 1 na sekondrai ya Kipiri kisima 1.

Aidha, Serikali imepanga kujenga mabwawa ya maji kwa kupitia Mpango shirikishi wa jamii *(PADEP)*. Mpango huo utahusisha vijiji 7 vya Tarafa za Kiwele (Mwitiko, Igugwa, Mgambo, Mwenge, Majojoro, Kilumbi na Zugimlole) na vijiji 12 vya Tarafa ya Sikonge (Malampaka, Usunga, Ukangamoyo, Utimle, Idekamiso, Udongo, Tumbili, Ibaya, Kasandalala, Mole, Mpombwe na Usesula).

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mabwawa hayo umekadiriwa kugharimu shilingi milioni 360. Uchimbaji wa visima 24 utafanyika pia kwa gharama ya shilingi milioni 283 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. Vijiji vitakavyohusika ni Mgambo, Mwenge, Majojoro, Kilimbi na Zugimlole katika Tarafa ya Kiwele, lakini pia na Pangala, Igigwa na Kisanga katika Tarafa ya Sikonge. Aidha, uchimbaji wa visima 2 utafanyika katika vijiji vya Majojoro katika Kata ya Kiloli na Mgambo katika Kata ya Kitunda kwa msaada wa fedha kutoka katika Kampuni ya Uwindaji ya Kitalii

inayodhaminiwa na *Coolman Wild Life Fund.* Utekelezaji wa mipango hiyo utapunguza shida ya maji Wilayani Sikonge.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itakayotekelezwa hadi kufikia mwaka 2025. Katika programu hiyo, Halmashauri za Wilaya zitapewa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali iliyopangwa na Wilaya zenyewe. Ugawaji wa fedha kwa Wilaya mbalimbali utazipa kipaumbele Wilaya ambazo viwango vyake vya huduma ya maji viko chini. Utaratibu huo ni jitihada za Serikali za kuweka uwiano mzuri wa kupandisha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya zenye viwango vya chini vya huduma hiyo ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Sikonge. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza na ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwanza, kwa kuwa Wizara iliahidi kutoa fedha za *Quick Wins* kwenye miradi kadhaa ya maji nchini kwenye Wilaya kadhaa ikiwemo Sikonge. Lakini mpaka sasa hivi fedha hizo hazijafika kwenye Wilaya, na mimi nina hakika kabisa kwamba fedha hizo zingefika zingeweza kukamilisha miradi yetu mingi sana ya maji kama alivyoiorodhesha. Je, ni lini Serikali inaahidi kwamba fedha hizo zitakuwa zimefika ili ziweze kusaidia kukamilisha miradi kwa Wilaya ya Sikonge na kwa Wilaya kadhaa ambazo Wizara ilikwishaahidi?

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Shukuru Kawambwa alishatoa ruksa kwa Naibu Waziri kuja Sikonge ili niwe naye katika kuangalia matatizo ya maji kwenye Mji wa Sikonge na mpaka sasa hajafika Mheshimiwa Naibu Waziri. Naibu Waziri anasema vipi juu ya hili. Anakiuka maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wake au yuko tayari sasa kuja kukamilisha hiyo ziara ambayo alielekezwa na Mheshimiwa Waziri tukiwa pamoja naye?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu *quick wins* napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote waliomo humu kwamba fedha za *quick wins* zimeshafika na kwa hivi sasa fedha hizo zipo Wizara ya Fedha katika taratibu mbalimbali ili ziweze kuhamishwa tuletewe Wizara ya Maji tuanze taratibu za kuzisambaza katika kila Wilaya. Kwa taarifa ni kwamba jumla ya shilingi bilioni 19 ndizo zitatumika katika *quick wins* kwenye Wilaya yote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu mwaliko wa kwenda huko napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari tutawasiliana mimi na yeye tuweze kupanga kipindi gani muafaka ili niweze kufika huko. (*Makofi)*

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea na shughuli zetu nashangaa mara kwa mara Waziri huyu mnapenda kumwalika, sijui ni shida ya maji tu au aah basi. (*Kicheko)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini katika kuzungumzia hajazungumzia ile miradi ya *World Bank* maana yake wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa tuna miradi 10 na miradi hiyo katika vijiji vya Kisima, Uiyenzele, Chinyahuku, Makose, Singonali wanasubiri miradi hii kwa hamu sana ili waweze kufikia hatua ya asilimia zile zinazozungumziwa 65 katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Je, miradi hii fedha zake zitapatikana lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mpwapwa wana vijiji 10 ambavyo kwa jina maarufu tunaita miradi ya Benki ya Dunia. Lakini pia kabla ya hilo napenda kwamba niwape hongera Wilaya ya Mpwapwa kwa jinsi walivyotekeleza miradi 10 ya awali ya vijiji 10 katika Wilaya yao ambapo kwa kweli walifanya vizuri sana na ni imani yangu kwamba na hii miradi 10 mingine watafanya kwa njia kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kujibu swali lake napenda kumfahamisha kwamba taratibu bado zinaendelea na ni imani yangu kwamba katika kipindi hiki kipya cha mwaka wa fedha ni kwamba taratibu zitakamilika na miradi yote ambayo itakuwa chini ya *World Bank* tutaweza kufanikiwa kupata fedha. Kwa hivi sasa taratibu iliyopo ni kwamba tunahitaji kwanza *guarantee* na pia vijiji vyote ikiwemo Wilaya zote kwa kupitia Halmashauri zao waweze na wenyewe kwamba kusaini mikataba maalum; na mikataba hiyo ndiyo sasa hivi inasambazwa. Baada ya mikataba hiyo ndiyo hatua hiyo itakwisha na hatua zitakazofuata kwa kufuatana na utaratibu wa *World Bank* tunaweza tukafikia hatua ya kupata hizo fedha.

Na. 33

**Kenya Kutangaza Vivutio vya Tanzania kuwa Vyake**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi jirani hutangaza baadhi ya sehemu za nchi yetu zenye vivutio vya kitalii kwamba ni zao; na kwa kuwa, wanathubutu hata kutangaza kuwa, Mlima Kilimanjajro na Visiwa vya Zanzibar kuwa ni sehemu yao; na kwa kuwa, hivi sasa wanatangaza kuwa, hata Mbuga ya Serengeti ni yao pia:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhakikisha kuwa, wahusika wanaacha kabisa kutangaza sehemu za nchi yetu zenye vivutio vya utalii kuwa vya kwao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, ningependa kutoa maelezo mafupi kuhusu chimbuko la nchi hiyo jirani ambayo ni Kenya kuvitangaza baadhi ya vivutio vyetu kwamba ni vya kwao. Wakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, kitovu cha utalii Afrika ya Mashariki kilikuwa Kenya, jijini Nairobi. Karibu ndege zote zilizokuwa zinaleta watalii

zilitua Nairobi na watalii wengi walishuka huko na baadaye kuelekea kwenye maeneo mengine ikiwa pamoja na Tanzania. Katika utaratibu huu ilikuwa ni rahisi kuwadanganya wageni kwamba vituo hivyo wanavyokwenda kuviona viko nchini kwao. Baadhi ya vivutio hivyo ni:-

(i) Mlima Kilimanjaro ambao hapo zamani wataliii walikuwa wanaupanda kupitia hata Kenya.

(ii) Hifadhi ya Serengeti ambayo ina ikolojia inayoshirikiana na Masai Mara. Watalii walikuwa wanaingia wakitokea Kenya na kupitia geti la Bologonja. Mambo hayo mawili ndiyo hasa yaliyochangia kumfanya mgeni kuhisi kuwa vivutio hivyo anavyokwenda kuona viko nchini Kenya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hoogan, kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaotoa taarifa hizo potofu mpaka sasa, Serikali kupitia Wizara yangu na Wizara nyingine husika imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kubadilisha utaratibu wa kupanda Mlima Kilimanjaro kwa kupitia upande wa Tanzania peke yake. Hivyo basi mtu yeyote anayehitaji kupanda Mlima Kilimanjaro hana budi kufika Tanzania.

(ii) Kufunga geti la Bologonja huko Serengeti kama sehemu ya kupitia watalii na kuwaelekeza watalii kupitia katika mipaka ya Sirari, Namanga na Holili.

*(iii)* Kurejesha kauli mbiu ya Bodi ya Utalii toka *Authentic Africa* na kurudi kwenye ile ya Tanzania *(The Land of Kilimanjaro and Zanzibar)*. Hii inahusu pia kurekebisha machapisho yote na matangazo ya utalii kama yale ambayo yamejitokeza katika siku za karibuni katika magazeti ya kimataifa ya *Travel World News, The New York Times Magazine* ya Marekani na *Africa and Travel Magazine of Canada.*

Mheshimiwa Spika, aidha, mikakati imewekwa ya kutangaza kwa bidii vivutio vyetu vya utalii na mahali vilipo ikiwa ni pamoja na kutangaza kwenye makala maalum za magazeti yanayochapishwa mjini London ya Jambo huko Uingereza, kupitia matamko ya viongozi wetu mbalimbali wa Tanzania na Watanzania kwa ujumla. Ni mategemeo yangu kwamba hali hii itaonyesha dhahiri mahali vivutio hivi vilipo na kufuta fikra hizi potofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua ni kuyashawishi Mashiriki ya nje na ndege kuanzisha safari za kuja

moja kwa moja Tanzania. Hivi sasa Mashirika yafuatayo ya ndege yanakuja Tanzania moja kwa moja:-

- Shirika la Ndege la Uholanzi (*KLM);*
- Shirika la Ndege la Uingereza *(British Airways);*
- Shirika la Ndege la Ethiopia *(Ethiopian Airlines);*
- Shirika la ndege la Falme za Kiarabu *(The Emirates);*
- Shirika la Ndege Qatar *(Qatar Airways);*
- Shirika la Ndege la Afrika Kusini *(South African Airways (SAA);* na
- Shirika la Ndege la Uswisi (*Swiss Air),* zinakuja Tanzania moja kwa moja.

Serikali inazungumza na Mashirika mengine ili nayo yaanzishe safari za moja kwa moja kuja Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe Mosi Agosti mwaka huu, Serikali itaanza kutangaza vivutio vya Tanzania kwenye televisheni ya *CNN* kwa ajili ya soko la ndani la Marekani na Canada. Matangazo haya yatahusu kuweka vivutio vya Tanzania katika Tovuti ya *CNN Travel*, na yatahusu kutangaza katika *CNN Headline News* na katika viwanja vya ndege 54 vya Kimataifa ndani ya Marekani. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Wizara imetenga fedha za kuendelea kuutangaza utalii na vivutio vya Tanzania katika magazeti makubwa katika nchi za Marekani, Ulaya na China.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa hatua hizi zitatoa uelewa zaidi kwani mambo yatakuwa hadharani na hatimaye kuwafanya majirani zetu waache kutoa taarifa potofu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipongeze hatua ambazo Wizara inazichukua katika kuhakikisha kwamba vivutio vya kitalii vya Tanzania vinatangazwa ipasavyo.

Lakini kwa kuwa sasa hivi dunia ni ya ushindani na sasa hivi Wakenya hawatangazi tena kwamba Mlima wa Kilimanjaro upo kwao wanasema ukitaka kuuona Mlima wa Kilimanjaro njoo Kenya, ukitaka kupanda Mlima wa Kilimanjaro nenda Tanzania. Afrika ya Kusini wanasema karibu Johannessburg masaa matatu tu kutoka Mlima wa Kilimanjaro. Sasa je, Serikali inajiandaa vipi kupambana na lugha za namna hii za kiushindani wa kibiashara ili kuendelea kuhakikisha kwamba vivutio vyetu bado watalii wanakuja Tanzania moja kwa moja badala ya kupitia Kenya na Afrika ya Kusini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba dunia sasa ni ya utandawazi na kwamba kila mtu anataka kutumia kitu ambacho kinaweza kuleta mvuto ili aweze kupata biashara. Sisi la kwetu kubwa ambalo ni lazima tufanye tuhakikishe dunia inaelewa Kilimanjaro iko Tanzania na hawa watu wa Afrika ya Kusini wanaosema uje Johannessburg ni masaa matatu tu kwenda Kilimanjaro wajue kwamba ni saa tatu kutoka huko Johannessburg kwenda Tanzania.

Hiki ndicho cha muhimu sana. Wataendelea pia wengine kusema uje Johannesburg baada ya saa tatu tutakufikisha katika Visiwa vya *Spices* vya Zanzibar (*Spice Island of Zanzibar*). Hili hatuwezi kuepuka sana lakini tuhakikishe kwamba kila mtu anajua *Spice Island of Zanzibar* ziko Tanzania na siyo mahali pengine popote ila Tanzania tu.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, uongo wa nchi jirani kwamba baadhi ya vivutio vya utalii vilivyoko katika nchi yetu uongo huu ni wa muda mrefu na hasa kuhusiana na Kilimanjaro. Lakini ni juzi juzi tu hapa mbuga ya Serengeti imetangazwa kama *World Heritage Sign* na bado wakasema iko kule Kenya.

Lakini sisi tunatangaza utalii kupitia *TTB, TATO, Ngorongoro Conservation Area Authority*, *TANAPA,* kupitia Balozi zetu huko nje sasa huu uongo kwa nini uendelee? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Nadhani hakuna haja ya jibu, Mheshimiwa ameonyesha uchungu wake tu kwamba uongo huu unaendelea mpaka lini. Kwa hiyo, nadhani Serikali mmesikia.

Na. 34

**Mkandarasi Barabara ya Somanga – Ndundu**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu ilitamka Bungeni kwamba barabara ya Somanga – Ndundu itakabidhiwa kwa Mkandarasi mwezi Januari, 2007.

Je, ni lini sasa Mkandarasi huyo atapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakati wa Kikao cha Bunge lako Tukufu cha tarehe 4 Julai 2006, Wizara yangu ilijibu swali namba 143 la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, kuwa Wizara ingekuwa imesaini Mkataba na Mkandarasi ifikapo Novemba 2006. Mchakato wa kumpata Mkandarasi ulikwenda vizuri ambapo zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii zilipokelewa mnamo tarehe 31 Oktoba 2006.

Lakini kutokana na sababu zisizojulikana ni Mkandarasi mmoja tu aliyeleta zabuni hadi siku ya mwisho kati ya Makandarasi sita waliokuwa wamepita kwenye mchujo wa kwanza *(pre-qualification)* na kuchukua nyaraka za zabuni.

Baada ya uchambuzi wa zabuni hiyo pekee iliyoletwa kufanyika, matokeo yalionyesha kuwa zabuni ya Mkandarasi huyu ilikuwa kubwa sana na kuifanya Serikali isiweze kuingia mkataba na Mkandarasi huyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hii, Wizara iliwasiliana na Mfadhili wa mradi huo ambaye ni *Kuwait Fund* ikimfahamisha matokeo ya uchambuzi wa zabuni pekee iliyopokelewa na mapendekezo ya Wizara ya kutaka kutangaza zabuni upya. *Kuwait Fund* walikubaliana na mapendekezo ya Wizara ya kutangaza upya zabuni ya ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 21 Machi, 2007 Wizara ilitangaza upya zabuni ya ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga. Zabuni zinatarajiwa kufunguliwa kesho yaani tarehe 19 Juni 2007 na Mkataba wa ujenzi unatarajiwa kusaini mwezi Agosti 2007.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa sasa hivi kuna matengenezo madogo madogo ya dharura yanafanyika huko kwenye barabara ya Somanga-Ndundu, lakini haya matengenezo hayako kwenye ubora wa *standard.* Je, Waziri anafahamu kwamba linalowekwa pale ni tope sio kifusi. Atatuhakikishiaje sisi barabara hiyo inatengenezwa kwa ubora? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hiyo hasa wakati wa mvua zilizonyesha hivi karibuni iliharibika sana. Wizara yangu kupitia *TANROADS* imefanya matengenezo na hasa upande wa Mkoa wa Lindi, matengenezo yaliyofanyika yaliridhisha.

Lakini ni kweli kwamba upande wa Pwani matengenezo hayakuridhisha. Ni kipande kirefu kidogo lakini kutokana na ufinyu wa fedha eneo lile hasa la Muhoro limekuwa likileta matatizo makubwa.

Lakini katika kuomba fedha zile za dharura mkoa wa Pwani uliidhinishiwa fedha ambazo zipo zinaendelea kutumika, sasa ubora wa barabara kwa kweli unategemea na fedha zenyewe zilivyo. Kama fedha hazitoshi huwezi kufanya matengenezo ya ubora mkubwa sana.

Hata hivyo ni mategemeo yangu kwamba suala hili tumelichukua ili kuhakikisha kwamba eneo hilo analolizungumza kwamba wanaweka udongo tu na sio changarawe liweze kuboreshwa na barabara iweze kupitika wakati wote. *(Makofi)*

Na. 35

**Matokeo ya Mitihani**

**MHE. SUSAN A. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa matokeo ya mtihani wa *Form IV* na *Form VI* yameonyeshwa kuwa, Shule za binafsi hususan za Misheni zimeshika nafasi za juu huku zile za Serikali zikifanya vibaya:-

(a) Je, matokeo haya yamesababishwa na nini;

(b) Je, Serikali inajipangaje ili kubadili matokeo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUM B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo na kwa ruhusa yako naomba kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi, viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa kwa namna ya kipekee walivyotufariji mimi na familia yangu wakati wa msiba mzito wa marehemu baba yangu. Mwenyezi Mungu awajaze kheri wote na tumwombe Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. (*Amin)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Shule za Misheni zilishika nafasi ya kwanza katika Mitihani ya Kidato cha 4 mwaka 2006 na Kidato cha 6 mwaka 2007, Shule za Serikali hazikufanya vibaya katika Mitihani hiyo. Matokeo ya Mitihani ya Kidato cha 4, wanafunzi 12 waliofanya vizuri zaidi 6 walitoka katika Shule za Serikali na 6 walitoka Shule za Misheni wote walifaulu katika darala la I. Katika Mitihani ya Kidato cha 6, kati ya shule kumi bora Kitaifa, 2 ni Shule za Serikali. Kati ya wanafunzi wasichana 10 waliofanya vizuri, 4 walitoka Shule za Serikali. Kati ya wanafunzi wavulana 10 waliofanya vizuri, 4 walitoka Shule za Serikali. Aidha, wanafunzi 3 wa kwanza katika kufaulu walitoka katika Shule za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kigezo cha kufaulu katika daraja la I – IV, kwa ujumla ufaulu katika Mitihani wa Kidato cha 6 Mwaka 2007 ulishuka kwa asilimia 6.1, ambapo watahiniwa 29,239 sawa na asilimia 87.21 ya waliofanya mtihani walifaulu, ikilinganishwa na mwaka 2006 ambapo watahiniwa 25,041 sawa na asilimia 93.31 walifaulu.

Ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha 4 mwaka 2006 ulishuka kwa asilimia 1.26, ambapo jumla ya watahiniwa 116,647 sawa na asilimia 82.30 walifaulu ikilinganishwa na

watahiniwa 102,064 sawa na asilimia 83.56 waliofaulu mwaka 2005. Kushuka kwa matokeo hayo ni kwa shule zote za Serikali na Zisizo za Serikali. Zoezi linaloendelea hivi sasa ni kutathmini ili kubaini maeneo na sababu zilizosababisha kushuka kwa ufaulu huo katika shule zote kwa lengo la kuchukua hatua za kurekebisha.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuinua ubora wa ufaulu katika Shule za Sekondari za Serikali, baada ya Wizara kubaini sababu za wanafunzi kutofanya vizuri katika mitihani, miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na:- Kuboresha ufundishaji kwa kuwapeleka katika mafunzo ("*In-Service Training*") walimu wa masomo yatakayobainika kuwa wanafunzi wamefanya vibaya.

Aidha, Wizara inaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa, kuajiri walimu zaidi, kujenga maabara, maktaba na nyumba za walimu katika Shule za Sekondari za Serikali kulingana na uwezo wa kifedha.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, suala langu la kwanza ni kwa kuwa mazingira ya Shule za Sekondari na za Serikali hasa zinazojulikana maarufu kama *Saint Kata* zitakuwa na mazingira mabovu sana kwa mfano hazina walimu wala Maabara. Je, Serikali inategemea kutengeneza wanasayansi wa aina gani?

Kwa kuwa hata zile shule tunazozijua kwamba ni za vipaji maalum kama *Tabora Boys and Girls,* Kilakala, Kibaha pamoja na Msalato nazo hazikung'ara kabisa katika matokeo ya mitihani hiyo. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu hilo wakati tunajua kabisa shule hizo zina maabara nzuri na walimu. Je, Serikali inatuambia nini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, la kwanza Serikali imejipanga na naomba nitangulize kwa kushukuru Serikali kuipatia Wizara ya Elimu kipaumbele. Ni matarajio yetu kwamba kiasi kile cha fedha kilichowekwa kwenye Wizara ya Elimu madhumuni yake makubwa ni kuboresha shule hizi pamoja na nyingine ambazo zilijengwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shule za vipaji naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba shule hizi sasa zimeboreshwa, zimeongezewa fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye vifaa vya kufundishia na kujifunzia maabara, maktaba na ukarabati mzuri wa majengo ili wanafunzi pamoja na walimu wapate fursa nzuri ya kujifunza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliomba Bunge lako Tukufu kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa pamoja na wananchi kwa shule hizi ambazo zinaitwa *Saint Kata.* Kwa kutumia lugha namna hiyo tunaweza tukawakatisha tamaa. Shule hizi zimekuwa ukombozi mkubwa sana kwa wananchi walio wengi na ni vyema tukajifunza kwamba

Mapinduzi ya elimu lazima yaanze kwa namna yoyote ile na *quality* itatengenezwa na sisi wote pamoja. Naomba tushirikiane tusikatishane tamaa. Ahsante sana. (*Makofi)*

Na. 36

**Tatizo Sugu la Ajira Nchini**

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la ajira limekuwa sugu sio tu kwa Tanzania bali kwa nchi nyingi duniani na kwa sababu hiyo vijana wengi wa Kitanzania wamebuni kazi mbalimbali za kujiajiri kama ilivyo kwa vijana wengi wanaoishi mipakani mwa nchi yetu Tunduma na Ileje na Kasumulo na nchi jirani ya Malawi wanaofanya biashara ya Sukari; na kwa kuwa, vijana hao wanapoleta Sukari toka Malawi na kupeleka bidhaa nyingine huko hupata usumbufu wa vyombo vya dola vinavyosimamia sheria za nchi:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, sasa ni wakati muafaka kuandaa utaratibu nzuri wa kutoa vibali maalum kwa vijana kupitia Ofisi ya Mkoa wa Mbeya na *TRA* ili vijana hao wafanye biashara hiyo kihalali?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kwa kuwapatia vijana hao vibali vya biashara kutasaidia kudumisha zile ahadi za Mheshimiwa Rais katika utoaji wa ajira kwa raia na nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuona umuhimu wa vijana na wananchi kwa ujumla kufanya biashara iliyo halali nchini kote ikiwa ni pamoja na vijana wa Mkoa wa Mbeya kufanya biashara ndogondogo zilizo halali, Serikali imekuwa ikifanya marekebisho ya mara kwa mara kwenye Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972.

Mwaka 2004 sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho makubwa katika maeneo matatu yafuatayo:-

(i) La kwanza kuondoa ada za leseni kwa biashara zinazoanza kwa mara ya kwanza na zile ambazo mzunguko wake wa mauzo ni chini ya shilingi 20,000,000. Kwa leseni za biashara zilizokuwa zinaendelezwa na zenye mzunguko wa mauzo wa shilingi 20,000,000 na zaidi kwa mwaka wahusika walilipa ada ya leseni ya shilingi 20,000 tu.

(ii) La pili, leseni ikishatolewa inakuwa ni ya kudumu hadi hapo biashara itakapofika ukomo kwa hiari au kufilisika au kufutwa na sheria nyingine itakayotungwa baada ya hapo;

(iii) La tatu, kutoa Hati ya Mlipa Kodi *(TIN)* bure ambayo humwezesha mfanyabiashara kupewa leseni ya biashara bure itakayomwezesha kufanya biashara aliyoomba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa mwezi Februari mwaka huu Bunge hili Tukufu lilitunga Sheria nyingine ya Usajili wa Shughuli za Biashara (*Business Activities Registration Act*.) Hivi sasa Serikali inaandaa Kanuni za kutekeleza sheria hiyo na zitakapokamilika itaanza kutumika mapema mwaka huu wa fedha. Serikali inaamini hatua zilizozichukua na inazoendelea kuchukua zitaweza kuwahusisha vijana wetu na wananchi kwa ujumla kufanya biashara zao kihalali na kwa urahisi zaidi na hivyo kutoa ajira kwa wananchi walio wengi badala ya mtindo wa vibali ambavyo mara nyingi huwanufaisha wafanyabiashara wachache.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inahakikisha kuwa kila mfanyabiashara anafanya biashara kulingana na taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na kuwa na leseni na kulipa kodi au ushuru unaotakiwa.

Kwa hali hiyo kwa wale vijana Mkoani Mbeya wanaofanya biashara kihalali kwa kuingiza sukari toka nchi jirani ya Malawi kwa kufuata taratibu zinazokubalika na Serikali hawapati matatizo yoyote. Wafanyabiashara wanaoingiza sukari nchini isivyo halali kupitia njia za panya hukumbana na taratibu za kisheria ambazo *TRA* huzitumia kudhibiti ukwepaji ushuru.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa wafanyabiashara kufuata utaratibu uliowekwa ambao unawawezesha wafanyabiashara hao kurasimisha biashara zao ambazo zitatambuliwa kisheria na hivyo kuwawezesha kupata huduma nyingine kama mikopo na kadhalika.

Vile vile kupitia utaratibu huu wanachangia kwa kulipa kodi ndogo kwa Serikali kwa maendeleo ya Taifa letu.

**MHE. MOHAMMED IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika baada ya kupata majibu mazuri kutoka kwa Waziri muhusika naomba niulize mwaswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa vijana wengi wa nchi hii wanamatatizo ya kupata ajira na vijana wengi hasa wanaoishi mipakani wameonyesha mwamko wa kijiajiri wenyewe kutekeleza agizo la ajira milioni 1.0 ambazo mpaka leo hazijatakelezeka. Je, Serikali katika kipindi hiki ambacho kinasubiri kupitishwa kwa hiyo *Business Activities Registration Act* haioni kwamba kuna umuhimu wa kutoa vibali vya muda ili wabebaji wa sukari hiyo wanaotumia baiskeli, wanaofanya biashara isiozidi laki tano au milioni moja,

wakaruhusiwa kuwa nafuu watu wa vijiji hasa kwa vile Bajeti hii imepandisha kiwango cha mafuta na kusababisha bidhaa kwa upande wowote?

Mheshimiwa Spika, la pili. Kwa kuwa Bajeti ya mwaka huu imekuwa ni mwiba wa mchongoma kwa kila Mtanzania. Je, Serikali haioni,

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge hebu kaa kwanza. Waheshimiwa Wabunge hii ndiyo aina ya lugha ambayo haistahili kutumika hapa Bungeni. Ni lugha inayojaribu kuchochea wananchi na tuwaachie walio nje ya ukumbi huu wanaozungumza vijiweni watumie lugha kama hizi. Humu ndani ya Bunge siwezi kuruhusu na ninatoa tahadhari, nimeangalia kwenye vyombo vya habari, kuna lugha nyingine kwa kweli nadhani kuna watu wamepania tu kuichafua Serikali yetu. (*Makofi*)

Kwa sababu wanazungumzia Serikali ni tapeli, Serikali ni.. maneno ya namna hii yanakuja wapi. Haiwezekani kwamba hawa wenzetu waliopewa jukumu la kuongoza nchi yetu leo hii tuwageuzi kuwaita maneno ambayo hayana maana. Sitatazamia Bunge hili wananchi wanatutazamia tutoe hoja tuisaidie Serikali hii kama kuna jambo mbadala la namna sera inaweza kuendeshwa vizuri litolewe kwa hoja nzito. Sisi sote hapa ni mashahidi Serikali yetu ni sikivu na yakitolewa mapendekezo katika lugha ya uzalendo tu ya kuipenda nchi yetu, ninahakika tutafikia pazuri. Kwa hiyo, natoa tahadhari ya awali mtaniona kidogo sijui vipi lakini ukianza kusema bei zimepanda, bei zimepanda lini. Bajeti ndiyo imetangazwa juzi mtu anasema bei zimepanda na mengine Bajeti hii ni mkuki. Swali lililopo hapa ni tofauti kabisa. Ni suala la ajira Mbeya na kadhalika sasa unauliza mkuki. Kwa hiyo, nasikitika sana hata swali lenyewe Mheshimiwa Sanya nalifuta kwa sababu halituendelezi mbele zaidi. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 37

**Homa ya Bonde la Ufa**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu imeathirika sana na homa ya Bonde la Ufa "*Rift Valley Fever" (RVF):-*

(a) Je, homa hiyo iligundulia lini kwa mara ya kwanza hapa nchini na Serikali ilichukua hatua gani za kuufuatilia na kuudhibiti ugonjwa huo?

(b) Je, tangu ugonjwa huo ugundulike, kumekuwa na milipuko mingapi, lini na wapi imetokea hapa nchini?

(c) Je, katika milipuko iliyotokea, ni wanyama wangapi wa aina zipi walioathirika na kufa na ni watu wangpi walioathirika na waliokufa kutokana na milipuko ya homa hiyo (*RVF*)?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtaona naongeza muda kidogo kwa sababu kulikuwa na utaratibu wa matangazo ya taarifa mbalimbali na ku-*amend* ile *Order Paper*. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Dalili za ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (*RVF*) nchini Tanzania zilionekana mara ya kwanza mwishoni mwa mwezi Januari 2007 katika vijiji vya Engaresero, Monik, Masusu, Malambo, Piyaya, Nasongoyo na Ojbalbal katika Wilaya ya Ngorongoro Mkoani Arusha. Hata hivyo kabla ya matukio hayo Serikali ilikuwa imetoa tahadhari kwa wananchi kuhusu tishio la ugonjwa huo kupitia vyombo vya habari tarehe 19 Januari, 2007 baada ya ugonjwa kusikika upo nchi jirani ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamaoja na kufuatilia mwenendo wa ugonjwa ambapo mifugo ilikaguliwa na jumla ya sampuli 5,360 kuchukuliwa na kufanyiwa uchunguzi. Katika kuimarisha juhudi za kuudhibiti, Serikali imenunua chanjo kiasi cha dozi milioni tano na nusu kwa ajili ya kuchanja ng'ombe, mbuzi na kondoo, sanjari na kutoa elimu na kuhimiza wananchi kujikinga. Jumla ya shilingi 4,798,675,000 zilitolewa kwa ajili ya kazi hizi.Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuona uzito wa tatizo la ugonjwa wa Homa la Bonde la Ufa katika hotuba yake ya mwisho wa mwezi ya tarehe 31 Machi, 2007, alitoa maelekezo kwa wataalam na wananchi, ambayo yamesaidia sana katika kudhibiti ugonjwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba juhudi za Serikali zimezaa matunda na kwa sasa hakuna tena matukio ya ugonjwa kwenye mifugo.

(b) Tangu ugonjwa huu ugundulike kumeshatokea milipuko minane iliyosababisha mifugo kutupa mimba na vifo kutokea kwa mifugo na binadamu. Katika miezi ya Februari na Machi 2007 kulikuwa na matukio katika vijiji 26 vya Wilaya 10 za Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro na Tanga. Aidha, kwa kipindi cha Aprili na Mei 2007 matukio yalikuwepo katika vijiji 46 vya Wilaya 19 za Mikoa ya Dodoma, Iringa, Mbeya na Singida. Hadi tarehe 31 Mei 2007 ng'ombe 46,680 mbuzi 56,990 na kondoo 32,900 nchini walikuwa wameathirika ambapo kati yao ng'ombe 5,610 mbuzi 6,896 na kondoo 3,998 walikufa.

(c) Tangu ugonjwa utokee hadi tarehe 20 Mei, 2007 idadi ya watu wagonjwa ilikuwa imefika 306 ambapo 15 bado wako hospitalini, 156 walitibiwa na kuruhusiwa na 134 walifariki. Mikoa yenye wagonjwa waliofariki ni Arusha (3), Dodoma (85), Iringa (2), Manyara (4), Morogoro (13), Mwanza (4), Pwani (2), Singida (20) na Tanga (1). Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika Kama nilivyokwishaeleza, matukio ya ugonjwa yamekwisha na ninaomba kutumia nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuhamasisha wananchi kuhusu janga hilo.

Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wabunge, Madaktari wa Mifugo na Binadamu, wataalam wote waliohusika na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa juhudi walizofanya kuelimisha wananchi kuhusu ugonjwa huu na namna ya kujikinga kiasi kuwa sasa ni salama kula nyama hakuna hofu yoyote.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ugonjwa huu wa *Rift Valley* uligundulika nchini tangu 2006. Pamoja na kutoa chanjo lakini tukizingatia kwamba Tanzania ni nchi ambayo iko katika Bonde la Ufa. Je, Serikali imejenga maabara ngapi kwa sababu ugonjwa huu unaweza ukalipuka wakati wowote ni maabara ngapi zimejengwa nchini?

Pili, ukizingatia kwamba nchi yetu hasa vijijini wanategemea mifugo na kilimo. Je, Serikali imetengeneza *centres* ngapi za kufuatilia mwenendo wa Ugonjwa huu kama ilivyo *centres* za UKIMWI unavyoweza kufuatiliwa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo Mifugo ina maabara yake Kuu ya Taifa pale Temeke na ndiyo imekuwa ikifanya *co-ordination* katika kufuatilia suala hili. Maabara hii sasa hivi inavifaa vya kutosha vya kisasa vya kuweza kushughulikia sampuli zinazochukuliwa kutoka sehemu mbalimbali kuhusiana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baada ya wataalam wetu wa mifugo na wa Ikolojia kufanya kazi ya kufanya tathimini ya takwimu za kisayansi za muda mrefu, tumeweza kugundua kuwa ugonjwa huu huwa unatokea kila baada ya miaka saba mpaka kumi. Na kama hivi ndivyo sasa ugonjwa huu haupo unatarajiwa utokee tena miaka saba au mpaka kumi ijayo na Serikali imejizatiti kukabiliana na hali hii kwa kufuatilia mienendo ya hali ya hewa kila mwaka ili kuweza kuona hali inakwendaje kuhusiana na uwepo wa ugonjwa huu kwa siku za usoni ili kusudi tusiathirike tena na ugonjwa huu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haiwezekani kuendelea tena. Kwa hiyo ninayo matangazo machache. Kwanza nitaanza na wageni. Nitoe tu taarifa wale wote ambao pengine hawakuwepo wakati wa *briefing* na wamekuwa wakiniletea vikaratasi vya kueleza wageni sasa hivi, nimevirudisha kwa sababu huo sio utaratibu. Kama kuna mgeni meza inatakiwa ielewe siku moja kabla. Sio mtu anamwona mgeni wake pale halafu anaandika kwa Spika hapo hapo. Ni utaratibu ambao hauna ufanisi na pengine unakuwa mgumu sana. Sasa hawa wafuatao ni wageni ambao nilifikishiwa rasmi kwa hiyo nawatambua. Pale *Speakers Gallery*. Wapo wageni mashuhuru, ambao ni Mabalozi na Wawakilishi wa Nchi mbalimbali za kirafiki waliopo hapa Tanzania. *Your Excellences Ambassadors and High Commissioners and other Diplomatic Staff. I will be mentioning your names please when I mention the name stand up so that Members of Parliament can acknowledge you.* Wa kwanza ni Mheshimiwa Wolfgang Ringe, Balozi wa Ujerumani, ambaye kama mnavyofahamu sasa hawa ndiyo wameshika Urais, *the Presidency of European Union. (Makofi)*

Pia tunaye rafiki yetu, Mheshimiwa Tovard Akeson Balozi wa Sweden. Tunaye Mheshimiwa France Barn, Mkuu wa *European Commission*, tunaye pia Francisco Catania, Balozi wa Italia. Tunaye Mheshimiwa Carloy Van Casteren, Balozi wa Uholanzi. Tunaye Mheshimiwa Jacque De Labron Balozi wa Ufaransa, tunaye hapo hapo Mheshimiwa Riserd Marick Kiongozi wa Ubalozi wa Poland, tunaye Mheshimiwa Bi. Oliver Nagrey, ambaye ni Afisa wa Siasa Ubalozi wa Ireland, tunaye Mheshimiwa Rafiki yetu sana Mpendwa Philip Paharm Balozi wa Uingereza. Kwa kuwa ni rafiki yangu kifamilia nataka kusema, Philip *you very warmly welcome to the House. (Kicheko/Makofo)*

Tunaye pia Mheshimiwa Joma Pauk, Balozi wa Finland naona ametoka kidogo alikuwa pale na Mheshimiwa Janne Solensen Balozi wa Denmark. *We are very happy that you are here and you spare sometimes to see us in* Dodoma *we command what your Nations are doing in co-operation for development of Tanzania with us. Thanks very much.* Naomba niwatambua wanafunzi 62, kutoka shule ya Msingi ya *Holly Trinity* ya hapa Dodoma wamekuja na Walimu wao naomba msimame. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Jenista Mhagama, pamoja na Wabunge wengine wa Mkoa wa Ruvuma wameniomba niwatambulishe wageni wao ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaotoka Mkoa wa Ruvuma wamekuja kujifunza jinsi mjadala wa Bajeti unavyofanyika. Wale pale karibuni sana.

Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, ameniomba niwatambulishe Vijana wake ambao wanasoma Dar es Salaam nao wamekuja kujifunza jinsi shughuli zetu zinavyoendeshwa. Mmoja ni Justina na mwingine ni Stella wale pale. Karibuni sana. Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ukiacha Mheshimiwa Mwenyekiti wa Fedha na Uchumi Dr. Abdallah Kigoda wanaomba sasa hivi watoke na Naibu Spika, wakakutane hapo *Speakers Lounge* kwa Mkutano wa dharura. Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi na ukimwacha na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Mambo ya Bunge. Kwa hiyo wengine wote watoke kuna jambo ambalo halitachukua muda dakika tano watakuwa wamemaliza. Kwa hiyo waingie hapo waweze kushauriana.

Mheshimiwa Fatma Othuman Ali Katibu wa Umoja wa Wabunge wa CCM kutoka Zanzibar ameniomba niwaarifu kwamba Wabunge wote wa Umoja huo kutakuwa na Kikao leo baada ya kuahirishwa Bunge kipindi cha asubuhi katika Ukumbi namba 231, Kwa sababu hatuahirishi Bunge asubuhi tunasitisha tu ili tukutane tena jioni. Sasa hii nadhani maana yake nadhani ni baadaya maswali au ni saa saba. Haikukaa vizuri lakini nadhani mnaweza kushauriana ukumbina namba 231, Umoja wa Bunge wa CCM kutoka Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, leo tutapokea wageni ambao ni timu yetu ya Taifa inayotoka Burkina-Faso. Mtakumbuka kwamba nchi yetu imekuwa ikifanya vibaya kwenye michezo kwa miaka ya nyuma na hata katika huu mchezo wa soka kiasi kwamba Rais wa Awamu ya Pili aliwahi kusema nadhani kwa uchungu kwamba Tanzania ni kama

kichwa cha Mwendawazi kila anayetaka kunyoa basi anajaribu. Anayejaribu kwa kipande cha chupa kwa mkasi.

Lakini hali hiyo inaanza kubadilika na tunahaja kwa sababu wananchi Tanzania nzima wameonyesha kufurahishwa na matokeo ya timu yetu kule Ouagadougou na sisi kama wawakilishi wa wananchi tusingeweza kukaa kimya nashukuru sana Serikali imefanya utaratibu wameruka kwa ndege kutoka Mwanza walikotua usiku wa manane na nadhani kwa sasa hivi wamekwishatua hapa Dodoma kabla hawajaenda Dar es Salaam kwa hiyo kutakuwa na ratiba fupi ya kuwapokea humu ndani ya Bunge kama tunavyowapokea vijana wanavyofanya vizuri katika masomo basi na hawa nao wametupa heshima. *(Makofi)*

Kwa wale wasioelewa sana mambo ya soka mara ya mwisho nchi yetu ilishiriki kwenye fainali za kombe la Afrika ni  mwaka 1980. Kwa hiyo imepita miaka 27. Tunaomba mwaka huu tuweze kushiriki kule Ghana kwa hiyo si jambo dogo. Tuungane na vijana wetu pamoja na Kocha Maximo ili kuweza kuwapa moyo. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo basi nitamwomba Mheshimiwa Waziri Nchi Ofisi ya Waziri Kuu masuala ya Bunge asimame chini ya Kanuni ya 124 ili kufanya mambo mawili kwanza waruhusiwe kuingia, kwa sababu tumewapangia viti humu na pili aweze kuahirisha mjadala katika wakati ambao utakuwa unafikia kwa sababu sasa tuna mjadala wa Wizara ya Fedha chini ya Kanuni ya 56 inaruhusu kuahirisha mjadala kwa tukio maalum kwa kipindi maalum ambacho si zaidi ya nusu saa. Mheshimiwa Waziri wa nchi..

**Hoja ya Kutengua Kanuni ya 124 na 56**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, BUNGE (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kama ulivyokwishasema kwamba vijana wetu wa *Taifa Stars* Maarufu kama *JK Boys*, watapita hapa Dodoma wakielekea Dar es Salaam baada ya kurudi na ushindi kutoka Burkina Faso naomba kwa heshima na taadhima kwa mujibu wa Kanuni 124 niweze kutengua Kanuni ya 114 Fasili ya Kwanza kuwaruhusu vijana hawa na Mwalimu wao waweze kuingia katika Bunge hili. Aidha kwa mujibu wa Kanuni ya 56 Fasili ya kwanza naomba mara watakapoingia mjadala wowote utakaokuwa unaendelea uahirishwe ili tuweze kuwapongeza kwa niaba ya Watanzania wote na kuwapa hamasa na ari waweze kuendelea kufanya vizuri ikiwa ni pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa aliyoifanya kwa ajili ya kuendeleza michezo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni ya 124 na 56 ilipitishwa naBunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja hiyo imeamuliwa kwa asilimia mia moja, basi *Sergeant-At-Arms* wakati tutakapopata ishara vijana wakishafika tutaingia kwa utaratibu huo kwa kipindi kama cha nusu saa hivi. Sasa tuendelee na shughuli nyingine.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR**: Mwongozo wa Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mudhihir.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, kutokana na maneno mazuri uliyoyazungumza kuhusu timu yetu. Je, lisingekuwa jambo jema kwa ruksa yako nikapendekeza kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba kwa sababu vijana wetu wametung'avya uso katika medani ya soka tukapendekeza kuchangia posho yetu ya siku moja ili kuwafuta jasho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mudhihir wewe hujui kusoma vitendawili. Nimeiomba Kamati ya Uongozi ikutane kwa sababu tunatumia Demokrasia kwa sababu hatuwezi kuamua tu kukata fedha za watu bila ridhaa yao. Kwa hiyo, kwa sasa hivi Kamati ya Uongozi kwa Kikao cha dharura wanashughulikia hilo hilo na watamshauri Spika.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2006, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi nilikuwa napenda kusema tu sasa hivi orodha yangu inawachangiaji 53 na nadhani bado kuna nafasi na imeongezeka na wachangiaji sasa ni 68 imebakia watano tu kufikia ile orodha ile ya mwaka jana 1973. Kwa hiyo, nadhani wale ambao bado wanafikiria kuchangia ni vizuri kutoa taarifa kwenye meza ili tuweze kuwapanga.

La pili, mtaona katika orodha hii mara nyingine nitakuwa naruka majina na kuwahisha mengine hili si suala la upendeleo. Kwa mfano leo hii Mheshimiwa George Simbachawene amepata habari za kusikitisha kwamba kijana wake ambaye alikuwa anasimamia ujenzi wa nyumba kule Kibakwe amejinyonga jana usiku. Sasa ni dhahiri kwa sababu anataka kuchangia inabidi nimpe kipaumbele. Kwa hiyo, mtakapoona msidhani napendelea. Mheshimiwa Ahmed Shabiby Mama yake Mzazi hivi sasa hali yake ni mbaya mbaya sana alikuwa anaomba kuchangia na kwa sababu yeye ni *transpoter* anataka kusema halafu aende mchana huu au kesho asubuhi aweze kwenda nyumbani kumshukuru na kumpeleka Nairobi ambapo ndipo kunafanyika matibabu.

Nimetoa maelezo haya kwa sababu isionekane kwamba orodha tunayo halafu Spika anaruka huyu ama yule. Tatizo lolote ambalo sisi ni binadamu likitokea nipeni taarifa nitaeleza na utaratibu utaendelea. Kwa sasa ninamwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya fedha na Uchumi Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda.

Maelezo ya ziada ni kwamba kama mnavyofahamu Wizara zilikuwa mbili, kulikuwa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, Mwenyekiti huyu amepewa nusu saa mbili. Kwa hiyo, ana uhuru wa kuongea kwa saa moja, ikiwa hotuba ni fupi tutashukuru.

Baada ya hapo Kambi ya Upinzani wanawasemaji wawili. Msemaji wa Uchumi na Msemaji wa Fedha nao wanakipindi kisichozidi saa moja. Watapeana wenyewe utaratibu yupi atachukua dakika ngapi lakini lisizidi lisaa moja. Kwa hao wote wawili.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 43(5)(b) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2006 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niwapongeze Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, kwa hotuba zao nzuri walizowasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mipango na Bajeti ya Mwaka 2007/2008 iliyowasilishwa ni ya Pili ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka jana bado naendelea kuipongeza Serikali kwa msimamo wake wa kuhakikisha kuwa misingi ya kiuchumi iliyokwisha wekwa haikufumuliwa. Kwa maana hiyo Mipango na Bajeti iliyowasilishwa ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Kamati yangu ilishauri kuanzishwa kwa utaratibu wa kuhusisha mapema Kamati za Kudumu za Bunge katika mchakato mzima wa kuandaa Mipango na Bajeti ya Serikali ili kujenga dhana ya mashauriano na kukosoana kwa kujenga *(Constructive Criticism)*, baina ya Serikali na Bunge.

Napenda kuipongeza Serikali kwa kukubali ushauri tulioutoa uliojidhihirisha wazi baada ya kuwa na majadiliano ya kina mwezi Aprili 2007 juu ya Mwongozo wa Serikali wa Bajeti na Mipango uliofanyika kati ya Bunge na Serikali. Hii ni hatua nzuri ya mwanzo kwani utaratibu huu utaondoa dhana ya kazi za Kamati za Bunge kuonekana kama ni kupitia tu shughuli za Serikali *(routine work)* bila ya kupendekeza mabadiliko yeyote.

Aidha, utaratibu huu utatoa fursa na muda wa kutosha wa kujadili Mipango na Bajeti ya Serikali katika hatua za awali na hivyo kujumuisha hoja na michango ya Wabunge kwa ukamilifu. Faida ya utaratibu huu ni kuifanya Serikali kuwaeleza Wabunge ni jinsi gani itakavyotekeleza Mipango na Bajeti ya Serikali kama ilivyoagizwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, katika kipindi kijacho, badala ya kulifanya Bunge la Bajeti kuwa jukwaa la kulalamikia na kunyang'anyana raslimali ya nchi baina ya Sekta na maeneo.

Aidha utaratibu huu unafuatwa na Mabunge mengi Duniani na unachukuliwa kama hatua ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya pamoja baina ya mihimili ya Dola na Bunge. Kwa hiyo, Kamati yangu inaendelea kushauri ili utaratibu huu upate ufanisi unaotegemewa ni vyema utengewe muda muafaka wa kutosha, ili Wabunge wapate kuchangia na kushauri Serikali kuhusu mwelekeo unaotarajiwa na ushauri huo upate muda wa kutathminiwa na kufanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua kuwa Mipango na Bajeti ya Mwaka 2007/2008 imezingatia azma ya Serikali ya kuendeleza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2005, mikakati mbalimbali ya Kitaifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, Malengo ya Milenia, Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Madeni, Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania n.k. Mipango yote hii ni endelevu na utekelezaji wake unaendelea vizuri. Hata hivyo, Kamati yangu ilitoa ushauri wa msingi kwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji wa kuzingatia kupanga mipango yetu na kugawa raslimali chache tulizonazo kwa vipaumbele *(priorities)* kwenye maeneo muhimu ambayo yatachochea kwa haraka kukua kwa uchumi wetu *(quick wins)*. Maeneo haya ni uwekezaji katika barabara, usafiri wa majini, reli na usafiri wa anga, kilimo, nishati pamoja na elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2007/2008, Serikali imepanga vipaumbele vyake kama ifuatavyo:- Elimu 18%, Barabara 12.8%, Afya 10%, Kilimo 6.2%, Maji 5.1%.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuorodhesha changamoto nyingi kila tunapofikia vipindi kama hivi tunapopanga na kuamua tutekeleze nini. Kinachojidhihirisha ni kuwa tatizo kubwa tulilonalo ni la uhaba wa rasilimali fedha. Hata kama tunazo raslimali nyingi bado hatujazibadilisha kwa kiwango kikubwa ili tuweze kuzitumia kama mtaji wa kuleta maendeleo yetu. Hivyo, inaweza ikatokea dhana tu ya kuonyesha kuwa Serikali ingeweza kuamsha mapato mengi tu bila hata kujua na kutathmini miundombinu ya kitaasisi iliyopo na uwezo wa kuandaa kuamsha mapato hayo. Huu ndio ukweli wa hali halisi ya uchumi wetu na mazingira ambayo Serikali inafanyia kazi Sera za Maendeleo ya kiuchumi. Ni suala moja kufanya maamuzi ya ndoto na upande mwingine kufanya maamuzi kuzingatia hali halisi. Kwa changamoto zilizopo tusiingie katika ule mkumbo wa methali ya Kiingereza isemayo *"If wishes were Horses, the Poor would ride them"*, maana tutakuwa tunaingia kwenye *wishful thinking*.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imefahamishwa kwamba maombi yote kama yangechukuliwa, Serikali kutokana na mapato yake ingebidi Serikali itafute shilingi trilioni 12. Zilizopatikana kwa uwezo tulionao kutoka vyanzo vya ndani ni trilioni 3.5 na vyanzo vya nje trilioni 2.5, hivyo kuwa na pengo la trilioni 8.5 ikilinganishwa na mapato yetu ya ndani na trilioni 6 kwa mapato ya jumla. Kamati imeishauri Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuongeza uwezo wa Serikali wa kugharamia mahitaji yake yenyewe kwa kuongeza mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani. Kwa maana hii tutaendelea kupunguza utegemezi wa vyanzo vya nje katika matumizi muhimu ya kitaifa, kwa mfano: Kilimo, Afya, Elimu na Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, miaka michache iliyopita utegemezi wetu ulikuwa karibu asilimia 50. Kwa sasa hivi, utegemezi wetu umefikia asilimia 39. Kwa hali hii ya sasa Serikali itabidi ifanye yafuatayo:-

(i) Kupanga maeneo ya kupewa kipaumbele ili yapatiwe fedha.

(ii) Kutafuta maeneo ambayo yatasaidia kuchangia mapato ya Serikali – yaani *(Tax Revenue Measures)*, kupitia, ada, kodi na tozo; pamoja na mikakati ya kuongeza mapato ya fedha za kigeni ili kupunguza pengo kati ya mauzo yetu nje na yale tunayoagiza.

(iii) Kujenga uwezo wa kuibua mapato kutoka vyanzo vingine ambavyo vina uwezo *(potential)* wa kutoa mapato hayo lakini kwa njia moja au nyingine bado havijajulikana au havijaguswa au havijafanyiwa kazi; na

(iv) kuelekeza fedha chache zilizopo katika maeneo ambayo yatazalisha zaidi na kuwa vyanzo vya kutegemewa vya kutoa mapato na hivyo kusaidia kukuza uchumi. Hatua ya msingi hapa ni udhibiti wa matumizi ya fedha zinazopatikana kuhakikisha kuwa Uchumi unapata thamani ya fedha zilizotumika. Hili litawezekana ikiwa Serikali, kwa makusudi, itazingatia sharti la matumizi bora, yasiyogusa matumizi yasiyo ya lazima, pamoja na uadilifu. Yote haya ni matokeo ya utawala bora *(Good Governance)*. Vipengele vyote hivi vinahitaji mihadi *(Commitment)* si ya Serikali tu, bali ya Watanzania wote kwa ujumla wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaamini kuwa *revenue measures* zilizochukuliwa na Serikali ni muhimu. Hata hivyo changamoto iliyo mbele ya Serikali ni kuhakikisha kuwa yale maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi kama vyanzo vya mapato, ujengwe uwezo na ufuatiliaji wa haraka wa kuyaibua maeneo hayo. Mkakati huu utasaidia sana Serikali na Uchumi wetu kutumia fursa zilizopo kwa mantiki ya kujiendeleza na hatimaye kupunguza utegemezi wetu kwa Wahisani na hatimaye kufuta mzigo wa deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Hali ya Uchumi: Kamati yangu inatambua kasi ya mabadiliko ya Uchumi inavyoendelea duniani, na hivyo Serikali kwa makusudi, ikubali kubadilisha mtazamo wake katika kuendesha Uchumi wa Taifa letu.

Kwa mfano, tunaelewa kuwa ili kujiletea maendeleo tunahitaji Watu, Ardhi, Siasa safi na Uongozi bora.

Kauli mbiu hii tumeifanyia kazi kwa kiwango cha kutosha, lakini uzoefu unatuonyesha kuwa hivi sasa nchi nyingi duniani zimebaini ili kuleta maendeleo sasa tunahitaji yafuatayo:-

(i) Raslimali MAJI kwa maendeleo yetu na maisha yetu.

(ii) Mawasiliano bora ya barabara, reli, usafiri wa anga, usafiri wa majini pamoja na Teknohama *(Information Technology)*.

(iii) Uendelezaji wa Madini ya Chuma na Chuma cha Pua *(Iron and Steel)* ili kuanzisha viwanda vinavyojitegemea.

(iv) Elimu yenye kupendelea Sayansi na Teknolojia ambayo inazingatia ugunduzi na ubunifu katika Sekta zote pamoja na ile ya Ulinzi na Usalama.

(v) Athari za kutokutunza mazingira kwa uchumi na jamii.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yanapopewa kipaumbele katika Mipango na Bajeti yamethibitisha kuleta maendeleo ya haraka *(quick wins)*. Kwa hiyo basi maeneo haya kwa viwango vyake vya utekelezaji vinabakia kuwa ni changamoto kwa Serikali na Wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kama walivyowasilisha taarifa zao Mawaziri wa Mipango na Fedha katika mwaka 2006/2007, Taifa letu lilikumbwa na ukame uliosababisha upungufu wa chakula na umeme pamoja na kuathiri ukuaji wa pato letu la Taifa. Takwimu za Uchumi zinaonyesha kuwa Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.2 mwaka 2006 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/07 Serikali ililenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi trilioni 2.460 na hadi Machi 2007 mapato hayo yalifikia shilingi trilioni 2.0 au asilimia 81.4 ya bajeti ya mwaka. Kwa upande wa matumizi, hadi kufikia Machi 2007 matumizi yalifikia shilingi trilioni 3.41 sawa na asilimia 93.8 ya bajeti ya mwaka mzima wa 2006/07. Mwenendo huu bado unaashiria changamoto kwa Serikali ya mahitaji ya matumizi makubwa zaidi ya mapato. Kimsingi mapato yetu tunayokusanya ni asilimia 15 wakati kiwango cha wastani tunachotakiwa tufike ni asimilia 18 ya Pato letu la Taifa. Kenya wamefikia asilimia 20, wakati Afrika Kusini imefikia asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei ulifikia asilimia 7.3 mwaka 2006 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2005. Hata hivyo, kufikia Aprili 2007 kiwango

kilipungua kufikia asilimia 6.1. Kushuka huku kumetokana na hali nzuri ya upatikanaji wa chakula baada ya mvua kunyesha.

Hata hivyo, bado mfumko wa bei usiohusiana na chakula ulifikia asilimia 8.2 wakati ule unaohusiana na chakula ulifikia asilimia 4.8. Elimu na usafirishaji na mafuta vilipanda kwa asilimia 11, 9.7 na 8.5 kwa kufuatana.

Mheshimiwa Spika, viashiria hivi vya uchumi mkuu, vinatuhimiza kuongeza uzalishaji wetu wa ndani na wa nje. Kamati yangu inaishauri Serikali kutumia mikakati endelevu ya kudhibiti mfumko wa bei ili kupunguza makali ya maisha kwa wananchi hususan wenye vipato vya chini. Kimsingi, mfumko wa bei ndio kigezo cha kupima utulivu wa bei *(price stability)* hasa za mahitaji muhimu ya wananchi na utulivu wa uchumi mkuu *(macro economic stability)*.

Misingi ya kiuchumi inaonyesha kuwa mfumko mkubwa wa bei unaathiri wananchi wenye kipato cha chini ambao ndio walio wengi na kuwapa nafuu wale wenye kipato cha kati na juu. Sababu kubwa ni kuwa wale wenye kipato cha chini inawachukua muda mrefu kurekebisha mfumo wa matumizi yao ya mahitaji muhimu ya kila siku panapokuwa na mabadiliko makubwa ya bei za bidhaa za msingi ikilinganishwa na wale wenye kipato cha kati na juu.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mapato yetu ya ndani upo umuhimu mkubwa wa kuimarisha mkakati wa kukuza mauzo ya bidhaa zetu nje *(Export led strategy).*

Thamani ya mauzo ya bidhaa nje ilifikia dola za Marekani 1,473.1 milioni mwaka 2005 wakati thamani ya bidhaa tulizoagiza kutoka nje ilifikia dola za Marekani 2,661.8 milioni mwaka 2005. Takwimu zinaonyesha kuwa dhahabu na samaki vimechangia takriban asilimia 55.8 ya mauzo ya bidhaa tulizouza nje.

Hali hii inasisitiza umuhimu wa kupanua uwekezaji katika maeneo mengine hususan yale ya sekta za huduma ili tupate mapato zaidi. Sekta ya utalii na *transit trade* vinaweza kuiingizia nchi fedha nyingi za kigeni. Aidha, mikakati ya kuendeleza gesi, mkaa wa mawe na chuma vitasaidia sana kuongeza pato la Taifa. Bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 78.8 ya mauzo yote nje wakati bidhaa asilia zilichangia asilimia 21.2 tu. Kwa wastani mauzo ya nje yalikuwa kwa asilimia 0.6 ukilinganisha na asilimia 30 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Spika, taswira iliyopo sasa katika Sekta ya mauzo nje inaonyesha kupungua kwa uzalishaji katika sekta za bidhaa asilia *(goods sector)* ikilinganishwa na sekta ya huduma *(services Sector)*. Kwa maana hii Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha kuendeleza usafirishaji, utalii, uvunaji wa maliasili kama vile bidhaa za misitu pamoja na uvuvi wa baharini na katika maziwa yetu.

Hatua hizi zitatunisha mapato ya Taifa kwa kiwango kikubwa. Takwimu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii zinaonyesha kuwa mapato yaliyokusanywa kutokana na

mazao ya misitu ni asilimia 4 tu. Changamoto sasa ni kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato katika maeneo yote husika.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya *quick wins* ni haya yafuatayo:-

(i) Eneo la uvuvi wa bahari. Eneo letu la *Exclusive Economic Zone* katika pwani ya Bahari ya Hindi bado hatujalitumia kikamilifu na kwa tija. Takwimu zinaonyesha kuwa tunakosa mapato makubwa kutoka bidhaa za samaki katika eneo hili. Badala yake kwa kushindwa pia kulidhibiti eneo hili, wanaofaidika ni wavuvi kutoka nje na hivyo kulikosesha Taifa letu mapato makubwa.

(ii) Serikali ipanue matumizi ya mfuko wa *Export Guarantee Scheme* ili ujumuishe bidhaa nyingi zinazozalishwa nje pamoja na kutumia kikamilifu fursa za mipango kama vile ya *AGOA* na *EBA*.

(iii) Eneo la *transit trade* litupiwe macho na Serikali. Takwimu zinaonyesha kuwa tutakapoboresha reli na barabara zetu na kuunganishwa kibiashara na nchi jirani za Rwanda, Burundi, *DRC*, Uganda na hata Zambia. Eneo la usafirishaji pekee linaweza kutuingizia dola za Marekani bilioni 2 kila mwaka. Hili litahitaji pia tuboreshe bandari ya Kigoma na Dar-es-Salaam.

(iv) Serikali iweke misingi imara ya kujenga uwezo wa kutumia misaada tunayopata kuwekeza kwenye maeneo ambayo yatazalisha na yatakayoongeza uwezo endelevu wa kujitegemea baadae. Fedha za Wahisani tutakuwa tunazitumia vibaya ikiwa zitatumika kugharamia kwa kiwango kikubwa matumizi ya kawaida *(Recurrent Expenditure or Other Charges)*.

(v) Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inafanya kazi nzuri ya kusimamia na kukusanya mapato. Hivi sasa *TRA* wanaweza kukusanya Shilingi bilioni 260 kwa mwezi. Haya ni mafanikio makubwa lakini bado changamoto kubwa kwa *TRA* kuongeza juhudi za kukusanya mapato zaidi. Mapato ya Serikali bado hayawiani na matumizi, hali inayosababisha kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ili kuziba pengo la bajeti.

Uwiano wa mapato yetu na Pato la Taifa *(GDP)* bado uko chini na kazi zaidi inatakiwa kufanyika. Bajeti yetu hadi sasa ni tegemezi kwa asilimia 39. Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze juhudi za kukusanya mapato yetu ya ndani. Kamati yangu inaamini kabisa *TRA* inaweza kukusanya mapato zaidi ikiwa itagusa yale maeneo yaliyoachwa au yanayojulikana kuwa ni sehemu ya mianya ya kupoteza mapato.

(vi) Kamati yangu imebaini kuwa eneo la uwekezaji wa mitaji ya nje ni muhimu sana *(Foreign direct investment)*. Mwaka 2005 tuliweza kuvutia mitaji ya thamani ya dola za Marekani 473.4 milioni ambayo ilikuwa ni ongezeko la asilimia 0.72 ukilinganisha na mwaka 2004.

Ni muhimu Serikali ikaendelea na mikakati yake ya kupunguza gharama za kufanya biashara/uwekezaji nchini *(cost of doing business)*.

Maeneo yanayohitaji kurekebishwa ni pamoja na urasimu na utoaji maamuzi, kupunguza gharama za nishati ya umeme pamoja na kuboresha miundombinu ya usafiri. Uwekezaji wa Mitaji ya nje ni moja ya eneo la *quick win*.

Mikakati hii inayohamasisha uwekezaji nchini *(investment drive)* itasaidia kupunguza utegemezi katika bajeti yetu ambayo kwa kipindi cha miaka

mitatu mfululizo umeendelea kuwa asilimia 39. Utegemezi wa bajeti ya Serikali kwa Wahisani kunaweza kuyumbisha uchumi wetu mara hisani hizo zisipotekelezwa.

(vii) Eneo la uwezeshaji wa Wananchi ni muhimu katika kutoa matunda ya haraka. Kamati imeishauri Serikali kukamilisha marekebisho ya utendaji kazi na kisheria wa Sekta ya Fedha ili kuiwezesha mchango zaidi kwa uchumi wa nchi yetu. Wananchi wengi wapate mikopo ya uzalishaji na biashara, mikopo ya nyumba, mikopo ya mali za kukodi; kama Serikali ilivyoahidi; eneo la riba lihuishwe ili kuruhusu *SACCOS* zilizoanzishwa zisaidie wananchi wenye vipato vya chini; na Benki Kuu itumie madaraka iliyopewa kisheria kuhakikisha kuwa mifuko ya dhamana ya mikopoinatumiwa na wananchi walio wengi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina lazimika kukatiza taarifa ya Mwenyekiti kwa sababu wale Mabalozi tuliowaona hapo ni Wageni wetu na kwa bahati mbaya inabidi waondoke. Wamekuja kwa mazungumzo ambayo yana maslahi makubwa sana kwa Bunge letu. Itakuwa na athari kama nisipowasikiliza. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aje ashike kwa muda wakati mimi naongea hapo *Speaker's Lounge* na Waheshimiwa Mabalaozi. Shughuli zingine ziendelee.

*(Hapa Naibu Spika Alikalia Kiti)*

*TIB* kama Benki ya Maendeleo iimarishwe mara moja. Eneo la Uwezeshaji halitasaidia tu katika kuongeza mapato bali pia litazalisha ajira kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inatambua ili maendeleo yapatikane katika uchumi wa nchi yoyote, huduma za taasisi za vyombo vya fedha ni muhimu. Wananchi wengi wanazo nyenzo za uzalishaji kwa maana ya ardhi na nguvu kazi. Tatizo kubwa ni mtaji pamoja na ujuzi, utaalam na ujasiriamali. Bado kwa Watanzania wengi suala la mkopo ni tatizo. Karibu asilimia 45 ya wale waishio mijini hawajanufaika na huduma za kifedha kupitia mikopo, Vijijini ni asilimia 57. Kuhusu vyanzo vya mapato tafiti zinaonyesha kuwa ni asilimia 36 na 35 ya watu kwa kufuatana, wanategemea uuzaji wa bidhaa za shambani na bidhaa ndogo ndogo. Ukichukua Tanzania Bara na Zanzibar karibu asilimia 86 ya wananchi hawana akaunti benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchunguzi unaonyesha kuwa matumizi ya mikopo yanaonyesha kuwa ni asilimia 4 tu ya Wananchi vijijini ambao wamekopa kutoka mabenki wakati karibu asilimia 38 wanakopa kutoka kwa marafiki au familia. Takwimu hizi zinaonyesha mfumo uliodumaa wa vyombo vya fedha vinavyohudumia wale wenye vipato duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa jitihada zake za dhati za kuondoa picha hii kwa kuanza na utaratibu wa shilingi bilioni moja kwa kila mkoa, pamoja na jitihada zake za hivi karibuni za

kumkaribisha Dkt. Yunus wa *Grameen Bank* kuja Tanzania kubadilishana mawazo ya jinsi ya kutoa mikopo kwa wananchi maskini. Benki ya *Grameen* hadi sasa ina wateja milioni 7 wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaelewa kuwa hata kwa Watanzania wa vipato vya kati na juu walio wengi pia wana matatizo ya kupata mikopo ya kati na ya muda mrefu. Ipo haja ya kutatua tatizo hili pamoja na kuboresha riba za amana na kupunguza riba za mikopo ili kuweka mazingira bora ya upatikanaji wa Mikopo ya Nyumba *(Mortgage Finance)* na Mikopo ya ukodishaji *(Lease Finance).* Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mikakati ya kurasimisha Wajasiriamali wadogo wadogo ili kuwatoa kwenye sekta isiyo rasmi, hatua ambayo itaiongezea Serikali mapato kwa kupanua wigo wa kodi (MKURABITA).

Mheshimiwa Naiabu Spika, wananchi wengi vijijini hawajajua utaratibu wa kuzitumia Benki hizi, hivyo wanaonufaika ni wachache. Kamati inapendekeza elimu huko vijijini iendelezwe ili kusaidia wananchi kufaidika na huduma hizi muhimu. La sivyo, jitihada za kuwawezesha wananchi hususan walio na kipato cha chini kupata mitaji haitazaa matunda yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa kila mkoa ili kuwezesha wananchi kupata mikopo ya masharti nafuu kupitia Benki za *CRDB* na *NMB* kwa kudhaminiwa na Serikali. Mtazamo wa Kamati ni kwamba fedha hizo zilitolewa bila maandalizi. Kamati inashauri kuwa wananchi wapatiwe elimu ya ujasiriamali, kanuni na taratibu za kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzalishaji wa moja kwa moja katika uchumi hautaendelea bila ya mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa masharti nafuu. Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuendelea na azma yake ya kuiwezesha *Tanzania Investiment Bank (TIB)* kutoa mikopo ya maendeleo.

Nchi nyingi zinazoendelea zimetumia mfuko huu kwa tija. Ni vigumu kwa Sekta za Kilimo na Viwanda kuendelea bila ya mikopo ya muda wa kati na muda mrefu. Aidha, Kamati imebaini kuwa Benki ya Posta ina mtandao mkubwa kuliko Benki nyingine nchini. Katika mchakato unaoendelea wa marekebisho ya sekta ya fedha Serikali iangalie uwezekano wa kuimarisha Benki hiyo na kupewa uwezo ili ihudumie vyema wananchi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *Second Generation of Financial Reforms* ukamilishwe ili miongoni mwa masuala husika mengine kupunguza ukubwa wa riba za mikopo ili kusaidia vyombo vinavyosaidia mikopo ya wananchi wenye vipato vya chini hususani vijijini; kwa mfano *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Sekta mbalimbali: Sekta ya Kilimo: Kamati yangu imejenga hoja kuishauri Serikali kujihami na utegemezi mkubwa wa mvua kwa sekta hii muhimu hasa ikizingatiwa kuwa ukame unachangia kushuka kwa ukuaji wa sekta hii mwaka hadi mwaka. Mpango kamambe wa kilimo cha umwagiliaji

uliokwishaanzishwa utekelezwe kwa nguvu zote, sambamba na upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani *(extension services)* na kuimarisha mikakati ya kuvutia wawekezaji wakubwa binafsi katika sekta ya kilimo.

Kamati inaona kuwa Sekta ya kilimo ni eneo mojawapo la kutoa matunda ya haraka *(quick win)*. Hatua zifuatazo inashauriwa zitekelezwe haraka na Serikali:-

(i) Mkakati wa kuongeza maafisa ugani ni muhimu ingawaje katika nchi zilizoendelea maafisa ugani hawahitajiki kwa kuhofia kuduma za ushindani baina ya wazalishaji mashambani.

(ii) Upo umuhimu wa uratibu wa tija wa usambazaji wa pembejeo za kilimo zinazopatikana ili wakulima wafaidike na ruzuku ya pembejeo inayopatikana. Eneo hili bado ni kero hivyo kuifanya ruzuku hiyo isiwe na athari katika mazao yanayolimwa hasa korosho, pamba, n.k.

(iii) Uzalishaji wetu wa kilimo haulingani na uwezo wa raslimali watu na raslimali za asili *(natural resources)*. Ni muhimu uwekezaji kwenye kilimo wa sekta binafsi na sekta ya umma kwa kushirikisha sekta ya fedha, uwe na malengo kwa kuongeza uzalishaji hasa wa bidhaa asilia.

(iv) Umefika wakati sasa kwa Serikali, kwa makusudi kabisa, kubuni na kuanzisha vivutio *(incentives)* vitakavyovutia wawekezaji wakubwa na wadogo katika sekta ya Kilimo.

Maeneo ya sheria, kodi na tozo zinazotozwa katika sekta ya kilimo yaangaliwe na kuhuishwa. Kodi na tozo zipunguzwe na zile ambazo si za lazima zifutwe. Kwa mfano, urasimu wa kutoa hati miliki za ardhi pamoja na tozo la Sh.200 kwa ekari, vitaendelea kukwaza maendeleo ya sekta hii muhimu.

(v) Kamati ina wasiwasi na kiwango chetu cha juu cha kuwa na tani 150,000 cha hifadhi ya chakula na cha tani 120,000 kilichopo sasa. Kiwango hiki ni kidogo kwa hifadhi ya Watanzania takriban milioni 37. Kiwango hiki kiongezwe, kiwe endelevu na kituvushe wakati wa uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda: Katika mwaka 2006, Sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2005. Mchango wake katika Pato la Taifa uliongezeka hadi asilimia 9.2 ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2005. Kamati imebaini kuwa kupungua kwa uzalishaji na ukuaji wa sekta ya Viwanda kulitokana na kupanda kwa gharama za umeme, mafuta ya kuendeshea mitambo na usafirishaji.

Vyote hivi vilichangia kuongeza gharama za uzalishaji katika Sekta ya viwanda kutoka shilingi trilioni 1.957 mwaka 2005 mpaka Shilingi trilioni 2.177 mwaka 2006. Kuharibika kwa reli na barabara kumeendelea kuchangia kupanda kwa gharama za

uzalishaji viwandani. Aidha, msukumo mdogo wa kuanzisha viwanda vinavyosindika mazao yetu, hasa ya kilimo unatupunguzia mapato kutoka sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado gharama za umeme unaozalishwa na *TANESCO* zimeendelea kupanda siku hadi siku. Kamati inashauri na kusisitiza programu za kuendeleza mradi wa Makaa ya mawe ya Mchuchuma „ mradi ule wa Chuma wa Liganga pamoja na mradi wa gesi Mtwara na Mkuranga na mradi wa *nickel* wa Kabanga ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha *Export Processing Zones (EPZs)* na *Special Economic Zones (SEZs)*. Ili kuwavutia wawekezaji katika programu hizi, tatizo la umeme wa uhakika na wa bei nafuu lazima lipatiwe ufumbuzi haraka iwezekanavyo ili vyombo hivi vichangie katika kukuza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini: Kamati imefahamishwa kuwa katika mwaka 2006 takribani asilimia 46 ya mauzo ya nje yametokana na mauzo ya dhahabu. Serikali inashauriwa kuharakisha mkakati wa *diversification* katika madini ili aina nyingine za madini kama chuma, *nickel*, ambazo hivi sasa zina bei kubwa duniani ziendelezwe kupitia wawekezaji wa nje na wa ndani. Wawekezaji watakaojitokeza kuendeleza maeneo haya, wahamasishwe na wajengewe mazingira mazuri. Mkakati wa sasa wa Serikali wa kuanzisha Wakala wa Kuendeleza viwanda vidogovidogo na biashara ndogondogo kupitia *SIDO* uandamane na uanzishaji wa Wakala wa kuendeleza Wachimbaji Wadogo wa madini kupitia *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Miundombinu: Kamati inaipongeza Serikali kwa kupata mafanikio katika Sekta mawasiliano ya simu. Hii imechangiwa zaidi na ushirikishwaji wa Sekta binafsi. Ukosefu wa miundombinu yenye uhakika na ubora wa Kimataifa ni gharama kubwa ya uwekezaji nchini.

Miundombinu ya kiuchumi kama vile Reli, Barabara, Bandari, Umeme, Maji, Teknolojia ya Habari, Mawasiliano *(ICT)*, vikiendelezwa itatoa chachu ya kuongeza uzalishaji katika sekta zote nchini; itaongeza ushindani katika mauzo ya nje na pia itawezesha Tanzania kufaidika na soko la nchi jirani kupitia matumizi ya huduma za Bandari na Reli (Uchumi wa Kijiografia).

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua zilizonyesha zimeathiri barabara nyingi nchini. Kamati yangu ilipokuwa inapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha ilibaini fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ni chache. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubaliana na pendekezo la Kamati la kufidia bajeti ya matumizi ya kawaida kutoka kila Wizara ili kufidia gharama za ukarabati wa barabara hadi kupatikana Shilingi bilioni 777.2 ambazo ni sawa na asilimia 12.8 ya bajeti. Barabara hizi zikikarabatiwa malengo ya kitaifa ya kukua kwa uchumi yatafikiwa. Hili ni eneo lingine la *quick win* ambalo matunda yake yataonekana mara tu baada ya kuanza ukarabati husika. Kamati inaishauri Wizara husika kujiandaa vyema na kuimarisha uwezo wake ili zoezi zima lifikie matarajio ya wananchi ya kupunguza kero ya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Mapato: Bajeti ya mwaka 2007/2008 itagharimu Shilingi trilioni 6.1 kutoka vyanzo vya ndani, misaada, misamaha ya ndani ya madeni na vyanzo vingine. Mapato ya ndani yanategemewa kuongezeka kutoka Shilingi trilioni 2.5 hadi Shilingi trilioni 3.0. Hii ni asilimia 60 ya mapato ya Serikali ikilinganishwa na asilimia 51 Mwaka 2006/2007. Kamati yangu imebaini kuwa shilingi trilioni 6.1 ambazo Serikali imepanga kuzitumia kwa mwaka 2007/2008, nyingi ya fedha hizo zitaelekezwa kwenye Halmashauri. Baadhi ya majukumu na rasilimali kutoka Wizara tano za Serikali Kuu zitakwenda kwenye Halmashauri. Wizara zitakazohusika ni Afya na Ustawi wa Jamii, Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Kilimo, Chakula na Ushirika, Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

. Mheshimiwa Naibu Spika, kupeleka madaraka kwa wananchi *(D by D)*: Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza kasi ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa *(Decentralization by Develution - D by D).*

Kamati ilifahamishwa kwamba uchambuzi uliofanyika umebainisha kuwa baadhi ya kazi zinazofanywa na Serikali Kuu zinaweza kutekelezwa kwa ufanisi na uwajibikaji zaidi kama zitahamishiwa katika Halmashauri. Mpango huu ni mzuri kwa sababu utahusisha wawakilishi (Wabunge na Madiwani) moja kwa moja katika kufuatilia maendeleo katika maeneo yetu.

Tukifuatilia vyema itapunguza maswali mengi yanayoelekezwa kwa Serikali Kuu. Fedha zikibaki Serikali Kuu, ufuatiliaji wa ngazi za chini unaathirika. Utaratibu huu utaimarisha uwajibikaji na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati yangu ina wasiwasi juu ya uwezo wa usimamizi wa fedha hizo. Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kumudu kusimamia fedha hizo. Uwezo wa kiutawala na kihasibu bado ni mdogo. Kamati yangu kupitia Wizara ya Fedha imebaini kuwa katika jumla ya mapato ya shilingi trilioni 6, Halmashauri za Wilaya zimetengewa Shilingi milioni 810. Lakini hata hivyo takribani asilimia 70 ya fedha za bajeti zitakwenda kwenye Halmashauri za Wilaya kupitia miradi mbalimbali kwa njia ya MES, *TASAF* n.k. Hapa ndipo tatizo linapojitokeza kuhusu usimamizi na matumizi ya fedha zote hizo huko Wilayani. Pamoja na nia njema ya Serikali ni vyema ijiulize uwezo wa Halmashauri hizi katika kutumia fedha hizo ukoje. Fedha hizi zikitumika vizuri zitasaidia Serikali kufikia malengo yake muhimu iliyojiwekea katika mpango wa MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa Serikali kufuatilia kwa ukaribu matokeo (*impact*) ya fedha katika Halmashauri zinavyotumika katika maeneo yaliyopangiwa kuwafikia walengwa. Serikali ipime thamani ya fedha zinazotolewa *(value for money).* Zoezi hili lisiangalie jinsi fedha zilivyotumika bali pia litathimini rasilimali zilizopatikana kutokana na matumizi hayo. Kamati inashauri Serikali ifanye maandalizi ya kutosha ya kujenga uwezo *(capacity building)* kupitia uboreshaji wa viwango vya Watumishi, vitendea kazi na elimu ya mipango ya nchi na kuimarisha usimamizi wa ufuatiliaji katika Halimashauri. Wizara ya Fedha tunaishauri kwa

makusudi iimarishe vitengo vya *Expenditure Tracking Unit, Internal Audit, Technical Audit* na *Cash Management Unit.*

Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete kwa hatua aliyochukua tarehe 15 Aprili, 2007 alipoitisha Kikao cha kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kukemea kwa nguvu upungufu uliojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubinafsihaji wa Mashirika ya Umma, Kamati yangu inatahadharisha kuwa ubinafsishaji wa Mashirika yaliyosalia ya Reli, *TANESCO* na *NIC* ufanywe kwa uangalifu mkubwa. Mashirika haya yanagusa maisha ya watu na uhai wa uchumi wa Taifa letu. Mathalani katika hatua za awali zilizofanywa na *PSRC* katika kubinafsisha Shirika la Bima la Taifa, (*NIC*) tathimini ya thamani ya majengo ilikuwa bilioni Tsh.23,655,000,000 lakini baada ya Kamati kuagiza tathimini ifanyike upya, thamani imeongezeka na kufikia bilioni Tsh.35,155,000,000. Hii inaimanisha kuwa *PSRC* hawakuwa makini katika kutekeleza wajibu wao kulingana na muda wa maamuzi. Muda wa *PSRC* unaisha Desemba 2007, ni vyema sasa Serikali ikajiandaa kutumia wataalamu husika ili kuanzisha kitengo cha ufuatiliaji wa karibu wa mashirika yaliyobinafsishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati: Kamati ilikuwa na maoni na mapendekezo yafuatayo:

Kwanza, Kamati inaishauri Serikali isimamie vizuri MKUKUTA na programu zinazoelekezwa kwenye Halmashauri zetu *(TASAF, PADEP, ADSP)* n.k. Aidha, masuala ya utawala bora yanayoandamana na rasilimali zinazoelekezwa vijijini yazingatiwe. Ni vema Halmashauri zote kupitia maboresho zifanyiwe *serious reform auditing*.

Pili, ni wakati mzuri kwa Serikali kujihami na upatikanaji wa umeme ili kuzuia hasara katika uchumi wetu. Programu za dharura zilizoanzishwa wakati wa uhaba wa umeme ziwe ni (*safety nets)* ni programu za kinga, hasa ikizingatiwa kuwa hadi kufikia mwisho wa Juni 2007 shilingi bilioni 204.5 zitakuwa zimetumika kulipia mitambo ya kununua na ya kukodi ya kuzalisha umeme. Aidha, kwa upande wa madini Kamati inaishauri Serikali kuendelea na hatua za kuhakikisha kwamba Taifa linapata manufaa zaidi kutokana na uwekezaji katika sekta ya madini ili kuongeza mchango wa sekta hii katika pato la Taifa.

Tatu, kwa vile Kilimo ndiyo sekta inayoajiri Watanzania walio wengi na imetengewa fedha nyingi na Serikali, tokea bajeti ya mwaka 2006/2007, matumizi ya fedha hizo yaongeze tija na ufanisi katika sekta hii muhimu. Uboreshaji wa miundombinu ya kitaasisi na ile ya barabara hasa vijijini itasaidia kuongeza uzalishaji katika Kilimo na hivyo kukuza uchumi wetu. Serikali inashauriwa kuwa iendeleze utafiti wa masoko ya mazao ya biashara yanayoweza kuzalishwa kwa wepesi na wakulima wadogo kwa kutumia teknolojia rahisi na endelevu.

Nne, katika eneo la Uwezeshaji wa wananchi wenye vipato vya chini, kupata mitaji kupitia mabenki, *SACCOS* na taratibu nyingine, ni vyema sasa taasisi hizi zipunguze gharama za utawala/uendeshaji, walengwa wazingatie kupunguza uwezekano wa hasara inayotokana na matumizi mabaya ya mikopo na hatimaye kushindwa kuilipa Benki.

Tano, ni muhimu kuzingatia hatua mbali mbali zinazopelekea kupunguza gharama ya fedha ili kupunguza riba inayotozwa. Miongoni mwa hatua hizo ni kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inakuwa chachu ya kuongeza vipato vya wakopaji, ongezeko la shughuli za kiuchumi *(growth impact assessment)*, na hatimaye kuongeza mahitaji ya mikopo zaidi. Riba kubwa inayotozwa na taasisi za fedha inaendana na wasiwasi wa ulipaji wa mikopo kwa upande wa wateja. Elimu iongezwe vijijini kuhamasisha wananchi kuchukua mikopo lakini walipe mikopo hiyo. Nidhamu ya mikopo ikuzwe.

Kamati inaishauri Serikali kuzingatia mfumo wa ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi ya misingi *(Public Participatory Approach)* hasa ikizingatiwa kwa hivi sasa mtazamo ni ule wa kupeleka madaraka kwa wananchi. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba ushirikishwaji katika mipango na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma pamoja na uwajibikaji bado unahitaji kuboreshwa zaidi hasa kuanzia ngazi za Vijiji, Serikali za Mitaa hadi ngazi ya Wilaya.

Uzoefu unaonyesha kuwa mara nyingi maamuzi ya mipango na ya kibajeti yaliyoridhiwa na kupitishwa katika ngazi za vijiji, Serikali za Mitaa na Waheshimiwa Madiwani, hubadilishwa kuwa maagizo ya matumizi *(expenditure instructions)* kutoka kwa wataalamu wa ngazi za juu bila ya kuzingatia maamuzi yaliyopendekezwa ngazi za awali.

Sita, Kamati imefuatilia kwa karibu utaratibu uliowekwa wa matumizi ya shilingi bilioni 1 kila Mkoa kama njia mojawapo ya kuwawezesha wenye vipato vya chini. Hata hivyo, uzoefu wa muda mfupi umeonyesha yafuatayo:-

(i) Masharti ya *NMB* na *CRDB* hayajaeleweka na walengwa wengi wanaolengwa hivyo kuashiria tatizo la upatikanaji usio sawa kwa maeneo nchini.

(ii) Uamuzi wa Serikali ulikuwa na malengo matatu, kwanza, wajibu wa kisiasa, pili, wajibu wa kijamii na tatu wajibu wa kiuchumi. Kwa upande mwingine utoaji wa fedha hizo kupitia mabenki yana wajibu mmoja tu ule wa kufanya kazi kwa faida na hasara ndogo.

Matokeo yake mabenki haya yataendelea kutoa mikopo bila ya kuzingatia uwiano wa ki-Mikoa (maeneo) na walengwa. Hii italeta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kwa Serikali hasa katika ngazi za vijijini.

Kamati ina ushauri ufuatao:-

(a) Kazi ya kuendesha mikopo iachiwe Mabenki yaliyoteuliwa, lakini kwa kuzingatia kuwa kila Mkoa unapata kiwango chake cha bilioni moja.

(b) Uongozi wa Mkoa ufanye utaratibu wa kuyaagiza Mabenki haya kugawa fedha hizo ki-Wilaya kutegemea Benki zilizoko huko. Mtandao wa *NMB* ni mkubwa. Zoezi la kulenga (*target*) Walengwa lifanyike na Serikali ya Wilaya ili kuhakikisha uwakilishi mzuri, hata kama hautagusa walengwa wote. Kwa kufanya hivi dhana ya uwezeshaji itatapakaa nchi nzima kuliko ilivyo hivi sasa.

Aidha, sehemu ya Fedha hizi zingekuwa ni sehemu muhimu ya kuchangia uanzishwaji wa Benki za Jamii *(Community Banks)* ili kutoa hamasa kwa nguvu za wananchi wanaochangia ili kuanzisha Benki hizi pamoja na kuongeza uelewa na ufahamu unaotokana na kujifunza jinsi utaratibu wa kuweka na kukopa unavyofanya kazi. Uanzishwaji wa Benki za Jamii ndio njia ya uhakika na endelevu ya kuwalenga wale wananchi wenye vipato vya chini katika muda ujao.

(c) Kwa vile mpango wa *Grameen Bank* unaoendeshwa na *Dr. Yunus* umeleta mafanikio, ujio wa mtaalamu huyu uzingatiwe na Serikali, ambapo benki ya *Grameen* moja ya dhamana yake ni uaminifu tu kwa huyo maskini anayeomba mkopo huo. *(Makofi)*

Saba, Kamati inaendelea kutoa msisitizo wa kuanzisha mapema utaratibu wa Mortagage *Finance* na *Leasing Finance*. Utaratibu huu utawawezesha wananchi kujenga makazi yao pamoja na kukodisha zana na vifaa mbalimbali katika shughuli zao za kuendeleza Uchumi. Ni maoni ya Kamati yangu kuwa utaratibu huu uanze mapema.

Nane, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizozichukua za kubuni hatua za kukusanya mapato kibajeti kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 *(revenue measures)*. Bajeti ni muhimu izingatie matarajio ya wananchi. Katika kipindi cha 2006/2007 wananchi wengi wamekuwa wakilalamikia makali ya uchumi yaliyotokana na gharama kubwa za mahitaji yao ya msingi ya kila siku *(basic needs)*. Chanzo cha hali hii ni mfumko wa bei ulioongezeka kutokana na bidhaa zinazohusiana na chakula na ule usiohusiana na chakula.

Mfumuko wa bei usiohusiana na chakula *(non-food inflation)* umechangiwa na mafuta. Mafuta yamechangia mfumko wa bei kwa asilimia 9 ukiacha ule wa usafirishaji uliochangia asilimia 7. Tanzania hatuzalishi mafuta na hivyo, tutaendelea kuagiza mafuta hayo ambayo hadi hivi sasa hakuna dalili yoyote ya kuonyesha kwamba bei za mafuta zitapungua. Kwa hiyo, basi mafuta yataendelea kwa hali yoyote kuchangia mfumko wa bei nchini. *(Makofi)*

Changamoto kubwa ni kuwa ughali wa mafuta unagusa maeneo mengi ya kiuchumi. Katika bajeti ya 2007/08 ushuru wa mafuta ya aina zote umepanda pamoja na mafuta ya taa na yale ya viwandani. Matokeo yake ni kuongeza gharama za usafirishaji ambazo zitawagusa wananchi. Lakini pia gharama za ada ya leseni za magari zimeongezeka. Hili ni ongezeko litakalowagusa wananchi moja kwa moja. Aidha,

kupanda kwa ushuru wa mafuta yanayotumika viwandani kutaongeza gharama za uzalishaji viwandani na hivyo kuongeza bei ya bidhaa zitakazozalishwa. Maeneo yote haya yataongeza gharama zinazowagusa wananchi wa kawaida moja kwa moja.

Kwa maana hii basi ni lazima utekelezaji wa Bajeti hii uwe na mwelekeo wa kuchukua hatua zote zile zinazotakiwa ili kupunguza makali yatakayojitokeza kwa mwananchi wa kawaida. Miongoni mwa hatua hizo ni usimamizi imara wa matumizi ya fedha za umma pamoja na kuhakikisha kwamba kanuni na taratibu za manunuzi kama zilivyowekwa kisheria zinazingatiwa katika ngazi zote.

Kama tulivyopendekeza mwanzoni, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwezo na udhibiti wa kukusanya mapato kutoka vyanzo vingine. Kwa mfano, vile vya eneo la uvunaji wa bidhaa za misitu – magogo na asali, eneo la uvuvi hasa ule wa baharini *(deep sea* na *Economic Exclusive Zone)*, eneo la madini, eneo la uwindaji n.k. ambako bado Serikali haijakamata kikamilifu mapato yote na hivyo kufanya yawe maeneo ya kuvujisha viwango vikubwa vya mapato ya Serikali. Kwa kufanya hivi mapato ya ziada yatakayopatikana yafidie baadhi ya ushuru na kodi hasa zinazogusa matumizi ya msingi ya wananchi walio na kipato cha chini hususan mafuta ya taa, vinywaji baridi n.k. na hivyo kupunguza bei ya bidhaa hizi. Hali hii itawapunguzia mzigo wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu Serikali inaweza kuangalia upya uamuzi wake pamoja na kuhuisha baadhi ya kodi na ushuru uliopendekezwa. Changamoto hili linaangukia mikononi mwa *TRA* ambayo Kamati ina imani kuwa inaweza kufikia malengo kutokana na utendaji wake wa tija na ufanisi tuliouzoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ya uhaba wa fedha pamoja na haja ya kubainisha maeneo ya kipaumbele katika uchumi wetu inajitokeza kwa vile Serikali imepiga hatua kubwa katika kupunguza umaskini usio wa kipato kwa wananchi wengi, ila sasa changamoto kuu bado inabakia katika kupunguza umaskini wa kipato. Ushauri huu wa Kamati uwe ni changamoto kwa Serikali ya kuendelea na hatua zake za kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali, narudia, "inaishauri Serikali" pamoja na ongezeko la ushuru katika bidhaa za mafuta, iboreshe mazingira ya kujenga ushindani katika biashara ya mafuta. Hali hii itapunguza uwezekano wa waagizaji na wasambazaji wachache kutumia ukiritimba na hatimae kuwabebesha mzigo watumiaji wa bidhaa za mafuta wakiwemo wananchi wa kawaida *(End Users) (Makofi).*

Kamati inaamini kuwa hili likitekelezwa kwa usahihi tija na ufanisi katika biashara ya mafuta vitafanya bei za bidhaa za mafuta kupungua kutokana na ushindani huo. Bei za mafuta zikipungua hasa ya mafuta ya taa itasaidia kupunguza kwa kiwango kikubwa uharibifu wa mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika utaratibu mzima wa kuwawezesha wajasiriamali kupitia SMEs ili kuongeza viwango vya ajira nchini na kuongeza mapato yao na hatimaye kupanua wigo wa kodi. Hadi mwishoni mwa mwezi Machi, 2007 Mfuko wa Dhamana wa Biashara ndogo ndogo ulitoa udhamini

wa mikopo ya Shilingi bilioni 1.204 tu; ukilinganisha na ule wa Miradi ya Maendeleo uliopata Shilingi bilioni 19.61 na ule wa uuzaji Bidhaa nje uliopata shilingi bilioni 149.17. Kwa picha hii utaratibu huu hautoi fursa ya kusaidia wale wenye vipato vya chini. Serikali ibadilishe utaratibu huu ili kuwasaidia zaidi wajasiriamali wadogo.

Kamati inaelewa umuhimu wa hatua za mapato *(revenue measures)* zilizochukuliwa na Serikali hasa tukizingatia umuhimu mkubwa wa kuboresha barabara zetu katika kipindi hiki. Barabara zetu ni vyema zikakarabatiwa hivi sasa ili kuwezesha shughuli za kiuchumi ziendelee vizuri. Hata hivyo, Kamati yangu inaishauri Serikali kuangalia tena uamuzi wake wa kubadili mfumo wa kutoza ada ya mwaka ya leseni za magari, hasa kwa kuzingatia vigezo vya ujazo wa injini. Kamati inashauri kuwa, kwa sababu wananchi walio wengi wanategemea huduma za usafirishaji na wamejiingiza katika biashara ya usafirishaji; kwa mfano, bajaji, teksi, daladala, *pick up,* n.k. uhuishaji wa viwango vya ada kwa kutumia kigezo cha ujazo wa injini utapunguza athari za kupanda bei kwa watumiaji wengi wa huduma hizi na vilevile utapunguza gharama kubwa za ukusanyaji mapato yenyewe kwa upande wa *TRA*. Kwa hiyo, basi Kamati inashauri kuwa ada ya kiwango cha Sh.80,000/= iangaliwe ili itumike pia kwa magari ya zaidi ya ujazo wa injini wa 1500 cc. Aidha, ieleweke kwamba kiwango hiki kwa watumiaji pikipiki ni kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali vile vile kwa kutoa pendekezo la utaratibu mbadala wa kutoza ushuru kulingana na ujazo wa injini za magari kuwa ***builting*** katika ushuru wa kuingiza magari nchini kulingana na viwango vya ujazo. Mapato yatakayopatikana yafidie ushuru wa bidhaa za mafuta. Tathimini ya eneo hili ikifanyika mapato yatakayopatikana yafidie ushuru utakaotozwa kwenye mafuta ya taa. Hatua zote hizi zinategemea udhibiti na usimamizi bora wa mapato katika *entry points* zote zinazotumika kuingiza bidhaa za magari nchini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kumnukuu baba wa Taifa *"it can be done, play your part" and so is TRA* wanaweza kufanya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia tena na kuhuisha utaratibu wa Makampuni yanayopata misamaha ya kodi za mafuta, gesi na misamaha mingine, ili kuboresha taratibu za ulipaji kodi wa Makampuni haya na kuongeza pato kwa Serikali. Kamati inakubali kuwa misamaha ya kodi kwa shughuli za kiuchumi ni sehemu muhimu ya kutoa motisha ya uwekezaji na uzalishaji. Ni muhimu basi kwamba malengo yanayokusudiwa yanafikiwa kutokana na misamaha hiyo. Kamati inaamini kuwa utaratibu huu wa misamaha ukifanywa kwa uangalifu makampuni husika yatafaidika na Serikali itafaidika *(win win situation)*, hatimaye mapato ya Serikali yataongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati wa kuongeza fedha zilizotengwa kwa sekta ya barabara. Uwezo wa sekta hii uimarike ili kuhakikisha fedha zilizotengwa zinasaidia kukwamua tatizo la mawasiliano baina ya eneo na eneo, pamoja na nchi jirani. Aidha, vipaumbele vilivyowekwa kwenye bajeti hii vikiandamana na matumizi mazuri ya raslimali

zilizotengwa, uchumi wetu utapata matunda ya haraka. Yote haya ni magizo yatokanayo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa. Naomba nitumie fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, (Mwenyekiti), Mheshimiwa Adam K. Malima, (Makamu Mwenyekiti) , Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Dk. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmoukh S. Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad R. Mohammed, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar S. Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dk. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Adam K. Malima,(Mb), Makamu Mwenyekiti kwa kunisaidia kuiongoza Kamati, Mheshimiwa Gaudence Kayombo Mb, Naibu Waziri, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Abdisalam Khatibu, Mb, Mheshimiwa Mustafa Mukulo, Naibu Mawaziri, Wizara ya Fedha. Aidha, naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara, Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa ushirikiano na mshikamano walionyesha kwa Kamati wakati wa kutekeleza majukumu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe mwenyewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Makatibu wa Kamati, Ndugu Anslem Mrema na Hellen Mbeba kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya taarifa ya Kamati ilihusika kuchambua Wizara zote mbili sasa nitamwita mwakilishi wa Kamati ya Upinzani tuanzie na yule atakayekuwa anahusika na Wizara zote mbili. Sasa naiita Kambi ya Upinzani.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda nitoe pongezi zangu za dhati kwa timu ya Taifa kwa ushindi iliyoupata juzi na naomba niwape moyo wahakikishe kwamba mechi ijayo dhidi ya Msumbiji wanashinda ili tuweze kwenda huko Ghana katika michezo ya mataifa huru ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu hotuba ya hali ya uchumi wa Taifa na Mpango wa Maendeleo na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43(5)(c) na 81(1), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kaskazini, viongozi wa Chama changu cha CHADEMA na Viongozi wa Kambi ya Upinzani na wananchi wengine wote wapenzi wa demokrasia kwa ushirikiano wao mkubwa kwangu na kunipa moyo katika kipindi cha mwaka mmoja toka Mkutano wa Bajeti uliopita. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Anne S. Makinda, (Mb.) pamoja na Mheshimiwa Samwel Sitta , (Mb.), kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge letu katika misingi ya kidemokrasia na kuhakikisha hadhi na uhuru wa Bunge vinalindwa. Tunaipongeza pia azma ya Mheshimiwa Spika ya kulifanya Bunge letu kuwa Bunge bora Afrika ifikapo mwaka 2011. Kambi ya Upinzani inamhakikishia Mheshimiwa Spika, ushirikiano mkubwa katika kutimiza lengo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa tena leo na kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Namwomba Mwenyezi Mungu atujalie afya njema na hekima ili tuwatumikie vema Watanzania. Mungu atupe busara ili tuwatumikie Watanzania bila kujali rangi, kabila, dini, jinsia, hali ya maungo, hali ya afya na bila kujali itikadi za vyama vyetu vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kupitia hotuba hii na Hotuba ya Waziri Kivuli wa Fedha inachambua kwa kina hali ya uchumi wetu na kutoa maoni ya upande wa pili wa shilingi kwa mujibu wa Kanuni zetu kama zinavyoonyeshwa katika Kanuni za Bunge, Toleo la 2004. Lengo kuu ni kutoa mchango wa Kambi ya Upinzani katika kukuza uchumi, kufanya uchumi uwe imara unaokua kwa kasi na kuimarisha jitihada za kuupiga vita umaskini miongoni mwa Wananchi wetu na kuboresha maisha ya Watanzania wote katika ujumla wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijadili hali ya uchumi wa nchi na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuboresha Mpango huo wa Taifa. Tunatoa mchango wetu tukizingatia kuwa tunaingia mwaka wa pili wa fedha toka serikali ya awamu ya nne ishike madaraka. Kambi ya Upinzani kwa upande wake imepata uzoefu wa kutosha na kupata uwezo mkubwa wa kuichambua bajeti ya Serikali na kupima uwezo na utayari wake katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa ujumla na Maoni ya Kambi ya Upinzani malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2006/2007 yalikuwa kama ifuatavyo:

Kwanza, tuliweka lengo la Pato halisi la Taifa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2006, napenda tu kusema kwamba tumevuka lengo hilo na pato la taifa limekuwa kwa asilimia 6.2. Kiwango hiki kilikadiriwa kwa kuzingatia kuwa, ukame, ukosefu wa umeme

na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia vingeathiri uchumi wetu. Kiwango cha kasi ya upandaji bei kilipangwa kisichozidi asilimia 4.0 ifikapo mwezi Juni mwaka 2007. Nasikitika kwamba tumeshindwa kufikia lengo hili kwa sababu mpaka mwezi uliopita kiwango cha upandaji bei kilikuwa zaidi ya asilimia 6. Mapato ya ndani kuongezeka kufikia asilimia 14.5 ya Pato la Taifa na kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni itakayokidhi mahitaji ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi saba lengo hilo pia tumeshindwa kulifikia kwa sababu mpaka sasa tuna hifadhi ya fedha za kigeni ambazo zinaweza zikalisaidia taifa kwa kipindi cha miezi mitano tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Uchumi Jumla katika Mwaka 2006/2007, Pato la Taifa kwa mujibu wa Taarifa ya Serikali lilifikia takribani sh. 15 trilioni kwa bei za mwaka 2006 ukilinganisha na *Tshs.* 13 Trilioni mwaka 2005. Kwa takwimu hii inaonyesha kuwa Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.2 na hivyo kuvuka lengo la ukuaji wa asilimia 5.9 lililotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi za Serikali zikiangaliwa kwa uangalifu utagundua kirahisi kabisa kuwa uchumi wetu haukukua jinsi ambavyo inaelezwa na taarifa za Serikali. Taarifa za Serikali zinaonyesha kuwa mwaka 2005 thamani ya shilingi ya Tanzania kwa dola moja ya Marekani ilikuwa sh. 1128.8 na wakati huo Pato la Taifa lilikuwa takriban sh. 13 Trilioni. Mwaka 2006, shilingi ya Tanzania ilikuwa na thamani ya sh.1251.9 kwa dola moja ya Marekani. Kwa bei za mwaka huo Pato la Taifa lilifikia *Tshs*. 15 Trilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi za Serikali, thamani ya shilingi ya Tanzania mwaka 2006 ilishuka kwa asilimia 10.9, hivyo thamani halisi ya Pato la Taifa 2006 kwa bei za mwaka 2005 ilikuwa chini pungufu kwa asilimia 10.9 ambayo ni *Tshs* 12.15 Trilioni tu. Tukilinganisha na Pato la Taifa la mwaka 2005 ambalo lilikuwa 13 Trilioni kwa bei za mwaka 2005, tutaona kuwa ukuaji wa Pato la Taifa uliporomoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchumi wetu umegawanyika katika sekta tisa . Sekta hizi ni Kilimo, Uchimbaji Madini, Bidhaa za Viwandani, Umeme na Maji, Ujenzi, Biashara na Mahoteli, Mawasiliano na Uchukuzi, Fedha na Huduma za Biashara na Uendeshaji wa Serikali. Kwa mujibu wa Takwimu za Serikali ukuaji wa kila sekta mwaka 2006 ni kama unavyoonyeshwa katika jedwali hili hapa chini.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Pato la Taifa (%) mpangilio kutokana na kasi ya ukuaji ni kama ifuatavyo:-

| **Na.** | **Sekta ya uchumi** | | **2005** | **2006** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uchimbaji Madini | | 15.7 | 16.4 |
| 2. | Ujenzi | 10.3 | 10.0 | |
| 3. | Biashara za Viwandani | | 9.0 | 8.6 |
| 4. | Biashara na Mahoteli | 8.2 | 8.4 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5. | Mawasiliano na Uchukuzi | | 6.4 | 7.5 |
| 6. | Fedha na Huduma za Biashara | | 5.3 | 5.5 |
| 7. | Uendeshaji Serikali | 5.1 | 5.1 | |
| 8. | Kilimo | 5.1 | 4.1 | |
| 9. | Umeme na Maji | | 5.1 | -1.8 |
| Jumla Pato la Taifa | | 6.7 | 6.2 | |

Chanzo: Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka, 2006 hadi Juni, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichambua takwimu katika jedwali hili hapo juu utagundua kuwa sekta ya Kilimo ambayo inachangia sehemu kubwa ya pato la taifa ukuaji wake umeporomoka kwa 1.0. Kwa kuwa Tanzania inapima uchumi wake kutokana na thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa nchini, kushuka huku kwa ukuaji wa kilimo kunaashiria kuporomoka kwa uzalishaji katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa tatu wa MKUKUTA. Ukuaji wa sekta ya kilimo ambayo ndiyo shughuli kuu vijijini uko katika hali ya kusuasua, unaonesha ni dalili mbaya katika juhudi za kupambana na umasikini. Sababu za ukame hazitoshi kuelezea upunguaji huu wa ukuaji katika sekta ya kilimo. Ni lazima sasa kama nchi tuamue maamuzi muhimu kwa ajili ya kuokoa kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta ya kilimo mwaka 2006 ulikuwa asilimia 44.7 tofauti na mwaka 2005 ambao ulikuwa asilimia 45.6. Nadharia za kiuchumi zinatuonyesha kwamba uchumi unaokua, mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi unapaswa kupungua mwaka hadi mwaka kwani ukuaji wa sekta nyingine kutokana na kupanuka kwa uchumi hupunguza mchango wa sekta ya Kilimo.

Hata hivyo, kwa Tanzania nadharia hii bado haifanyi kazi, hivyo, kupungua huku kwa Tanzania si dalili njema. Mchango wa sekta ya Kilimo katika pato la Taifa unashuka kutokana na ukame na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya Kilimo na Chakula. Hii inaonesha kuwa bado hatujafanya kazi sawa sawa katika kuleta mapinduzi ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za sensa za mwaka 2002/03 zinakadiria kwamba kuna jumla ya wakulima wadogo milioni 4.5 wanaolima takriban hekta milioni 44. Ukulima huu ni wa kifamilia zaidi, uzalishaji huu ni wa ubora wa chini na kwa ajili ya chakula tu (*subsistence*). Asilimia 70 ya wakulima wadogo wadogo hawana kipato kingine chochote nje ya kilimo na wengi wao wanatumia walichozalisha ingawa asilimia 70 tena wanauza kidogo katika walichozalisha.

Hivyo, kuna uongezaji thamani mdogo sana wa bidhaa za wakulima wadogo wadogo. Soko la bidhaa ni changamoto kubwa na vilevile kuna vikwazo vya kimuundo kama bodi za mazao na; au vyama dhaifu vya ushirika. Ni asilimia 8 tu ya wakulima wadogo wadogo wanaofanya kilimo cha umwagiliji na ni asilimia 3 tu wanapata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mingi ya mikopo hii ni kwa ajili ya mbolea, madawa na mbegu na kiasi kidogo sana ni kwa ajili ya vifaa (*machine*), nguvu kazi na umwagiliaji. Huduma za ugani zinafikia asilimia 35 tu ya wakulima wadogo wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya umaskini na maendeleo ya binadamu ya mwaka 2005 inaarifu kwamba tutaweza tu kupunguza umasikini iwapo ukuaji wa uchumi vijijini hususan sekta ya kilimo utakua kati ya asilimia 6 mpaka 8 kwa mwaka. Kwa hali ya sasa ilivyo ya uzalishaji katika kilimo hatutaweza kufikia malengo ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani Bungeni inapendekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa ili kuongeza uzalishaji katika kilimo na kuongeza ubora wa mazao ya kilimo:-

Moja, kuongeza ukuaji wa uchumi vijijini kwa kuhamasisha utangamano wa skimu za uzalishaji *(integrated production schemes)* ambazo zinahusisha upatikanaji wa pembejeo, teknolojia, huduma za ugani, usafirishaji na masoko.

Mbili, kuhamasisha uanzishwaji wa umoja wa wazalishaji wa mazao ili kuwapa sauti kubwa wakulima katika kutetea haki zao. (*Makofi*)

Tatu, kutoa vivutio (*incentives*) kwa taasisi za kifedha zitakazotoa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji mkubwa katika kilimo.

Nne, kutenga rasilimali nyingi zaidi kutoka katika bajeti ya nchi kwa ajili ya kilimo na shughuli zinazohusiana na kilimo. Waziri kivuli wa Fedha na Waziri Kivuli wa Kilimo watawasilisha makadirio ya rasilimali za kwenda kwenye kilimo kutokana na muono wa kambi ya Upinzani kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya madini mwaka jana ilikua kwa asilimia 16.4. Mwaka 2005 sekta hii ilikua kwa asilimia 15.7. Hata hivyo, ukuaji wa sekta ya madini hauendani na ukuaji wa ajira na kupungua kwa umaskini. Kama nilivyosema mwaka jana katika hotuba yangu ukuaji wa sekta ya madini hauendani na ukuaji wa ajira na kupungua kwa umaskini.

Taarifa ya hali ya umasikini nchini inaonesha kuwa sekta ya madini inachangia ajira chini ya asilimia moja. Yaani katika kila ajira 100 zinazotengenezwa nchini katika mwaka, sekta ya madini inachangia chini ya mtu mmoja katika ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasababishwa na sababu moja kubwa kuwa sekta ya madini na migodi haina uhusiano mzuri na sekta nyingine za uchumi yaani *forward and backward linkages*.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kwamba mgodi mpya wa Kabanga wa *Nickel* ni moja ya miradi mikubwa sana duniani lakini uliopo katika eneo la mbali na lisilo na miundombinu. Serikali bado haijaonyesha juhudi yoyote katika Bajeti ya mwaka huu ya kufungua miundombinu kwa mikoa ya Magharibi ili kuwezesha *Nickel* itakayochimbwa kufika bandarini Dar es Salaam na Tanga.

Kwa mujibu wa Taarifa kutoka *Economists Intelligence Unit (EIU)* ya mwezi Machi, 2007 *(Tanzania at a Glance 2007-2008),* wawekezaji wa mradi huo kampuni za *Barrick Gold* ya Kanada na Xstrata ya Uingereza na Uswizi walitangaza katikati ya mwezi Februari kuwekeza dola milioni 95 zaidi ili kufanikisha mradi huo. Uwekezaji huu ni muhimu sana kwa Tanzania kwani utatuondolea utegemezi wa dhahabu kwa kiasi kikubwa katika mauzo yetu ya nje. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mkataba wa wawekezaji hawa wa mgodi wa *Nickel* wa Kabanga unazingatia kwa kiasi kikubwa maslahi ya Tanzania na kuepuka makosa yaliyofanywa katika migodi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Kambi ya Upinzani inasikitika kuwa haijazungumzia kabisa Sekta ya mafuta na gesi asilia kwa kina. Mwaka jana kampuni ya Kifaransa inayoitwa *Maurel & PROM* ilitangaza kugundua gesi yenye takriban ujazo wa *Cubic* futi 5 trillioni katika Wilaya ya Mkuranga, katika shimo la *Mkuranga one*. Gesi hii ingekuwa ni sababu tosha kabisa kiuchumi kugeuza *IPTL* kutoka kwenye matumizi ya mafuta kwenda kwenye matumizi ya gesi na hivyo kupunguza gharama za umeme na pia kupunguza matumizi makubwa ya serikali katika sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, bado kuna makampuni mengi sana yanaendelea kutafuta mafuta katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Yako Makampuni ambayo tayari mikataba yake ya uzalishaji (*Production Sharing Agreement (PSA)* imesainiwa na mengine ndio kwanza yameomba kufanya utafiti tena katika maeneo ambayo hata hatukutegemea. Kwa mfano, kampuni ya *TULLOW Oil* kutoka nchini Ireland imeomba kutafuta mafuta katika eneo la Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika *(Lake Tanganyika- East Block A)* na kwa mujibu wa taarifa zilizopo katika tovuti ya shirika la petroli nchini, mkataba wa uzalishaji *(PSA)* ulipaswa kusainiwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2007. Taarifa kama hizi ni muhimu kutolewa Bungeni katika taarifa ya hali ya uchumi ikitaja angalau maombi ya kutafuta mafuta nchini yako kiasi gani na utafutaji unaendeleaje. Hii itasaidia sana kutuondolea matatizo huko baadae kuhusiana na mikataba ya wawekezaji hao na vile vile ingetusaidia kushirikisha wananchi wa maeneo husika katika kuandika mikataba ambayo itakuwa na faida kwao. Hata hivyo naipongeza kampuni ya *TULLOW* na shirika letu la *TPDC* kwa kuamua kutafuta mafuta katika mkoa wa Kigoma. *Inshallah* yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba imefika wakati Serikali kuwekeza katika viwanda vya kuongeza thamani ya bidhaa za madini yetu kwa kushirikiana na sekta binafsi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kimkakati kununua hisa za kati ya asilimia 10 na 20 katika migodi yote ya madini hapa nchini, na hatimaye kuhamishia Hisa hizo kwa wananchi kadri wanavyopata uwezo kiuchumi kwa lengo la kuwanufaisha wananchi

na rasilimali ya nchi yetu. Vile vile, tunaitaka Serikali kupiga marufuku usafirishaji wa mchanga wa madini kwenda nje ya nchi kunakofanywa na makampuni ya madini, kwani usafirishaji huu unalipotezea Taifa fedha nyingi na maliasili zake.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 8.6 kwa mwaka 2006 ikilinganishwa na asilimia 9 kwa mwaka 2005. Serikali inasema kwamba upunguaji huu ulitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kulikoambatana na mgao wa umeme hasa kwa viwanda ambavyo viko katika maeneo ya makazi ya watu. Vile vile, takwimu za Serikali zinaonesha kwamba mchango wa sekta ya bidhaa za viwandani uliongezeka kutoka asilimia 9 mwaka 2005 mpaka asilimia 9.2 mwaka 2006.

Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani kutokana na taarifa za kiuchumi zilizowasilishwa na Serikali mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa umeongezeka kwa sababu uzalishaji katika kilimo umeshuka lakini katika hali halisi mchango wa sekta hii haujaongezeka. Ni dhahiri sekta moja ikishuka, kitakwimu sekta nyingine itaonekana kupanda. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuhusu hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume na maelezo ya Serikali hali halisi ya uchumi inaonesha kwamba ukuaji wa sekta ya viwanda ambayo ni sekta muhimu sana katika uchumi wa nchi uliporomoka. Kushuka huku kwa ukuaji wa sekta ya viwanda kunathibitisha athari za mgao wa umeme zilizoikumba Taifa letu kinyume na kauli za Serikali kwamba mgao wa umeme haukuathiri uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi mbalimbali ambazo zinaendelea katika sekta hii, Kambi ya Upinzani inaamini jitihada za kutosha hazijafanywa katika mazingira bora ya uwekezaji katika eneo la kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo *(Agro Processing).* Taifa letu linapoteza mapato mengi kwa kuuza bidhaa ghafi. Uwekezaji katika eneo hili utasaidia sana kupanua uchumi wa maeneo ya vijijini *(Rural Economy)* na wakati huo huo kukuza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetueleza hapa kwamba uzalishaji wa ngozi ulipungua kutoka vipande milioni 3.7 mwaka 2005 hadi vipande milioni 3.4 mwaka 2006. Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali upungufu wa ngozi ulisababishwa na ukame ambao ulisababisha upungufu mkubwa wa malisho na vyakula vya mifugo na hivyo kupelekea kupungua kwa wanyama waliochinjwa na wanaotoa ngozi.

Kambi ya Upinzani haikubaliani na sababu hizi zilizotolewa kwa sababu takwimu za Serikali zinaonesha kuwa uzalishaji wa nyama uliongezeka kwa asilimia 2.6. Huwezi kupata nyama zaidi kama hujachinja mifugo. Kwa ongezeko la uzalishaji wa nyama linapaswa kuendana sambamba na uzalishwaji wa ngozi na kimsingi, wakati wa ukame wanyama huchinjwa zaidi kwa ajili ya chakula na hivyo tungetarajia ukame utupatie ngozi nyingi zaidi. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kutoka Serikalini kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilonalo katika sekta hii ya mifugo ni kwamba Serikali inakusanya asilimia 60 tu ya ngozi zote zinazozalishwa na asilimia 20 tu ya makusanyo yote ya ngozi ndiyo inayosindikwa. Mbaya zaidi, ubora wa ngozi zetu ni wa daraja la 3 na la 4. Katika mwaka wa fedha unaoisha pato linalotokana na bidhaa za ngozi limefikia shilingi bilioni 16.18 wakati kwa maoni ya Kambi ya Upinzani sekta hii inao uwezo wa kuliingizia Taifa mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 96.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya mkakati madhubuti zaidi ili kuboresha zao hili. Moja ya mkakati huo ni pamoja na kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya sekta ya mifugo na kuhamasisha wafugaji kuunda ushirika wenye nguvu ili sio tu kutetea maslahi yao bali pia kuboresha ubora, uzalishaji na kutafuta soko la ngozi. Kambi ya Upinzani inapendekeza kufikia lengo la ukuaji wa asilimia 5 mpaka 6 katika sekta hiyo. Maoni kamili ya Kambi ya Upinza ni katika eneo hili yatawasilishwa Waziri kivuli wa Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006 sekta ya umeme na maji iliathirika sana. Ukuaji katika sekta hii uliporomoka kutoka asilimia 5.1 mpaka *negative -1.8.* Ni dhahiri, janga la mgao wa umeme lilichangia sana kuporomoka kwa sekta hii. Sekta nyeti kama hii, kuporomoka kiasi hiki ni janga kwa Taifa. Janga hili halihitaji suluhisho la dharura tu, ni lazima tuwekeze katika miradi mikubwa yenye kudumu kwa muda mrefu.

Kwa mfano, kwa miaka mingi wataalamu na wananchi mbali mbali wameshauri uwekezaji mkubwa wa kuzalisha umeme kwa njia ya maji katika Mto Rufiji katika maporomoko ya *Stigler's Gorge*. Licha ya kwamba mradi huu unahitaji mkakati wa muda mrefu, lakini huu ni mwaka wa pili wa Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Nne. Mradi huu hautajwi kabisa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze ni mkakati gani hasa imeweka katika utekelezaji wa Mradi huu wa *Stigler's Gorge* na miradi mingine ya umeme badala ya kuwekeza katika miradi ya dharura tu ambayo tunaamini inafaidisha watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani pia wakati sasa umefika kuangalia uwezekano wa kuifanya mikoa ama mmoja mmoja au kikanda ijitegemee katika uzalishaji wa nishati ya umeme. Hii itasaidia kuondoa balaa la nchi nzima kuathirika kunapotokea janga la ukame kama ilivyotokea mwaka 2006 na kuwezesha viwanda kufanya *relocation* pale inapobidi. Njia hii pia itachochea maendeleo sawia kwa mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli ikijumuisha utalii ilikua kwa asilimia 8.4 mwaka wa 2006 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2005. Taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa kukua kwa sekta hii kulichangiwa zaidi na kuboreshwa kwa mazingira ya kufanya biashara pamoja na kuongezeka kwa shunguli za utalii, taarifa inaendelea kuonyesha kwamba jumla ya watalii 644,124

waliingia nchini mwaka 2006 ikilinganishwa na watalii 612,754 mwaka wa 2005. Mapato yaliyotokana na utalii ni dola za marekani 862.0 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii, mwaka 2006 wakati nawasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hali ya uchumi nchini nilieleza tatizo la upotevu wa mapato kutokana na sekta ya utalii kupitia kitu kinachoitwa *package tourism.* Taarifa kutoka kwa wadau wa sekta ya utalii zinaonyesha kuwa katika kila mtalii mmoja anayeingia Tanzania kwa siku moja dola 100 za Kimarekani inabaki katika nchi ya Ulaya au Marekani kwani watalii hivi sasa kupitia mfumo huu wa *package tourism* wanalipia kila kitu wakiwa huko kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukilinganisha idadi ya watalii wanoingia Tanzania na mapato ya utalii yaliyorikodiwa mwaka 2006 utagundua kuwa kila mtalii aliyeingia Tanzania alitumia dola za Kimarekani 1338 tu, hii haingii akilini. Iwapo kila mtalii alikaa nchini siku saba tu na iwapo nusu ya watalii walitumia mfumo huu wa *package tourism* na hivyo kila mtalii kulikosesha Taifa dola za Kimarekani 100 kila siku. Kwa takwimu za mwaka 2006, Taifa lilipoteza mapato ya dola za Kimarekani milioni 225. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ndogo ya uwindaji wa kitalii kumetokea malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi. Sekta hii imekuwa ni chanzo cha mapato mengi ya Serikali kupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani katika maoni yake ya Bajeti itakayosomwa muda mfupi ujao inadhani kuwa Taifa lingeweza kukusanya mapato mengi zaidi katika sekta hii na ili lengo hili lifanikiwe, pamoja na mambo mengine hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa:-

Moja, sheria ya uhifadhi wa wanyamapori ya mwaka 1974 kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho makubwa na au kuifuta na kuitunga upya. Sheria mpya itoe kipaumbele kwa Watanzania katika *TASNIA* ya uwindaji wa kitalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ifikapo mwisho wa kipindi cha umilikaji vitalu, vitalu vyote virudishwe Serikalini kwa ajili ya ugawaji mpya na kampuni za uwindaji za Watanzania zipewe fursa na nafasi ya kwanza kushindania umiliki wa vitalu. *(Makofi)*

Taratibu za ugawaji wa vitalu ziwe wazi ikiwa ni pamoja na kutangaza vitalu vilivyo wazi na biaonuwai zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaongeza juhudi za kutangaza zaidi vivutio vya utalii vilivyopo nchini mwetu na hivyo kufikia lengo la kuwa na idadi ya watalii milioni moja kwa mwaka, ni vyema Serikali ikachukua hatua za makusudi kudhibiti upotevu huu wa mapato yatokanayo na utalii. Waziri Kivuli wa Fedha na Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii wataelezea mapendekezo ya mikakati maalumu itakayopelekea kuongeza mapato zaidi kutokana na sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Serikali inaonyesha ya kwamba thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kwa asilimia 2.8. Ongezeko hili, kwa mujibu wa Serikali, lilichangiwa zaidi na bidhaa zisizo asilia kama dhahabu na bidha za viwandani. Naomba nichukue fursa hii kufanya uchambuzi kidogo kuhusiana na mauzo yetu nje ya nchi kwa kupitia jedwali ambalo lipo katika taarifa ambayo nimewapatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichunguza kwa makini jedwali ambalo nimewapatia utaona dhahiri kabisa kwamba ni bidhaa mbili tu, yaani Madini na Samaki, zinazochangia takribani asilimia 55.7 ya mauzo yetu yote ya nje. Kwa uchumi wowote ule unaokua na wenye lengo la kunufaisha watu wengi zaidi mwenendo huu wa mauzo ya nje unatisha. Mbaya zaidi sekta hizi zinazochangia zaidi ya nusu ya mauzo yetu nje ziko mikononi mwa watu wachache na wengi wao kutoka nje. Hivyo Watanzania walio wengi na wanyonge hawafaidiki moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifanya uchunguzi zaidi katika takwimu nilizotoa hapo juu utaona kuwa, mauzo yetu ya nje yanachangiwa kwa zaidi ya nusu na bidhaa ambazo zinazotoka sehemu moja ya nchi. Sote tunafahamu kwamba madini na samaki ambazo zinachangia asilimia yote zinatoka katika mikoa ya kanda ya Ziwa, Shinyanga, Mwanza, Mara na Kagera. Ukiongeza mchango wa Pamba na Kahawa kutoka eneo hili la nchi mchango wake katika mauzo ya nje unafikia takribani asilimia 60 ya mauzo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii siyo nzuri kwa umoja na mshikamano wa taifa letu wachochezi wachache wanaweza kuanza kudai sehemu kubwa ya mapato yanayotokana na mauzo nje yarudi maeneo hayo na hii inaweza kuhatarisha amani yetu. Hivyo ni lazima Serikali ichukue hatua za haraka kurekebisha hali hii kwa kuhamasisha uzalishaji katika mikoa mingine na mazao mengine na hasa mazao ya kilimo na hivyo kuongeza pato la mauzo kutoka nje na kwa muda huo huo kuongeza usawa wa kiuchumi miongoni mwa mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuanza kutumia bajeti ya nchi ili kuchochea uzalishaji wa bidha za Viwandani na Mashambani na hivyo kuongeza mauzo ya bidhaa nje yaani *(budget as a policy instrument)*. Baada ya muda mfupi ujao Waziri Kivuli wa Fedha atawasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu taratibu makini kwa ajili ya kuchochea uzalishaji katika uchumi na mauzo ya nje kupitia Bajeti ya Serikali jambo ambalo haliko wazi katika Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha juzi. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Serikali kutoka Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji inaonyesha kuwa katika mwaka 20006/2007 kulikuwa na jumla ya kilomita 9,000 za barabara kuu na Kilomita 18,000 ya barabara za mikoa zilizofanyiwa ukarabati katika kipindi cha Mwaka wa Fedha umekwisha. Kwa mujibu wa taarifa hii katika mwaka wa fedha unaomalizika hakuna hata kilomita moja ya barabara ya lami ambayo imetengenezwa na Serikali ya Awamu ya Nne. Serikali ya Awamu ya Nne ilifanya ukarabati tu wa barabara na haijatengeneza hata kilomita moja ya barabara katika kipindi cha mwaka nzima wa fedha uliopita. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Serikali Awamu ya Pili, Rais wa Serikali ya awamu ya pili, ndugu Ali Hassan Mwinyi mara baada ya kushika uongozi wa nchi yetu aliulizwa na waandishi wa habari wa vyombo vya magharibi juu ya vipaumbele vya utawala wake akawajibu kwa kusema 'Kipaumbele changu cha kwanza ni barabara, kipaumbele changu cha pili ni barabara, na kipaumbele changu cha tatu ni barabara'. Rais wa awamu ya tatu ndugu Benjamin Mkapa ambaye ndiye aliyenukuu maneno haya mtangulizi wake wakati alipokuwa akikabidhiwa Uenyekiti CCM naye pia akasema vipaumbele vyake ni Barabara, Ukuaji wa uchumi na Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kwamba katika moja ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Nne swala la miundombinu ya barabara halipo na hii inathibitishwa na hatua ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kutojenga angalau kilomita moja ya barabara mpya na badala yake kuendelea kukarabati Barabara ambazo zimetengenezwa na Serikali ya Mzee Mwinyi na Mheshimiwa Mkapa. Kama ipo barabara mpya iliyofunguliwa, Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda Taarifa hiyo itolewe kikamilifu ndani ya Bunge hili Tukufu. Katika hili la miundombinu na barabara Kambi ya Upinzani inapendekeza vipaumbele katika barabara zifuatazo:- *(Makofi)*

Maoni ya Kambi ya Upinzani ni kuwa kwa mwaka huu wa fedha asilimia 21 ya bajeti itengwe kwa ajili ya miuondombinu ya barabara kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi. Vipaumbele ni katika kufungua maeneo ya nchi ambayo hajafunguliwa ya kutosha au hata kabisa kwa muda mrefu sasa. Hivyo, tofauti na Mpango wa Serikali katika Bajeti ya Serikali 2007/08 maoni ya mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya barabara, pamoja na kuendeleza miradi iliyopo, kufungua miradi ya ujenzi katika barabara muhimu zifuatazo:

Moja, Masasi-Tunduru-Songea mpaka Mbamba Bay, Tunduma- Sumbawanga-Mpanda mpaka Kigoma. Kigoma-Tabora mpaka Manyoni. Mbeya-Sikonge mpaka Nzega. Iringa-Dodoma-Kondoa mpaka Babati. Babati-mpaka Singida na Oldeani-Matala mpaka Lalago. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote vile miradi hii inahitaji fedha nyingi sana na haiwezi kuisha kwa haraka na kwa pamoja kwa wakati moja. Hata hivyo ni lazima kuanza ili kuendelea kuipangia fedha za maendeleo katika kila mwaka wa bajeti mpaka zitakapo kamilika. Uwekezaji huu utalipa kwani utaifungua nchi yetu, utaongeza uzalishaji na kupanua uchumi wetu. Waziri Kivuli wa Fedha na Waziri Kivuli wa Miundombinu watatoa maelezo ya zaidi juu ya utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukua kwa uchumi kuwe na manufaa kwa Watanzania ni lazima serikali kwa makusudi kabisa iamue kuweka sera rafiki kwa masikini *(pro-poor policy).* Sera rafiki kwa watu masikini ni zile sera zinazoelekea kuweka rasilimali katika sekta zinazokua na zinazoajiri watu wengi zaidi. Kilimo ni sekta pekee inayoweza kuondoa umasikini nchini Tanzania. Hivyo, lazima maamuzi ya makusudi yafanywe ili kuwekeza rasilimali za kutosha kabisa katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Naibu kwa mujibu wa utafiti wa nguvu kazi uliofanyika mwaka 2005/2006 hivi sasa Tanzania Bara ina jumla ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi wanaofikia milioni 20.6. Utafiti huo unaonyesha kuwa wastani wa ongezeko la watu katika soko la ajira kila mwaka ni watu 760,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa kwa mara ya kwanza baada ya muda mrefu sasa tunayo Tafsiri ya Taifa ya Ajira, kwa viwango vya *ILO*. Tafsiri hiyo inazingatia mazingira ya ajira katika Tanzania ambapo sehemu kubwa ya watu wanafanya kazi za kujiajiri badala ya kuajiriwa, na kazi nyingi ni za msingi katika sekta ya kilimo na sekta isiyo rasmi. Kati ya watu milioni 20.6 wenye uwezo wa kufanya kazi, watu milioni 18.3 walikuwa wana kazi na watu milioni 2.3 hawakuwa na kazi. Kwa mujibu wa tafsiri hiyo 11% ya Watanzania hawana kazi. Katika jiji la Dar es Salaam 31.4% ya watu hawana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndugu Jakaya Mrisho Kikwete, wakati wa kampeni zake aliahidi kutengeneza ajira 1,000,000 katika kipindi cha miaka 5. Hii ni sawa na ajira 250,000 kila mwaka kuanzia mwaka 2006 mpaka 2010. Nasikitika kwamba Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika Hotuba yake na hata katika Taarifa ya Hali ya Uchumi haikuelezea ni ajira ngapi zimetengenezwa kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na kama tumefikia malengo ya mwaka kwa mujibu wa ahadi ya Mheshimiwa Rais na ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Hata kama tungeweza kutimiza lengo la kuwa na ajira 250,000 bado hii ingelikuwa ni 33% tu ya Watanzania wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka. Taarifa ya Hali ya Uchumi inaelezea tu 'kuwa Serikali itawashirikisha vijana katika kuanzisha na kutekeleza mipango, mikakati na Programu mbalimbali. Hii ni lugha iliyozoeleka miaka nenda rudi na haitoi sana matumainikuwa lengo la Millioni moja (1) itafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa tatizo la ajira lianze kutazamwa kwa muono mpana zaidi na tunashauri katika mwaka huu ujao wa fedha mchakato wa kuchambua upya sera ya Taifa ya ajira uendane na mjadala wa kitaifa kuhusu ajira, ujira na tija. Tatizo la Ajira ni 'Bomu' linaloweza kulipuka wakati wowote lisiposimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imefurahishwa sana na uamuzi wa kurudisha miliki ya Kampuni ya Ndege Tanzania katika serikali. Uamuzi huo ni ushahidi tosha wa kwamba tulifanya maamuzi mengi mabaya sana katika ubinafsishaji wa mashirika yetu ya umma. Pia umetugharimu sana. Linalotusikitisha ni kwamba wahusika waliofanya maamuzi haya mabovu hawajachukuliwa hatua zozote. Kambi ya upinzani inapendekeza kutenga fedha za kutosha kabisa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2007/2008 kulifanya Kampuni ya ndege Tanzania lifanye kazi zake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006 Shirika la Reli Tanzania lilisafirisha mizigo tani 775,281 ikilinganishwa na tani 1.1 mwaka 2005. Usafirishaji wa mizigo ulipungua kwa takriban asilimia 34. Upungufu huu ulitokana kwa kiasi kikubwa na Treni ya abiria kuanzia safari zake Dodoma badala ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kwa tathmini hii nchi yetu haiendi mbele bali inarudi nyuma. Hebu tujiulize, wakati tunapata uhuru treni ilikuwa ikitoka Kigoma inatia nanga Dar es Salaam. Leo, miaka 45 baada ya uhuru, treni ikitoka Kigoma inaishia Dodoma. Twaenda mbele au twarudi nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea taarifa kwamba hatua ya ukodishaji wa shirika la reli kwa kampuni ya *RITES* ya India sasa imekamilika. Tunatoa angalizo ya kwamba pamoja na kuwa matumaini ni kuwa mwekezaji ataborasha miundombinu ya reli na kununua vichwa vipya, kubadilisha line na mitambo iliyochakaa, ni vigumu mwekezaji ambaye nia yake ni biashara kufanya haya yote Angalizo hii iwe Ilani kwa Serikali kusimamia kikamilifu zoezi la Ukodishaji wa Reli yetu, na kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ukodishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini Serikali itakuwa tayari kuleta taarifa ya mara kwa mara Bungeni ili kuona jinsi utekelezaji huo unavyoenda kulingana na matarajio yetu. Kambi ya upinzani inapendekeza mkakati maalum ubuniwe ili kuongeza uwezo wa reli yetu ili kusafirisha mizigo ya kutosha kutoka nchi jirani za Burundi na *DRC.* Reli ya kati inalipa sana kiuchumi, changamoto ni kuwekeza katika reli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu 2006/2007 nilizungumzia kuhusu taarifa ya hali ya umasikini nchini na kutaka iwe sehemu ya taarifa ya hali ya Uchumi. Katika kitabu cha Hali ya Uchumi mwaka 2006, suala la umasikini limeongelewa sanjari na utekelezaji wa MKUKUTA. Kasi ya upunguaji wa Umasikini bado ni ndogo mno. Hata hivyo kitakwimu, kasi ya upunguaji wa umasikini mijini ni kubwa zaidi kuliko ile ya vijijini japo katika hali halisi mambo yanaweza kuwa tofauti kabisa, hasa kwa upande wa umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kugawa rasilimali zetu kulingana na *clusters* za MKUKUTA, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa hali ya umaskini kiwilaya izingatiwe katika kugawa rasilimali za Bajeti. Kambi ya Upinzani inatambua kuwa fedha zinazokwenda katika Serikali za Mitaa zinagawiwa kwa *formula* maalum, iliyo wazi na yenye kueleweka kwa kila moja, badala ya *formula* ya sasa ambapo Wilaya inaweza kukosa fedha kutokana na vigezo ambavyo havitokani moja kwa moja na wilaya yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe hali ya umasikini kiwilaya kwa wananchi kwa kigezo cha idadi ya wananchi walio katika Umaskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukua kwa uchumi kuwe na manufaa kwa Watanzania ni lazima serikali kwa makusudi kabisa iamue kuweka sera rafiki kwa masikini *(pro-poor policy).* Sera rafiki kwa watu masikini ni zile sera zinazoelekea kuweka rasilimali katika sekta zinazokua na zinazoajiri watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni sekta pekee inayoweza kuondoa umasikini nchini Tanzania. Hivyo, kama Kambi ya Upinzani ilivyopendekeza lazima maamuzi ya makusudi yafanywe ili kuwekeza rasilimali za kutosha kabisa katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama wa mashirika ya kikanda na ya kimataifa. Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* Utekelezaji wa itifaki ya ushuru wa forodha inaendelea kutekelezwa na maandalizi ya itifaki ya Soko la Pamoja inafanyiwa kazi. Uamuzi wa kuruhusu nchi za Rwanda na Burundi kuwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umepokelewa kwa hisia tofauti na wananchi wa Tanzania.

Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kuwa uanachama wa nchi hizi katika EAC utatusaidia sana Tanzania kwani uamuzi huu utakuza soko la bidhaa la ndani la eneo letu. Tanzania ianze kuangalia uwezekano wa kuishawishi nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili nayo ijiunge na Jumuiya ya Afrika Mashariki na hatimaye kuwa na Soko la Pamoja na Maziwa Makuu *(Great Lakes Community ie glcom)* na kisha umoja wa Sarafu. Tukipata soko la pamoja kutoka Bahari ya Hindi mpaka Bahari ya Atlantik, chumi za nchi yetu zitapaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi zote za Afrika Mashariki zipo katika mjadala kuhusuu Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Ni imani yangu kuwa maoni ya wananchi yatazingatiwa katika ripoti ya Kamati ya Rais ya Uharakishaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwa Watanzania ni kuepuka unyonge na kujiona sisi tupo nyuma kwa kila kitu na badala yake kuweka mikakati thabiti ya kufaidika na Shirikisho kama litakuja leo au kesho vyovyote itakavyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inarejea ushawishi wake wa kutaka nchi yetu irejee uanachama katika *COMESA*. Vile vile ijadiliane kuhusu *Economic Partnership Agreements (EPA)* kupitia kundi la nchi za ESA. Lengo ni kuwa katika soko kubwa litakalochochea uzalishaji wetu wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuitangaza nchi ni muhimu sana katika kushawishi uwekezaji nchini. Kituo cha Uwekezaji, *TIC* bado kina changamoto kubwa. Ni lazima tutumie pesa nyingi kujitangaza. Kuna ushindani mkubwa katika kila nchi kujitangaza, wengine hata majimbo hujitangaza, mfano Jamhuri ya Afrika Kusini. Lazima tuchangamke sasa katika ulimwengu huu wa ushindani kama tunataka wawekezaji wa maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *MCC* utasaidia sana kuboresha miundombinu, kusambaza huduma za maji na kuondokana na tatizo la umeme.

Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kabla ya kuwasilisha *'compact proposal'* kwa Serikali ya Marekani, ni vema Waheshimiwa Wabunge ama kupitia Bunge zima au

katika Kamati husika waone, kujadili na kupitisha mpango huo. Uwazi katika Miradi ya Maendeleo ni kitu muhimu sana ili kuondoa hisia za upendeleo kwa baadhi ya maeneo.

Nnaomba hotuba yangu hii irekodiwe kwa mujibu wa Taarifa iliyogawiwa na siyo jinsi ambavyo nimesoma. Kwani inabidi sasa nitoe muda wa kutosha kwa Waziri Kivuli wa Fedha ili aweze kuja na kutusomea Taarifa yake kuhusiana na Mapato na Makadirio ya Bajeti ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama alivyokuwa ametangaza Mheshimiwa Spika, kwamba tutakuwa na vijana wetu wa *Taifa Stars* watakaokaribisha humu ndani ya Bunge. Kwa hiyo, ninamwachia Mheshimiwa Spika kiti, ninaomba mvumilie. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Tulikuwa tumekwishasikia msemaji mmoja na wako wawili. Sasa naarifiwa kwamba wale wageni wetu wa Timu ya Taifa wamekwishawasili. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani itakuwa si vizuri Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani azungumze, nimkatize na pengine haitakuwa vizuri. Kwa hiyo, namwambia *Serjeant-At-Arms* anipe taarifa mara moja ili tuweze kufanya utaratibu wa kuwapokea wageni hawa.

Au bado mnifahamishe basi. Bado, kwa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, bahati mbaya kwake ni kwamba Mheshimiwa Zitto ameitumia nusu saa yake. Imekaribia nusu saa nadhani. Ni kweli dakika ishirini. Tutapata, tuna *time* hapa. Kwa hiyo, una nusu saa na ushee tu. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI, OFISI YA WAZIRI MKUU, FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Bajeti ya Fedha kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Wawi kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi walizonikabidhi katika kipindi cha 2005 hadi 2010. Nawaahidi nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 14.06.2006 Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alifanya mazungumzo na Wabunge wa CCM na hatimaye Wabunge wa Kambi ya Upinzani. Katika kikao hicho pamoja na mambo mengine mengi, Rais aliendelea kutoa ahadi yake ya kuumaliza mpasuko wa kisiasa ulioko Zanzibar na kusema "Tumeisha anza, siyo rahisi sana lakini tutaumaliza." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani itaendelea kuunga mkono juhudi za Rais katika kuutafutia ufumbuzi mpasuko wa kisiasa wa Zanzibar pamoja na kero za

Muungano, ila Kambi ya Upinzani ingelipenda kuweka bayana kwamba imani ya Watanzania inaendelea kupungua siku hadi siku kutokana na ahadi kama hizo kutolewa na Rais aliyemtangulia na pia kutokutekelezwa kikamilifu kwa miafaka ya 1999 na 2001 kati ya CCM na CUF. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais mwenyewe ameahidi kutembea kwenye maneno yake, sisi Kambi ya Upinzani tunapongeza hatua zilizochukuliwa za kuanza mazungumzo ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mpasuko wa kisiasa Zanzibar, ila tunawaomba wale walioko kwenye mazungumzo pamoja na mimi mwenyewe waelewe kuwa muda umekuwa kuwa muda umekuwa mrefu, ni vyema Watanzania wakajua hatua iliyofikiwa ili kuondoa shaka juu ya mazungumzo yanayoendelea.Watanzania walio wengi wanapenda kuwa na imani na kauli ya Rais, na Sisi katika Kambi ya Upinzani tunaahidi kuzidi kufuatilia kwa karibu mwenendo mzima wa mazungumzo huku tukielewa kuwa muda wa subira unazidi kuyoyoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kukushukuru wewe, Naibu wako na Watendaji wa Ofisi yako, wakiongozwa na Katibu wa Bunge, kwa kutupatia fursa mbali mbali sisi Wabunge kujifunza shughuli za mabunge ya wenzetu. Moja tulilojifunza katika mabunge mengi, Kambi ya Upinzani huwa inapata fursa ya kutoa bajeti mbadala, lakini kutokana na Kanuni zetu kwa bahati hilo haliruhusiwi. Kwa hiyo, tutaendelea na taratibu za kuishauri Serikali na tunaamini itatusikiliza.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa kifupi kuwakumbusha Watanzania kwa kupitia Bunge lako Tukufu, kwamba nchi yetu ilipata uhuru mwaka 1961 na kuwa *Republic of Tanganyika* na Zanzibar 64 tukapata Serikali ya Mapinduzi. Bahati nzuri TANU na ASP hatimaye zote zilirithiwa na CCM.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakhia Hamdan Meghji, Mbunge, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake, pamoja na wakuu wa vitengo na asasi zilizochini yao kwa kazi nzito ya maandalizi ya Bajeti hii pamoja na kwamba Kambi ya upinzani ina maoni tofauti katika baadhi ya maeneo ya wigo wa mapato ya ndani, kodi katika mafuta, na viwango vya mishahara ya wafanyakazi wa chini na mapato yatokanayo na raslimali zetu.Tofauti hizo nitazielezea baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii fupi kuwakumbusha Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu, kuwa tokea Nchi yetu ipate Uhuru (Tanganyika) 1961 kukawa na "*Republic of Tanganyika"* na baada ya Mapinduzi Zanzibar 1964, kukawa na *"People's Republic of Zanzibar"* na hatimaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Nchi yetu imeongozwa na TANU na ASP na hatimaye CCM. Hivyo ni dhahiri kuwa mafanikio na mapungufu yote ya maendeleo ya Nchi yetu yametokana na Uongozi na Sera za CCM, ambayo ni mrithi wa TANU na ASP.

Mheshimiwa Spika ni wajibu wetu sote kujiuliza, katika kipindi hichi chote cha uongozi wa aina moja. Je kwa sera tulizokuwanazo Mtanzania wa kawaida maisha yake yameboreka? Kwamba sasa anaweza akapata angalau milo miwili bila ya wasi wasi?

Mwananchi wa kawaida anaweza akasomesha watoto wake na watoto hao wakasoma vizuri na hatimaye wakapata elimu inayokubalika? Au anaweza kujiajiri kwa kupata mikopo kwa urahisi yenye riba nafuu? Haya ni masuala ya msingi ya kujiuliza sisi Watanzania. Tunaposema haya hatusemi kwamba Tanzania hakuna maendeleo. Au Anaweza kupata huduma ya kijamii bila ya kulipia kwa gharama kubwa na kama anaweza kupata bei muafaka ya mazao yake kwa kuuza anakotaka kama ilivyokuwa kabla ya Uhuru na Mapinduzi? Je hata anayefanya kazi amepata mshahara unaokidhi muda wake wa kazi na mahitaji yake?

Mheshimiwa Spika, tunapo kumbushana haya hatusemi kwamba Tanzania hakuna maendeleo au mabadiliko, lakini je maendeleo hayo ni endelevu kiasi cha kumhakikishia Mtanzania kwamba baada ya "Sera ya Kilimo ni Uhai" ya Mwaka 1976, je tunajitosheleza kwa chakula cha kutosha na hata ukame ukitokea tuna chakula cha akiba? Au bado tunaendelea kuhemea chakula? Kwamba tuliwahi kuwa na hekta 450,000 za umwagiliaji sasa zipo 278,888 tu, hayo ni maendeleo endelevu? Kwamba Mwalimu alituambia " kupanga ni kuchagua" Je , kununua ndege kwapesa taslim Tsh 42 bilion, inayoweza kutua katika viwanja visivyozidi vitano katika nchi nzima na hata kushindwa kutua Dodoma ambayo ni Makao Makuu ya nchi na ya Bunge; ndege inayotumia wastani wa Tsh.6 million kwa saa ya kuruka na kuacha kuwatengenezea barabara wanachi wa Kusini ambao ni wazalishaji wakubwa wa Korosho, Muhogo, Ufuta na raslimali za Misitu na au kuacha kujenga zahanati, shule zenye kuwanufaisha wananchi walio wengi bila ya wao kujitolea, ni matumizi mazuri ya raslimali chache tulizo nazo? Au ndio ule msemo wa kiswahili kwamba "Punda afe lakini mzigo wa bwana ufike". Kwamba huku unataka kumuondolea umasikini, upande wa pili unamuongezea kodi kwa mlango wa nyuma. Kodi ya mafuta ambayo kupanda kwake katika soko la dunia hakutabiriki, ikipanda gharama za uzalishaji nazo zinaongezeka, hivyo mlaji kubeba mzigo wa kodi.Je kwa sera hizi zisizomjali mwananchi, uchumi utakua na umasikini kupungua?

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2007/2008 ni Bajeti ya pili ya Serikali ya Awamu ya Nne. Lengo letu kuu katika Kambi ya Upinzani kupitia utekelezaji wa Bajeti ya mwaka unaokwisha kwa shabaha ya kuonesha mafanikio na mapungufu na kisha kupendekeza njia mwafaka ya kuwa na Bajeti bora itakayoleta nafuu ya maisha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ni zaidi ya urari wa mapato na matumizi ya Serikali. Bajeti ni tamko la kisera lenye lengo mahususi katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi. Kambi ya upinzani Bungeni chini ya uongozi wangu na msaidizi wangu kwa msaada wa Mheshimiwa. Dr.Slaa, Mbunge wa Karatu, inaundwa na vyama vya *CUF, CHADEMA, TLP* na *UDP*. Naomba kutumia fursa hii kuvishukuru vyama vyetu kwa kuanza kujenga maelewano ambayo sio tu kusaidia juhudi za kambi yetu kutoa maoni ya pamoja juu ya hutuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha bali kuisaidia Serikali katika *muona wa pili wa shilingi*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tathmini ya Kambi ya Upinzani kwa ufupi utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007,

na baadaye nieleze misingi na shabaha ambayo kama Serikali ingalizingatia Mapato na Matumizi ya Serikali ya mwaka 2007/2008 yangaliboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Serikali ilipanga kutumia jumla ya Tshs. 4.8 trilioni. Kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Mwenyekiti, sitaki niyarudie haya. Kati ya hizo jumla ya Tshs. 2.83 trilioni zilipangwa kutumika kulipia mishahara na matumizi mengine, Tshs. 287.8 bilioni kwa ajili ya Riba, Madeni na mengineyo (mfuko mkuu) na Tshs. 1.7 trilioni kwa miradi ya maendeleo. Katika fedha hizi za maendelo fedha za ndani zilikuwa ni Tshs. 641.7 bilioni tu ambayo ni sawa na asilimia 37 ya Bajeti yote ya maendeleo na hivyo kuifanya Bajeti ya Serikali kuwa tegemezi kwa asilimia 63%.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa bajeti, mfumo wetu wa bajeti bado hauko wazi kiasi cha Wabunge kushindwa kufuatilia kwa undani vifungu vya mapato na matumizi. Wakati Waziri akiwasilisha mtazamo wa bajeti kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, tatizo hili lilijitokeza.Hatuwezi kufuatilia na kujua fungu linaloitwa *'O/C'* na '*Employment Allowance'* lina vifungu vingapi vidogo vidogo.

Aidha, baadhi ya Wizara kama Elimu, Kilimo na Afya, fedha zao zinatoka katika mikondo zaidi ya minne, hivyo wahasibu, hasa wa Halmashauri wanashindwa kufuatilia kwa undani fedha zinazoingizwa katika Halmashauri zao. Utaratibu huu unasababisha kujirudia *double accounting* kwa mapato na matumizi.

Kambi ya Upinzani inaona haya ni mapungufu makubwa. Hapa kwetu mafungu ya Bajeti yanachukuliwa kwa ujumla jumla tu, hivyo kuwafanya Wabunge kutokufahamu kwa kina matumizi ya mafungu hayo. Hii ni tofauti na nchi nyingine nyingi kama Zambia na Mauritius,Uganda na India kutaja chache tu, zinazofuata mfumo kama wa kwetu wa *CPA* ambapo hata Mshahara wa Rais unaonyeshwa, Ziara za Rais, kwa mwaka zinajulikana. Aidha ziara zote za Mawaziri, Wabunge na Watumishi wote zinaorodheshwa na hivyo kuifanya kazi ya Wabunge ya kuisimamia Serikali kuwa rahisi lakini pia kuondoa mianya yote ya matumizi hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona haya ni mapungufu makubwa yanayohitaji kurekebishwa mara mmoja, kwani, uwezekano wa kuwa na matumizi mabya na au ubadhirifu/uwizi wa mapato ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, bado serikali inakusudia kutumia zaidi katika matumizi ya kwaida (Tshs.3.886 bilioni) kuliko matumizi ya maendeleo Tshs.2,201 bilioni. Hii ni kama tulivyo wahi kusema kuwa ukubwa wa Serikali utasababisha matumizi makubwa ya kawaida. Kambi ya Upinzani inaona kuna kasoro kubwa ya kiuwiano kati ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo, hivyo kuchelewesha ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini. Fedha nyingi zinatumika katika uendeshaji wa Serikali kuliko katika maendeleo na huduma za jamii na hivyo kupnda kwa pato la Taifa kutokuwa na manufaa ya moja kwa moja kwa mwananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali *(CAG)* katika Wizara na Idara tano tulizochambua, tumebaini kuna upungufu wa makusanyo wa mapato yasiyopungua shilingi 73.8 billion, (*Ferry Kivukoni 442.5 million,* Veta,762 Millioni; Tansort,71.billon + 1.3 bilioni 72.3 bilioni. Aidha,misamaha ya Kodi nayo imekuwa ya kutisha, kwani hadi kufikia mwezi huu wa Juni,inakisiwa Tshs.673 billion zitakuwa zimesamehewa kama kodi. Hiki ni kiasi kikubwa kwa nchi inayoomba misaada kila kukicha. Kambi ya upinzani inaona huu ni upungufu mkubwa wa mapato ya wanyonge wa Watanzania kwa kuyatupa bila utaratibu wa wazi na unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaomba kumalizia tathmini yake kwa kuomba tena ufafanuzi kutoka kwa Waziri, baada ya wajumbe wake kukosa maelezo katika Kamati Ya Fedha na Uchumi kuhusu mambo yafuatayo:-

Waziri alieleze Bunge lako Tukufu thamani halisi ya gharama za ujenzi wa majengo ya Benki Kuu ambayo kwa taarifa tuliyo nayo sisi ni kwamba majengo hayo *Twin Towers* yamegharimu si chini ya ya *USD* 340 million kwa kujenga katika eneo la 40,000 sq.m. wastani wa kila Sq.mita moja imegharimu zaidi ya Dola za Marekani 8000 wakati kwa mujibu wa gharama za ujenzi hapa Tanzania haziwezi kuzidi Usd 800. Kwa bei hii kuna zaidi ya Usd.7200. Miji ambayo ujenzi ni ghali kama New York, London, Tokyo gharama ya majengo kama hayo si zaidi ya Dola za Marekani 2,000 kwa kila kitu ikiwa ni pamoja na gharama ya ardhi, na nakishi mbalimbali . Serikali inasema nini juu ya matumizi haya makubwa ambayo yamefanya ujenzi huo ghali mara nne zaidi ya miji hiyo mikubwa duniani? Serikali inalieleza nini Bunge hili kuhusu taarifa zilizoko kuwa hata tenda ilitolewa kwa utaratibu unaotia mashaka? *(Makofi)*

Pili, Bunge lililopita tuliomba Bunge lako Tukufu lipewe maelezo juu ya uwekezaji wa *BOT* katika Mwananchi *Gold Mine,* kwamba je *BOT* iliendelea kuwekeza katika kampuni hiyo binafsi na iliwekeza kiasi gani na mapato yaliopatikana hadi sasa ni kiasi gani.Tunaomba Serikali itupatie maelezo ya kina ambayo tuna tumaini yatakuwa tofauti na ya mwaka jana, yatakuwa si majibu ya kisiasa.

Tatu, katika kikao cha bajeti cha 2006/07 Bunge lilielezwa kuwa ule Mradi ulioasisiwa na Marehemu Baba wa Taifa wa kuwapatia wanajeshi wetu fedha kwa ajili ya kuendeshea mradi wa Nyumbu, *Meremeta Gold Co.* ambayo ilikuwa chini ya uongozi wa *Time Mining* ya South Africa(baada ya kuichukua kutoka kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kudhaminiwa na *BOT* kwa *USD 100* milioni, iko katika hatari ya kufilisika, lakini tukaambiwa kuwa *BOT* ilikuwa ikifanya tathmini.. Kambi ya Upinzani inapenda kupata taarifa ya kina kuhusu tathmini iliofanywa na *BOT* ya mradi huo .

Nne, Mheshimiwa Spika, katika Kamati ya Fedha na Uchumi tuliomba kupewa taarifa juu ya malipo hewa yaliyofanywa na *BOT,* katika Akaunti ya kulipia Madeni ya Nje *(Debt Service Account).* Kambi ya Upinzani ina taarifa kuwa si chini ya Dola za Kimarekani 200 milioni zime haulishwa kwa njia hii, kiasi cha kuifanya hata shilingi yetu itetereke kinyume na taarifa tunazopewa za kupungua kwa mauzo ya nje. Pia tulisoma katika vyombo vya habari kuwa *IMF* na Waziri wa Fedha waliagiza uchunguzi ufanywe,

Serikai inasemaje juu uchunguzi wa taarifa hii? Je Serikali inaeleza nini kuhusu utaratibu huu wa Taarifa kutokutolewa kwa Bunge ambalo ni chombo cha Wananchi na Badala yake uchunguzi unaagizwa na Chombo cha Nje yaani *IMF?* Serikali inaeleza nini kuhusu majukumu ya Bunge hili hasa katika kusimamia rasilimali za nchi hii na jasho la Wananchi? *(Makofi)*

Tano, katika Kamati tuliomba kupewa taarifa juu ya *JFC,* Waziri katika majibu yake kwa kamati ukurasa wa pili alisema "wakati uamuzi kuhusu mapendekezo ya Tume unasubiriwa,bajeti ya 2007/2008 imetenga mgao wa Zanzibar kwa utaratibu wa asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti." Katika hotuba ya Waziri Bungeni ukurasa wa 47, juu ya mgao huo anasema; "Kwa hiyo....... 2007/2008 imetenga..........asilimia 4.5 ya misaada ya nje ya Bajeti" tunaomba atupe tafsiri sahihi ya kauli zake hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tukiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani katika Bajeti ya 2004/2005 tuliulizia juu ya kukiukwa kwa utaratibu wa kumpata mzabuni wa kuchunguza mauzo ya dhahabu unaofanywa na kampuni ya Alex Stuart Asseyers, mwaka huu tulitegemea Serikali ingelisema ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kutokana na taarifa ya Alex Stuwart Asseyers baada ya Serikali kuilipa kampuni hiyo si chini ya *USD 65,000.000* sawa na shilingi bilioni 85 inayotokana na mapato ya mrahaba wa 1.9% kati ya 3% inayopta Serikali kiasi ambacho kingeweza kukopesha wanafunzi 20,000 wa Vyuo Vikuu ambao leo tunawataka walipe asilimia 40% na kutokana na umasikini ulio kithiri hivi sasa vijana wasiopungua mia tatu wanaosomea *UALIMU SAUT* wamerudishwa makwao kwa kukosa asilimia 40% wakati raslimali zao zinatolewa "sadaka." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani na Watanzania kwa ujumla tunaona haya ni mapungufu makubwa katika matumizi ya rasilimali na zaidi pale Serikali inaposhindwa kueleza Bunge lako Tukufu mapato yaliyopatikana kutokana na kazi ya Alex Stuwart Asseyers.

Mheshimiwa Spika, japo kuwa kila mwaka kelele zinapigwa kuhusu misamaha ya kodi, bado hali haijawa nzuri. Zaidi ya shilingi 673 bilioni ya mapato yametolewa kama misamaha. Ni lazima tuandae utaratibu kwa mwaka huu kupunguza angalau asilimia 50% ya misamaha hiyo ili kupunguza Rushwa na bajeti tegemezi, lakini pia kuwa na utaratibu ulio wazi zaidi wa kutoa misamaha ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 59 Serikali inakusudia kuanzisha utaratibu wa kupitisha moja kwa moja *fast tracking* bila ukaguzi bidhaa zote zinazoagizwa utaratibu huu ni mzuri kama upo uadilifu wa kutosha wa walipa kodi na wakusanyaji wa kodi. Serikali ilipoona kuna udhaifu katika utekelezaji Bandarini hivyo wakaamua kukodisha kwa makampuni mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Soika, Kambi ya Upinzani ingetegemea Serikali kuja na tathmini ya utekelezaji wa makampuni hayo ili iwe rahisi kwa Bunge kuamua, juu ya utaratibu unaopendekezawa na Serikali kama usimamiwe na *TRA* au kampuni binafsi, kwani pia yapo mashaka kwamba kushindwa kwa makampuni yaliyoko bandarini

kufanya kazi zao kama inavyotakiwa, itumike njia hii ili wapate wasaa wa kuficha udhaifu wao.

Aidha,utaratibu huu unaweza kuwa njia moja ya kuipunguzia mapato Serikali. Kambi ya Upinzani, pamoja na kwamba inakasirishwa sana na kitendo cha wafanyabishara kunyanyaswa wakati wa kutoa mizigo yao.

Kambi ya Upinzani, pamoja na kwamba inakasirishwa sana na kitendo cha wafanyabishara kunyanyaswa wakati wa kutoa mizigo yao, bado haijashawishika na utaratibu huu hadi hapo Serikali itakapofanya tathmini ya utekelezaji kwa makampuni yanayofanya kazi kwa niaba ya *THA* na *TRA* ili kama ni sifa au lawama ziwe kwa chombo chetu tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haikubaliani kabisa na ongezeko la kodi katika mafuta ya aina yeyote ile, kwani inapingana na dhana nzima ya kukua kwa uchumi na kupunguza umasikini, inaathiri programu nzima ya Mkukuta na uzalishaji, inamkandamiza mwananchi wa kawaida ikizingatiwa hasa kuwa asilimia 90 ya Watanzania wanatumia mafuta ya Taa kwa matumizi yao ya kila siku. Kambi ya Upinzani itatoa mapendekezo yake juu ya njia bora ya kupata Mapato mengine bila ya kupandisha kodi ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi wetu, mfumo mzima wa Bajeti una mapungufu makubwa. Kwanza hauwashirikishi Wabunge katika maandalizi ya kupanga vipaumbele pamoja na kuwa Wabunge wanaishi vijijini, wanakaa karibu kabisa na wananchi na ndiyo wenye kujua vipaumbele katika maeneo yao. Wananchi nao wamewachagua kuwa Wabunge ili wawe sauti yao.

Mfumo wa bajeti wenyewe hauko wazi, hivyo kuwanyima Wabunge na hata Maafisa Wahasibu kujua kwa uwazi mafungu ya matumizi na uingizwaji wa fedha za matumizi.

Aidha, utaratibu wa *Cash Budget* nao hausaidii tena, kwani sasa Serikali inajua kiwango cha mapato ya uhakika kwa mwezi, hivyo Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo yafanyike:-

(i) Kuwe na Kikao Cha Mipango, katika ngazi ya Wilaya, Mkoa kila Mwezi wa Novemba ili kuweka vipaumbele vya kiwiliya na Mikoa na hatimaye kufuatiwa na kikao cha wadau mwanzoni mwa mwezi wa January, kabla ya Kamati ya Mipango ya Bunge Mwezi wa January/Februari;

(ii) Kupunguza idadi ya Wizara zinazohudumia jambo moja, hasa kwa fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri, kwa kukusanya fedha yote inayokwenda kwenye mradi au matumizi kwenye Wizara husika tu (kwa mfano fedha za elimu zinazotoka TAMISEMI, Maendeleo ya Jamii na kadhalika zote ziingie TAMISEMI ziende Haamshauri). Wizara ya Elimu ibakie kusimamia Taaluma na kuwaandaa Walimu tu.

(iii) Kuachana na utaratibu wa *Cash Budget* na kurudisha utaratibu wa *'Warrant of Funds.'* Utaratibu huu utawezesha Wizara/Halmashauri kutumia katika viwango vya bajeti bila ya kungoja fedha. (Afisa Muhasibu atakae tumia zaidi ya kiwango alichoidhinishiwa, adhabu yake ni kufukuzwa kazi bila ya onyo);

(iv) Kupunguza gharama za uendeshaji kwa kupunguza ukubwa wa Serikali, kuratibu vyema safari za viongozi na watumishi, kupunguza magari ya anasa na kwa kuzitumia zaidi ofisi zetu za kibalozi badala ya safari za viongozi na ofisi hizo kuangaliwa upya mfumo wa matumizi yao ili yalingane na shughuli zilizoko katika ubalozi husika;

(v) Kuongeza Mabalozi wa Heshima katika nchi au miji ambayo nchi yetu inaweza ikaimarisha bishara hasa utalii na mauzo ya nje;

(vi) Kupunguza idadi ya makampuni yaliyoko bandarini kwa kuipa jukumu *TRA* na kuiongezea uwezo wa kuitendaji na vifaa vya kisasa. Aidha, *TRA* kuingia ubia na makampuni yenye utaalamu maalum kwa njia ya *"Puplic- Private Partnership"* ili kukusanya kwa uhakika kodi katika maeneo ya Maliasili, Madini, Utaliina kadhalika;

(vii) Kuandaa operesheni maalum kwa ajili ya kupambana na wahalifu wanaotorosha raslimali zetu, kwa kushirikiana na nchi marafiki kama vile China ambayo inanunua magogo na mbao nyingi kuliko zilizoko katika takwimu zetu;

(viii) Kuongeza wigo wa kodi baada ya kuondoa kundi la wafanyakazi wanaosamehewa kodi. Kima cha chini kipande hadi kufikia Sh. 215,000/= na kuongeza viwango vingine kwa asilimia inayolingana na mapato ya Serikali;

(ix) Kupitia upya Mikataba yote ya ajira katika Sekta Binafsi ili kulinda maslahi ya wafanyakazi;

(x) Kuwawezesha Watanzania wajasiriamali ambao wako tayari kuwekeza kwenye viwanda vya vito ili kudhibiti usafirishaji wa mali ghafi ya vito;

(xi) Kutathmini upya utekelezaji wa Sera ya Serikali kuhamia Makao Makuu Dodoma;

(xii) Kuongeza bajeti ya maendeleo kwa kiwango kisichopungua asilimia 45 badala ya 36 ya Serikali mkazo vipaumbele vikiwa Elimu, Afya, Kilimo, Miundombinu na Utawala Bora;

(xiii) Kugawa mapato ya Muungano kwa kutumia asilima 15 ya mapato itakayokwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar badala ya 4.5 inayotokana na Misaada;

(xiv) Kuanzisha Bandari Huru, yaani *'Free Port'* Zanzibar kama njia ya Tanzania kuwa na 'Dubai yake' ili kupanua biashara ya kupitia nchini kwetu *(transit trade);*

(xv) Kuondoa mara moja utaratibu wa *Pre-Shipment Inspection* unaofanywa na Makampuni ya nje na kazi hiyo kuwa chini ya *TBS* yenyewe na hivyo kuwaongezea mapato, kuwaondolea usumbufu waagizaji, kuwapunguzia gharama waagizaji na kuongeza ajira.

(xvi) Kuwarahisishia Watanzania kwa kuifanya mamlaka ya manunuzi nchini ijitegemee kwa kutumia utaratibu wa manunuzi wa mtandao *(e-Procurement)* kwa ajili ya kusajili makampuni katika ngazi za wilaya, Mkoa hadi Taifa na nje zinazotoa huduma kwa Serikali. Kuiboresha mamlaka hii ili isaidie kupunguza rushwa katika manunuzi na kuipunguzia hasara Serikali ya wastani wa si chini ya 15% ya manunuzi yake yote.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano uliopita wa Bajeti tulisema sana juu ya jambo hili la kutegemea wafadhili katika maendeleo yetu. Kambi ya Upinzani inaipongeza *TRA* kwa kukusanya mapato kwa kiwango marudufu kulingana na miaka iliopita. Lakini pia tulisema kuwa uwezo wa Serikali kukusanya mapato ni mkubwa zaidi, ila kuna uzembe mkubwa na kutojali *(laxity),* ubadhirifu na ufisadi kama inavyodhihirishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwaka hadi mwaka.

Madhara ya Bajeti ya namna hii ni kwamba tunapopata matatizo inabidi kupitapita *(realocation)* na kupunguza matumizi kadhaa ili tu kuweka hali sawa ya madhara yaliyotokea. Hii ni hatari kwa Maendeleo kwa Watanzania kwa kiasi kikubwa, kwani hata bajeti ya mwaka huu baadhi ya Wizara zilipunguziwa fedha bila mpangilio. Mathalan, Mwaka wa fedha umepita hakuna hata barabara moja mpya iliyofunguliwa. Kambi ya Upinzani, inaomba kupendekeza njia ambazo itapunguza utegemezi kutoka asilimia 42 ya sasa hadi asilimia 31 kutokana na njia za mapato kama inavyoelezwa hapa chini.

Mheshimiwa Spika, uvuvi katika Bahari Kuu ni moja ya maeneo ambayo kama Serikali ingelikuwa makini na kuchukua maamuzi tunayopendekeza, mapato ya Serikali yangeongezeka marudufu bila kugusa mafuta. Meneo yenyewe ni kama yafuatayo:-

Kwanza, Kuongeza ada ya leseni kwa meli za nje zinazovua katika bahari kuu hadi kufikia *USD 100,000* kutoka, inayotozwa sasa ambayo ni *USD 18,000* kwa mwaka. Somalia ambako kwa muda mrefu hakukuwa na Serikali wanatoza *USD 100,000* kwa leseni. Kulingana na takwimu zilizopo ni kuwa, kuna meli 140 (japo Kumbukumbu za Bunge-Kikao Cha tatu 5$^{th}$Feb,2004 Serikali ilisema kuwa imetoa leseni 193 za Meli za Uvuvi) za nje zilizopatiwa leseni za uvuvi katika bahari kuu ya Tanzania. Kwa maoni haya, mapato yatakuwa Shilingi bilioni 19 ambayo sasa hayakusanywi. Sisi tunasema

ukichukua meli 140 na wakitoza dola 100,000 tayari wanapata Shilingi bilioni 19 za haraka. Hizi meli ziko hapa Tanzania hivi sasa.

Pili, kuongeza tozo la mrahaba wa mauzo la asilimia 10%. Katika bidhaa za Samaki zinazovuliwa katika Bahari Kuu, kila meli kwa mwezi inavua wastani wa tani 2000 za samaki kwa makisio ya chini sana, japo kwa kawaida wanavua Tani 1,500 kwa siku. Bei ya soko kwa kilo ya samaki ni *USD 2.5.* Kwa wanaojua biashara ya sekta hii, kiwango cha uvuvi ni kikubwa zaidi. Kwa maoni haya Mapato yatakuwa Shiligi bilioni 740 ambayo sasa hayakusanywi na Serikali. *(Makofi)*

Tatu, katika kuhakikisha kuwa Sekta hii ya Uvuvi inaleta mabadiliko ya kiuchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla Bandari ya Mtwara, Dar es Salaam na Zanzibar inashauriwa zitenge maeneo ya bandari za samaki *(Fish Ports and Fish Processing plants)* ili meli zote za uvuvi wa bahari kuu zilazimike kununua mahitaji yao yote ya mafuta, maji, chumvi na vyakula wanapokuja kukaguliwa kwa ajili ya kukusanya mapato ambavyo hivi vinaweza kuchangia sio chini ya Shilingi bilioni tatu (3bn.) kwa Serikali. (Vyombo vyetu vya ulinzi,vikishirikiana na *TRA* na Mamlaka ya Uvuvi kudhibiti mapato haya) Kwa uamuzi huu mapato yatakuwa Shilingi bilioni tatu (3bn) ambayo nayo sasa hayakusanywi na Serikali.

Nne, uvuvi katika Lake Victoria na Tanganyika, haujadhibitiwa vizuri. Hivi sasa kuna uvunaji haramu wa wastani wa Tani 36,000 kwa mwaka zinavuliwa kimagendo katika maziwa hayo, matokeo yake viwanda vyetu vinakosa mali ghafi. Tunashauri hatua ya dharura kuikabili hali hii kwa kutumia vyombo vya ulinzi na *TRA* ili kuongeza mapato na ajira. Zoezi hili litaongeza wingi wa samaki, hivyo viwanda vya samaki vitaongeza uzalishaji na kodi itaongezeka. Hatua hii ni ya kuongeza uwezo haitegemewi kwa kuingiza mapato. Serikali imeshindwa kushughulikia hadi leo.

Mheshimiwa Spika, maoni haya Kambi ya Upinzani sio tu yamepanua wigo wa kodi, lakini pia kwa hatua hizo tutakuwa tumedhibiti uvunaji wa raslimali zetu ambapo sasa hazivunwi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, chanzo kingine kikubwa ambacho vile vile mapato yake hayakusanywi sasa na Serikali katika Sekta ya Maliasili hasa ni bidhaa za magogo na mbao.

Kutokana na ripoti za kiutafiti kutoka kwa kundi la wahisani na pia asasi kadhaa zisizo za kiserikali, (Kama *TRAFFIC*) (2005/2006) Serikali ilikusanya asilimia nne tu ya mapato kwa mwaka 2004 yaliyopaswa kukusanywa kutoka katika bidhaa za magogo na mbao. Wanunuzi wakubwa ni China, India na Japan. Katika utafiti huo, katika kipindi cha mwaka 2001/2005 China peke yake ilinunua Cubic metre 18,316 x $150 kwa rekodi za Maliasili Tanzania kwa bei ya wastani wa *USD2.7m.* sawa na Tshs. 3.5bl. na Cubic metre 108,605 kwa rekodi za Forodha za China. Kwa maana hiyo ama kwa ufisadi au vyenginevyo Serikali imekosa mapato ya Cubic metre 90,289 x $450 = $40.6m. sawa na Shilingi bilioni *52.8.* Utafiti huu ulihusu magogo na mbao zinazotoka Mikoa ya Kusini

tu. Taarifa hii inathibitisha Taifa lilikoseshwa fedha kwa kuuza kwa Dola 150 tu wakati bei halisi China ilikuwa Dola 450. Pia kiwango kilichouzwa kimefichwa. Huu ni Ufisadi.

Mheshimiwa Spika,Kambi ya Upinzani inashauri hatua zifuatazo zichukuliwe:-

Halmashauri za Wilaya zilizoko katika maeneo ambayo bidhaa hizi zinapatikana ziwe mawakala wa kukusanya mapato kutokana na bidhaa za maliasili. Uamuzi huu utapunguza kwa kiasi kikubwa ufisadi uliopo sasa katika Wizara ya Maliasili. Kila Halmashauri inayokusanya kodi ipatiwe gawio kutoka sehemu ya makusanyo, Mapato yote yakusanywe na *TRA* kwa kutumia stakabadhi za *TRA* kupitia Halmashauri za Wilaya kama ilivyoelezwa hapo juu.

Mtu yeyote atakayekamatwa kwa kutorosha maliasili afilisiwe kwa mujibu wa sheria, kama haipo itungwe;

*TRA* mbali na kukusanya mapato ishirikiane na Bodi ya Mauzo ya Nje kuhakiki bei za Bidhaa zetu zinazouzwa nje ili kupata mapato halali ya Rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na utalii, bahati nzuri Mheshimiwa Zitto Kabwe ameyasema kwenye ile *package* ya watalii, lakini kwa *estimate* zetu tunaweza kukusanya Shilingi bilioni 67.5 kama Serikali itakuwa *serious* kuisimamia sehemu hiyo. Kwa hatua hizi, mapato ya maliasili misitu itaongezeka kwa asilimia 90 ya mapato ya sasa, makusanyo halisi yatakuwa Shilinig bilioni 100 ambazo hazikusanywi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona kuwa inakusanya mapato kwa wingi hadi kufikia asilimia 16.8% ya pato la Taifa katika Sekta hii ya Utalii. Hata hivyo, Serikali imeshindwa kufikia malengo ya watalii milioni moja kwa mwaka kama ilivyokuwa imepanga. Idadi ya watalii wanaokuja nchini ni wastani wa laki sita (644,124). Isitoshe, Serikali imekuwa ikipoteza mapato kutokana na watalii kulipia gharama za safari zao na baadhi ya huduma kwa *Tour Operater* huko huko kwao kwa wastani wa *USD 200-300* kwa mtu mmoja kwa siku. Mtalii anapofika Tanzania, huwa analipa wastani wa *USD 80-150* tu. Hivyo, kuzipunguzia mapato hoteli zetu na kwa maana hiyo na Serikali. Kama nusu ya watalii hawa (322,062), kuwa wanakuja katika "*Packege Tour*" na kuwa tunakusanya wastani wa *USD 100* kwa siku kwa kila mmoja kwa muda wa siku saba, ukiacha mapato yasiyo ya moja kwa moja. Katika eneo hili Serikali ingelikusanya kama kodi ya mapato asilimia 30 sawa na Shilingi bilioni 67.5 ambazo hazikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Maliasili, kuna vitalu 152. Kwa wakati huu Serikali inakodisha kwa wastani wa *USD 7500* kwa mwaka (mara nyingi wamiliki nao hukodisha kwa wenye fedha kwa wastani wa *USD100,000* kwa mwaka). Ili kuongeza mapato ya Serikali, Kambi ya Upinzani inashauri hatua zifuatazo zichukuliwe ili kuongeza mapato kama ifuatavyo:-

Kuwajasirimisha Watanzania vitalu vyote vya uwindaji ambavyo vingi tumewapa wageni;

Ili kupata thamani halisi, washauriwe kuingiza Vitalu hivyo katika soko la mitaji kwa kutumia *"eletronic commerce."*

Kupandisha viwango vya kodi ya Uwindaji;

Kutoza asilimia 30% ya mapato yatokanayo na Mtanzania atakayekodisha kwa mtu mwingine.

Kwa hatua hii, Watanzania watakuwa wamewezeshwa kumiliki rasilimali zao wenyewe na pia kwa kuongeza viwango vya kodi ya uwindaji makusanyo yanakisiwa kuwa Shilingi bilioni 85 ambayo hayakusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Madini, kwa kulingana na ukaguzi uliofanywa na Kampuni ya Alex Stuart, kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali imepoteza shillingi trillion 1.3. Hii imetokana na Serikali kutokuwa makini katika kufuatilia nyaraka halali zinazotumiwa na makampuni ya kuchimba madini. Ili kuifanya sekta hii ya madini kuwa na manufaa kwa Taifa na Watanzania wote, hatua zifuatazo zikichukuliwa sekta hii itachangia zaidi:-

(i) Kufanya mapitio ya sheria ya madini na kupandisha asilimia ya mrahaba toka 3% hadi 5% kwa kuanzia;

(ii) *TRA* kuimarishwa kiutendaji na kukusanya kodi zote katika sekta ya madini;

(iii) Katika mpango wa maendeleo wa kampuni husika, maendeleo ya jamii zinazozunguka migodi yaonekane wazi wazi na kuingizwa katika mpango wa mwekezaji;

(iv) Kati ya 5% za mrahaba utakaotozwa 2% iabaki katika Halmashauri ya Wilaya/Mji ambamo mgodi upo;

(v) Katika masharti ya kuwekeza kwa wageni,ni lazima waingie ubia na Mtanzania au Halmshauri angalau kwa asilimia 10 ikiwa ni pamoja na thamani ya ardhi;

(vi) Kuweka sharti ndani ya Mikataba na kubadilisha sheria kwamba atakayekiuka mkataba au kusafirisha mali itokanayo na raslimali za nchi kampuni husika itafilisiwa;

(vii) Kuhakiki madeni waliyokopa wawekezaji ili kupata kiasi halisi walichokopa, ikiwa ni pamoja *na Tax Holiday* kwa lengo la kufuatilia muda wa Kusamehewa Kodi.

Mheshimiwa Spika, mambo yote haya yapo katika sura ya 25 kwenye kitabu changu na ninaomba taarifa yote hii iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na tukichukua wastani wa mapato tunayopoteza kwa mwaka katika sekta hii, Serikali ingelikusanya jumla ya shillingi bilioni 433 kwa kuziba tu mianya ya kukwepa kodi. Vile vile kutokana na uamuzi wa kupandisha mrahaba, Serikali ingekusanya jumla ya shilingi bilioni 41.8 kutokana na mauzo ya madini, hasa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali za kitafiti zinaonesha kuwa Tanzania inapoteza mapato mengi sana katika madini ya vito kwa sababu ya uzembe na ufisadi. Kwa mfano, katika Soko la Dunia mauzo ya Tanzanite mwaka 2005 yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 400. Hata hivyo, rekodi ya Tanzania ni Dola milioni 16 tu. Tuna taarifa kuwa Kenya ilipata tuzo kwa kusafirisha Tanzanite nyingi duniani wakati hawana Tanzanite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama eneo hili likisimamiwa vizuri tunaweza tukakusanya Shilingi bilioni 100 ambazo Serikali sasa hivi haikusanyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ingekubaliana na ushari wa Kambi ya Upinzani, Serikali ingepitia upya kabisa mwenendo mzima wa biashara ya madini haya ili kuwa na chanzo kimoja tu cha mauzo. Udhibiti huu ungepatia Serikali mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 100 ambayo haikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tumekuwa tukipoteza fedha nyingi sana ni eneo la misamaha ya kodi. Kama ilivyo katika taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, inakadiriwa kuwa takribani Shilingi bilioni 673 zilitolewa kama misamaha ya kodi katika mwaka wa fedha unaomalizika. Ili kuongeza mapato yetu ya ndani, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali ipunguze misamaha ya kodi kwa asilimia 50. Uamuzi huu mapato yatakuwa Shilingi bilioni 336.5 ambazo hazikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya kodi ya mapato, sheria na.11 ya mwaka 2004 kifungu cha 7(1) na (2), kila atakachokitoa mwajiri itabidi kikatwe kodi isipokuwa kama mfanyakazi atatumia fedha zake na mwajiri akamrudishia. Kwa mujibu wa sheria hii, posho zote za warsha, semina, makongamano, mikutano na vikao zinapaswa kukatwa kodi ya mapato. Hii pia inajumuisha posho wanazopata Waheshimiwa Wabunge kutokana na vikao hapa Dodoma na Dar es Salaam. Ikirekebishwa sheria ya kodi ili kutoza kodi mapato haya kwa kiwango cha *VAT* yaani asilimia 20. Hatua hizi pia ingelenga kupata manufaa yafuatayo:-

(a) Mifuko ya Pensheni itapata wanachama zaidi;

(b) Kodi ya Serikali ambayo ni ya uhakika *(Pay As You Earn,* itapanda maradufu kwani *employment allowance* haitozwi); na

(c) Wafanyakazi watakuwa na kipato kitakachowapa moyo wa kufanya kazi hivyo kuongeza ufanisi kazini.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu Serikali ingepata mapato ya Shilingi bilioni nane (8bn) ambazo hazikusanywi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mauzo ya hisa za *NMB* imeelezwa hata kwenye Kamati ya Fedha kwamba *NMB* kwa tathmini iliyofanywa ilikuwa tupata Shilingi bilioni 15, lakini baada ya kufanyiwa tathmini ya pili tumeonekana inaweza kupatikana Shilingi bilioni 45 kwa maana hiyo Serikali itapata mapato ya Shilingi bilioni 30 zaidi mbali ya 15 iliyoweka Serikali. Eneo lingine linalonyima Serikali mapato yake ni uuzwaji wa hisa zake kwa bei isiyokuwa ya soko. Kwa mfano hisa ya asilimia 25 za Serikali za Wiilliamson Daimond ziliuzwa kwa *USD 183,000* tu.

*NIC* ilitaka kubinafsishwa kwa thamani ya Shilingi bilioni tatu (3bn) tu,hadi Kamati ya Fedha na Uchumi ilipodai tathmini mpya, kulingana na tathmini mpya iliyofanywa na Chuo Kikuu kishiriki cha Ardhi. Thamani imepanda hadi Shilingi bilioni sita (6bn). Hisa za *NMB* zinatarajiwa kuuzwa kwa Shilingi bilioni 15. Kiwango hiki ni cha chini kulingana na bei ya soko. *NMB* ni benki inayopata faida sana na imeweza kutoa gawio kwa wanahisa. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuuza hisa za *NMB* kwa bei ya soko. Kwa ushauri huu Mapato yatakuwa Shilingi bilioni 45 badala ya Shilingi bilioni 15 ongezeko la Shilingi billioni 30.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo bado halijatumiwa vizuri na la kuuza mauzo nje ya nchi na hasa nchi jirani *(Bonded Goods)*. Kama bandari ya Mtwara ingejengewa maghala ya kuhifadhia mazao na bidhaa kwa kufanya mauzo ya bidhaa zetu za viwandani kama vile *cement* na mifugo, mchele na bidhaa nyingine katika nchi ya Comoro, ambayo matumizi yao kwa mwaka, *cement* kwa mwaka 70,000, Mchele 40,000, ngombe ni 4000 kwa wiki, ambayo inaitegemea sana Tanzania katika vyakula na vifaa vya ujenzi. Aidha, tutasukuma uuzaji wa bidhaa zetu nje kama muhogo,korosho,ufuta na samaki. Uimarishaji huu utaweza kutuingizia kiasi cha shilingi billioni mbili (2bn) kutokana na kodi peke yake ambayo sasa haikusanywi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Serikali ilifuta kodi ya *VAT* katika mafuta ya petrol. Uamuzi huu haukuleta matarajio ya unafuu kwa mwananchi wa kawaida. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa irudishwe *VAT* katika eneo hili na hivyo kupata mapato ya Shilingi bilioni 153 bila athari kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa mfumo wa leseni za madereva uboreshwe kwa kutoa leseni mpya kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya komputa. Leseni hizi zitakuwa na uwezo wa kuhifadhi taarifa zote muhimu za madereva. Hii itasaidia kupunguza uhalifu na hasa ajali za barabarani na pia itakuwa ni sehemu ya kitambulisho. Mradi huu uendeshwe kwa utaratibu wa *PPP*. Kwa makisio ya chini, madereva laki mbili na nusu mwaka huu wa fedha na ada ya leseni kuwa Sh.50,000/=, tutakusanya jumla ya shilingi bilioni 12.5 ambazo sasa hazikusanywi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na dhamira yetu toka mwaka 2003 kwamba ununuzi wa ndege ya Rais ni anasa na gharama zisizo na msingi kwa sasa Serikali inatumia Shilingi milioni sita (6ml) kwa saa ya kuruka ndege hii. Kambi ya Upinzani

bado inaendelea na ushauri wake kwamba ndege hii kama alivyofanya Rais wa Ghana Bw. John Kufouri iuzwe kwa mnada. Kwa uamuzi huu, Serikali itapata mapato Shilingi bilioni 35. *(Makofi)*

Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge, ndege hii inachukua watu tisa tu na Rais anasafiri na watu 17. Kwa hiyo, hata wengine hawaingii ndani ya ndege hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushari huu uliotolewa na Kambi ya Upinzani, kama Serikali ingekubali kuufanyia kazi kuhusu sera ya mapato, yangeipatia Serikali jumla ya mapato ya ziada ya Shilingi bilioni 2,181.3. Ushauri wa Mapato haya yote ni kutokana na kuboresha vianzio vilivyopo na kubuni vipya ambayo Serikali haikuviona.

Mheshimiwa Spika, muhtasari wa ushauri wetu juu ya mapato ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mapato kutokanana ada za leseni za meli zinazovua bahari kuu shilingi bilioni 19; mapato kutokana na Mrahaba kutokana na Uvuvi katika Bahari kuu shilingi bilioni 740; mapato kutokana na mafuta kwa meli za uvuvi shilingi bilioni tatu (3bn); mapato kutokana na bidhaa za misitu shilingi bilioni 100; mapato kutokana na biashara na Comoro kupitia Bandari ya Mtwara shilingi bilioni mbili (2bn); na mapato kutokana na punguzo la asilimia 50 ya misamaha ya kodi shilingi bilioni 336.5.

Mapato mengine ni kutokana na kodi ya asilimia 20 kutokana na posho za semina na kadhalika shilingi bilioni nane (8bn); mapato kutokana na mauzo ya hisa za Serikali i.e *NMB* shilingi bilioni 45; mapato kutokana na ukusanyaji wa kodi isiyokusanywa kwenye madini shilingi bilioni 433; mapato kutokana na ushuru wa mauzo kutokana na madini ya Vito i.e. Tanzanite shilingi bilioni 100; mapato kutokana na vitalu vya uwindaji wa Kitalii shilingi bilioni 85; mapato kutokana na mrahaba wa 5% katika madini shilingi bilioni 41.8; mapato kutokana na *VAT* katika mafuta ya petrol na disel shilingi bilioni 153; mapato kutokana na mauzo ya Ndege ya Rais shilingi bilioni 35; mapato kutokana na leseni za madereva shilingi bilioni 12.5; mapato kutokana na utalii shilingi bilioni 67.5. Jumla ni Shilingi bilioni 2,181.3.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Zakia Meghji mnamo tarehe 14 Juni 2007, Serikali inapendekeza kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi na tozo nyingine za kodi chini ya sheria mbalimbali ambazo zingeiingizia jumla ya shilingi billioni 239.161. Kutokana na ushauri wetu, tunapendekeza kodi na ushuru uliotumika mwaka 2006/2007 usibadilike isipokuwa kodi ya ongezeko la thamani katika bidhaa za mafuta ya Petroli.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wetu wa mapendekezo yetu ya mapato tungeweza kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 5.3 kama mapato ya ndani. Makusanyo haya yangekuwa ni ziada ya makusanyo ambayo Serikali imepanga kuyakusanya kwa

kiasi cha Shilingi trilioni 1.8 tofauti ya zaidi ya Trilioni tano (5tr) na bila kumuumiza mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia kuwa nchi yetu itapata misaada na mikopo kutoka nje kama jinsi ambavyo imeainishwa katika Makadirio ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008, Makadirio ya Mapato ya Bajeti hii yangefikia jumla ya Shilingi trilioni 7.99.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani katika Matumizi. Katika kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata matunda ya kile kinachokusanywa, Serikali ingeweka mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa mapato ya ndani, Kambi ya Upinzani inashauri kiwango cha chini cha mshahara wa wafanyakazi wa umma kiwe Sh. 215,000/= kwa mwezi. Kwa kufanya hivyo, utaondoa wafanyakazi ambao hawatozwi kodi. Kwa maana hiyo, utakuwa umepanua uwanja wa kodi na wafanyakazi wote watakuwa wanalipa kodi na kwa maana hiyo, wigo wa kodi utakuwa umepanuka na kwa sababu mapato tumesema yanatoka wapi, kwa hiyo hakuna tatizo la kupata fedha. Kwa ngazi nyingine mshahara ungepanda kwa asilimia ambayo italeta uwiano baina ya kipato cha chini na cha juu. Ufafanuzi wa kina utatolewa na Waziri Kivuli wa Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, elimu ni kipaumbele chetu kikuu katika matumizi ya Serikali. Hata hivyo sekta ya elimu inapaswa kutengewa fedha zaidi ili kuboresha elimu. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani ni kuwa, Serikali imejikita zaidi katika hatua ya awali kuwa na shule nyingi, idadi kubwa ya wanafunzi, jambo ambalo limefanikiwa vizuri sana. Hongereni.

Kutokana na kazi kubwa iliofanywa na Kambi ya Upinzani ya kutafuta mapato zaidi, mwono wetu ni kuimarisha hatua iliofikiwa kwa kuelekeza matumizi yetu katika kuboresha viwango vya elimu ili kuwa na elimu bora. Hivyo, tunashaurikuwa tuhakikishe mkazo mkubwa unawekwa katika kuwaelimisha walimu, katika ule mtindo wa zamani. Kwa kuwa hivi sasa tuna upungufu mkubwa wa Walimu kufuatia ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata, Serikali yetu ingeajiri walimu kwa muda kutoka nchi jirani za Kenya, Uganda, Malawi, Zimbabwe Zambia na India.

Utaratibu huu ungedumu kwa miaka miwili ambapo tutakuwa tayari tumehitimisha walimu wapya, tumetafuta vifaa vya kufundishia pamoja na vitabu na nyumba za walimu kuwa katika hadhi inayokubalika ili kurejesha heshima ya mwalimu katika jamii.

Tusingejali chochote katika kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu bora. Uamuzi huu usingekuwa na tatizo lolote kwani Watanzania wengi sana walikwenda kufundisha katika shule za nchi hizi wakati wao wakiwa na shida. Mfano, kumbukumbu zinaonyesha kuwa Mheshimiwa Bujiku Sakila alikuwa Mwalimu huko Msumbiji baada ya uhuru wa nchi hiyo mwaka 1975.

Mhehismiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, mtazamo wetu ungekuwa katika kuweka shule kuwa rafiki wa mwanafunzi kwa kuboresha majengo. Katika ujenzi wa nyumba za walimu tungetumia teknolojia wa *"Pre-fabricated houses"* ambayo ni rahisi na haraka. Katika kuendeleza Teknolojia hii na pia ujenzi huu wa nyumba za Walimu, viwanja vya michezo, mabweni na Maabara. Majeshi yetu ya Magereza na JKT kupitia mashirika yao ya ujenzi, yaingie ubia na makampuni ya nje kwa utaratibu wa *PPP* ikiwa pia ni hatua ya kupata utaalamu ambao utapunguza kwa kiwango kikubwa ujenzi wa nyumba zao pia.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kambi ya Upinzani, Serikali ingetenga asilimia 20 ya bajeti yote katika Elimu kama ilivyo katika bajeti hii ingeweza kwa kiwango kikubwa kuwa na Elimu Bora. Maelezo zaidi katika matumizi yetu katika Elimu ya Msingi na Sekondari yatafafanuliwa na Waziri Kivuli wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wanapata elimu ya juu na iliyo bora, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, wale wote watakaopata udahili katika vyuo vyetu vya elimu ya juu wapate mkopo kwa asilimia mia moja (100%).

Katika kuhakikisha kuwa mikopo itakayotolewa inakuwa ni kwa Watanzania tu*,* vyombo vya fedha ndivyo vihusike na utoaji wa mikopo na Bodi ibaki na kazi ya kutoa miongozo na taratibu tu. Wanafunzi wote watakiwe kufungua *Bank Account* na *TIN* kwa udhibiti na uhakika wa marejesho pia kuongeza wigo wa walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani,inashauri kuwa ili kuongeza ushindani wa kupata ubora wa wahitimu, uwekwe utaratibu ambao ungegeuza sehemu ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kuwa misaada i.e *grants* kulingana na viwango vya kufaulu katika mitihani ya mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ushauri juu ya utaratibu gani utatumika katika kuteua asasi za kifedha zitakazotumika kutoa mikopo na vile vile jinsi ya kugeuza mkopo kuwa *grant* utatolewa na Waziri Kivuli wa Elimu ya Juu.

Leo tumesikia Tabora vijana wamechukua matofali kwenda kujenga zahanati, trekta lilipinduka wamevunjika miguu, tunasema si utaratibu mzuri wa kufanya shughuli hizo. Kwa kutumia utaratibu wa *pre-fabricated* inawezekana kabisa kazi hiyo ikafanyika kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Katika suala la miundombinu tunashauri kwamba pamoja na uchache wa fedha zinazopatikana Serikalini lakini Serikalini mpaka leo hakujakuwa bayana katika suala zima la ku–*identify* miradi ambayo itajengwa kwa *BOT* na ile ambayo itajengwa kwa *PPP*.

Tunaishauri Serikali ianishe maeneo hayo kwa sababu wawekezaji katika maeneo haya wapo lakini mpaka leo Serikali haijatoa majibu. Tumekosa Shilingi bilioni 2.5 kutoka Kampuni moja kutoka Australia kwa sababu tu Serikali haijatoa majibu na

tunakuja hapa tunasema miundombinu ina matatizo. Ina matatizo kwa sababu hakuna maamuzi Serikalini! Kambi ya Upinzani inafikiri hiyo itasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wetu katika kilimo, unalenga kuboresha kilimo na hivyo kuhakikisha kinakua kwa asilimia nane kwa mwaka. Tunashauri yafuatayo:-

(i) Tuhakikishe kuwa wakulima wetu wanalima kwa ajili ya soko, hivyo ubora na wingi wa bidhaa iwe ni agenda muhimu kwa upande wetu. Ili kupata bei nzuri katika soko tuweke mazingira bora kuhakikisha mazao yataongezwa thamani kabla ya kuuzwa *(add value through processing);*

(ii) Pamoja na mazao mengine, tujitahidi kuhimiza kilimo cha mazao ambayo yatatupatia nishati mbadala kwa lengo la matumizi ya nishati hiyo katika kukifanya kilimo kuwa cha kisasa kwa gharama nafuu;

(iii) Tuimarishe *rural infrastructure* ambayo itasimamiwa na *rural road agency* na barabara hizi ziwe zinapitika mwaka mzima;

(iv) Vyuo vyote vilivyokuwa vinatoa mafunzo na elimu ya kilimo kuanzia ngazi ya chini vitafufuliwa. Jambo hili litaongeza wataalam wengi wa Ugani ambao watakuwa na taaluma kulingana na zao husika na eneo husika;

(v) Kutafuta teknologia *(Hygrex)* inayoweza kukausha na kuhifadhi mazao hasa matunda kwa ajili ya soko la nje hasa Marekani ya Kaskazini na Arabuni;

(vi) Kuainisha na kuwanisha *(integrate)* viwanda vinavyotumia malighafi za kilimo ili kuongeza thamani ya mazao yetu nje na kuongeza bei kwa mkulima;

(vii) Kuhakikisha kuwa wakulima na wafanyabiashara wanapata taarifa sahihi za bei za bidhaa katika masoko ya ndani na ya nje ya nchi kwa kutumia vyombo vyote vya habari nchini kwa muda maalum**;**

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imepanga asilimia 12 ya Bajeti yote kwa ajili ya kilimo badala ya asilimia 6.2 iliyotengwa na Serikali katika Kilimo. Maelezo juu ya ushauri wa matumizi wa miradi ya maendeleo atayatoa Waziri kivuli wa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vyanzo vipya vya mapato vilivyobuniwa na Kambi ya Upinzani, ili kuhakikisha kuwa tunajenga jamii yenye afya, itakuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wa elimu ya msingi na Sekondari wanapimwa afya zao bure *(preventive health care)* , jambo ambalo litasababisha kuwapa hamasa wazazi wao ili na wao kuwa na utaratibu wa kupima afya zao. Serikali ihakikishe madawa ya kutosha yanakuwepo kuanzia katika ngazi ya Zahanati mpaka kwenye Hospitali.

Kwa kutumia utaratibu ule ule wa kutumia *pre-fabricated technology*, zahanati zitajengwa sambamba na matayarisho ya wataalam ili kuepuka raia kupoteza maisha kwa

ukosefu wa mtaalamu. (Ukikosa mwalimu mtoto atajua kucheza na wenzake,ukikosa mtaalamu wa utibabu utapoteza maisha). Utaratibu huu unalenga uwiano mzuri wa huduma, mipango sahihi na siyo maamuzi ya kisasa ambayo siyo endelevu.

Mheshimiwa Spika, tumetenga 9% ya bajeti hii kwa ajili ya sekta ya afya. Maelezo zaidi juu ya matumizi ya kiasi hiki kilichotengwa atayatoa Waziri Kivuli anayehusika na sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, baada ya mchakato wa kupata njia za kupata mapato mapya ya ndani, inashauri kuwa asilimia 21 ya mapato ipewe sekta hii na lengo kuu liwe ni kutengeneza barabara kuu za kuifungua Tanzania kiuchumi. Aidha, tunashauri kuwa katika utaratibu wetu wa ujenzi umuhimu uwekwe katika ujenzi wa barabara kwanza na sio kwa madaraja kama inavyofanyika sasa, barabara za kipaumbele ziwe kama zifuatazo: Masasi - Tunduru - Songea, Tunduma - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma, Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma, Iringa– Dodoma – Babati, Mbeya – Sikonge –Tabora- Nzega, Babati –Singida, Oldeani-Matala - Lalago.

Mheshimiwa Spika, kwa kutengeneza barabara hizi tutakuwa tumeifungua milango ya biashara kwa Tanzania nzima, hivyo basi bandari za Mtwara na Kigoma zitakuwa ndio injini za mapato kwa nchi hii kutokana na uzalishaji kwa mikoa inayozunguka mikoa hiyo ya Mtwara na Kigoma. Ili kuhakikisha kuwa miradi ya miundombinu haikwami na kama kweli Serikali inataka mabadiliko ya haraka ibainishe miradi inayotaka kuendeshwa kwa *BOT* na *PPP* ili kurahisisha uwekezaji katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wengi wamekuja kwa njia ya *BOT* na *PPP* lakini hadi leo hakuna maamuzi.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta hii tumetenga 8% ya bajeti yetu kivuli. Tunaishauri Serikali ihakikishe kuwa uzalishaji wa umeme wa maji toka *Stigglers Gorge* unazalishwa ili kuondokana na kutegemea umeme wa bwawa la Mtera ambalo uwezo wake unapungua kutokana na sehemu kubwa ya bwawa kujaa tope.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inalenga kushauri kupata nishati mbadala inayotokana na uzalishaji wa kilimo *(Bio-energy)*. Katika mchakato huo wa uzalishaji nishati bidhaa kadhaa zitapatikana bila kusahau mbolea *(organic fertilizers).* Jambo litakaloinua kilimo hai kwa Watanzania, inashauriwa kila Mkoa uwe na mradi wake wa kuzalisha umeme wa kutumia *Bio-energy* na *Tanesco* iwe na jukumu la uratibu na usambazaji tu. Ushauri huu utasaidia sana kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia umeme ikiwa pia ni hatua ya kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona umuhimu wa kufufua utaratibu wa kusafisha mafuta *(Refinery)* ili kupata lami ambayo itatumika kujengea barabara na bidhaa zinazotokana na mafuta. Wapo wawekezaji wengi walikuja kuomba mradi huu, lakini bado anatafutwa *"stretegic invester"*.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee, tunaishauri Serikali iifanye Mikoa yote ya Pwani bila ya kuisahau Mafia kuwa wazalishaji wakuu wa *"Biofuel"* kutokana na kuwa ni wazalishaji wakuu wa zao la nazi. Kwa umuhimu huo, kuna haja ya kuhakikisha uchumi binafsi kwa wananchi wa Mikoa ya Pwani unakua kwa vile itakuwa ni sehemu nzuri kwa kilimo cha Mibono *(Jatropha)* ambacho soko lake liko juu sana (*USD 350* kwa tani).

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani juu ya utaratibu wa mgao wa kutumia fedha. Kama tulivyoshauri katika hatua mbalimbali za maoni yetu, katika kutekeleza mipango yake Serikali na kuwafanya watekelezaji wa mipango hiyo waweze kutekeleza vyema, utaratibu wa *"cash budget"* haufai. Utaratibu uliokuwa unatumika zamani wa *"Warrant system"* urudiwe. Aidha, Fedha badala ya kutolewa kwa mtindo wa kila mwezi, utaratibu wa kutoa fedha kwa kipindi cha miezi minne minne utumike.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vipaumbele tulivyoshauri, tumegawa mapato kama ya bajeti hii kivuli kama ifuatavyo:-

Miundombinu, 21% sawa na shilingi bilioni 1, 678.734; Elimu, 20% sawa na shilingi bilioni 1,598.794; Kilimo,12% sawa na shilingi bilioni 959.277; Afya, 9% sawa na shilingi bilioni 719.457; Nishati 8% sawa na shilingi bilioni 639.518 na Maji, 7% sawa na shilingi bilioni 559.578.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani juu ya Sura ya Bajeti ni kama ifuatavyo:-

| | **Mapato:** | **TSh.** |
|---|---|---|
| A. | Mapato ya Ndani | 5,399.722bn |
| B. | Mikopo na misaada ya nje ikijumuisha *HIPC/MDRI* | 2,549.249bn |
| C. | Mauzo ya Hisa za Serikali | 45.000bn |

Jumla ya mapato yote ni Shilingi bilioni 7,993.971.

**Matumizi**

| **Matumizi ya Kawaida** | **3,940.213 bn** |
|---|---|
| 1) Mfuko Mkuu / CFS | 615.039 bn |
| 2) Wizara | 2,410.751bn |
| 3) Mikoa | 86.704 bn |
| 4) Halmashauri | 827.719 bn |

| | | |
|---|---|---|
| **Matumizi ya Maendeleo** | | **4,053.758bn** |
| (i) | Fedha za Ndani | 2,591.866bn |
| (ii) | Fedha za Nje | 1,461.892bn |
| Jumla ya Matumizi yote | | 7,993.971bn |

Mheshimiwa Spika, kutokana na mchanganuo huo, tofauti za kimsingi za hoja ya Waziri wa Fedha na Ushauri wa Kambi ya Upinzani ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii kivuli utaiwezesha Serikali kutumia fedha za ndani asilimia 48 kwa ajili ya maendeleo, badala ya asilimia 21 tu iliyowasilishwa na Serikali.

Pili, ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii kivuli utaiwezesha Serikali kutumia kiasi kisichopungua asilimia 45 ya bajeti yote kwa ajili ya maendeleo, badala ya asilimia 36 tu iliyowasilishwa na Serikali.

Tatu, ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii kivuli utaiwezesha Serikali kupunguza Bajeti tegemezi. Mikopo na misaada toka kwa wahisani ni asilimia 31.8 ya bajeti nzima kivuli badala ya utegemezi wa asilimia 42 uliowasilishwa katika bajeti ya Serikali. Kwa ujumla bajeti yetu imepunguza utegemezi kwa kulinganisha na bajeti ya Serikali kwa asilimia 10.2.

Mheshimiwa Spika, mlinganisho wa kati ya ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti yake kivuli na Sura ya Bajeti ya Serikali ni kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lengo kuu la ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti hii kivuli niliyowasilisha ni kuchochea ukuaji wa uchumi, kuondokana na bajeti tegemezi kama Taifa na kuwa na Taifa lililoelimika lenye utawala unaoheshimika. Katika hotuba yetu nimeonyesha wazi wazi kuwa tunazo fursa kubwa za kupata mapato ya ndani. Tatizo ni *"mind set"*. Changamoto kubwa tuliyonayo kama Taifa ni kwa viongozi kuwa tayari kujifunza kutoka kwa wengine bila kujali itikadi za kisiasaili kwa pamoja tuwaondolee umasikini Watanzania waliokalia raslimali zinazozidi mahitaji yao. Lazima sote tujiulize kwa nini wageni na wajanja wanatajirika,lakini wakulima na wafanyakazi wetu ni masikini? Taifa hili ni letu. Tusemezane, tujadiliane hatimaye tusonge mbele. *(Makofi)*

Tuliyosema yanawezekana, yanahitaji viongozi na watumishi kuweka maslahi ya Taifa mbele. Raslimali tulizonazo zinatosheleza kama zitasimamiwa na kutumika kwa maslahi ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba mambo mawili ya ziada, kwanza hotuba yote hii iingie kwenye *Hansard* lakini pili nichukue fursa hii kuwapongeza sana timu yetu ya mpira iliyofanya vizuri, imeitia Tanzania katika ramani mpya ya michezo na tunaamini sasa soka itatumika kuendeleza ajira, kuongeza kipato cha Tanzania.

Pili naomba nitoe rambirambi na pole kwa ndugu zetu waliopata ajali Singida na tunaomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote Peponi, Amin! Tunaiomba Serikali sasa kwa kweli iongeze fedha katika maeneo ambayo yanaweza kuokoa maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kukushukuru na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa kunisikiliza. Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kwa bahati mbaya kwa mara ya kwanza tutakuwa hatuungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani kwa hotuba yako.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi kwa mujibu wa shughuli zetu ningeanza kuwaita wachangiaji ambao ni 68 hivi sasa, lakini mtakumbuka pale asubuhi tulikwishaamua kutengua Kanuni zinazohusika ili kuahirisha mjadala huu kutuwezesha sisi Wabunge kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania kuwapokea *Coach* Maximo na Timu nzima ya *Taifa Stars* iliyotuwakilisha vizuri sana huko Oagadougou. Kwa kitendo hiki wajue vijana kwamba nchi inawathamini sana na tutawaunga mkono mpaka mwisho kule Ghana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa namwita *Serjeant-At-Arms* awashushe wageni hao mashuhuri na mashujaa wetu waingie ndani ya Bunge ili taratibu ziendelee za kuwaenzi. *Serjeant-At-Arms* tafadhali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu utakaokuwepo wataketi kulia kwangu na kushoto kwangu na wataitwa majina mmoja mmoja na kwa niaba ya wananchi wote wa Tanzania watashikana mikono na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani. *(Makofi)*

Baada ya hapo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo halafu ndiyo Waziri Mkuu atahitimisha. Ahsante sana.

Nitaomba wanapoingia, basi tuweze kusimama na kuwapigia makofi, siyo lazima kusimama? Haya tukae basi. Karibuni sasa. *(Makofi)*

*(Hapa Wachezaji wa Timu ya Taifa Stars waliingia Ukumbini na kuchukua nafasi zao)*

**SPIKA:** Naomba wengine wakae upande wa kulia na wengine kushoto kwangu. Nadhani tumeenea. Basi viongozi wa timu, *Coach* Maximo pamoja na wasaidizi wake na Wachezaji wa timu ya Taifa karibuni hapa Bungeni.

Namwita sasa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo aweze kusema machache. Karibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Taarifa!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Kwanza, tunafurahi kuwapokea lakini kwa masikitiko hatumwoni mtu mmoja hapo ambaye yupo katika sehemu hii naye ni Kocha Msaidizi Ally Bushir.

**SPIKA:** Yuko wapi Ally Bushir? Alah! Ahsante sana Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kutukumbusha. Hilo lilikuwa ni kosa kabisa! Wekeni kiti hapa kwa ajili yake. *(Makofi)*

*(Hapa Kocha Msaidizi Ndugu Ally Bushir aliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Karibu Kocha Msaidizi. Mara nyingine yakitokea makosa kwenye hafla mtu anapata heshima maalum. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri karibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wizara ya Habari ya Habari Utamaduni na Michezo kutoa tu machache ili shughuli hii iendelee.

Kwanza ninapenda nichukue nafasi hii kutamka na kutoa pongezi kwa Wachezaji na kusema tu kwamba tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba timu imekwenda Burkina Faso na wamerudi salama na katika wote waliopo hapa hakuna hata mmoja ambaye anaumwa. Kwa bahati mbaya tu ni kwamba walipoondoka Tegete alikuwa anaumwa macho ambayo ni *Nairobi Eyes* ambayo Dar es Salaam ipo, lakini sasa hivi hali yake ni nzuri hata macho yake yanaona vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba ni vizuri tukafahamu kwamba shindano hili ni shindano gani, kwa kifupi. Ni mashindano ya kutafuta mshindi katika mashindano ya Kombe la Mataifa Huru ya Afrika ambayo yanafanyika kila baada ya miaka miwili na mwaka 2008 mashindano haya yatafanyika nchini Ghana.

Sisi tupo katika kundi la saba, timu yetu inashiriki. Zipo timu nne. Ni Tanzania, Burkina Faso, Msumbiji, pamoja na Senegal. Ni mchezo wa ligi ya nyumbani na ugenini timu yetu kama ambavyo wote tunafahamu imejitahidi kucheza michezo mingi na katika michezo hiyo yote waliyoicheza sasa tunapiga *round* ya pili. Tumeshacheza *round* ya kwanza na sasa tunacheza *round* ya pili ambayo tumebakiza mchezo mmoja na Msumbiji.Kama ambavyo inajionyesha matokeo yalivyo ni kwamba timu yetu mpaka sasa imejitahidi tumefungwa mchezo mmoja tu na tumeshinda michezo miwili na tumetoka suluhu michezo miwili. *(Makofi)*

Hizi ni dalili nzuri kwa sababu tunayo matumaini makubwa kwamba mpaka sasa hivi sisi ni wa pili lakini kama tukishinda mechi na Msumbiji kwa magoli mazuri tuna uhakika wa kwenda Ghana. Kwa hiyo, kitu cha msingi ambacho tunakililia ni kwamba tunacheza tarehe 02 Septemba, 2007 timu yetu ina maandalizi mazuri na wana programu nzuri ambayo imeandaliwa na Chama cha Mpira na Wizara ikaipitisha chini ya udhamini mzuri wa mashirika matatu na ningependa mashirika hayo niyapongeze kwa dhati. *(Makofi)*

Mashirika hayo ni *Serengeti Breweries* ambao wao ndio wadhamini wakubwa ambao kila mwaka wanatudhamini Shilingi milioni 770 na wametupa udhamini wa miaka mitatu.

Kwa maana hiyo ni Shilingi bilioni 2.2. Wengine ambao wanatudhamini ni Mbunge mwenzetu ambaye tunaye, Mheshimiwa Mohammed Gulam Dewji, ndiye aliyetoa chachu ya kutudhamini Shilingi milioni 100 kwa kuanzia lakini ameendelea kutuongezea fedha kila tunapokwenda. Juzi kabla hatujaondoka alitoa tena shilingi milioni 100.

Kampuni nyingine ambayo kwa kweli inatusaidia sana ni Benki ya *NMB*. Benki ya *NMB* ilipoanza ilitupa Shilingi milioni 400 lakini hawakuchoka wamekuwa wakituambia kwamba kama tuahitaji vifaa wanatupatia na bado wanaendelea kutoa udhamini.

Kwa hiyo, hii ni hali ambayo imetusaidia Serikali kwa kiasi kikubwa sana, kwa sababu tatizo kubwa ilikuwa ni namna ya kuiweka kambini timu na kuisafirisha, lakini hawa wametuwekea jambo nzuri sana.

Jambo lingine zuri zaidi ni kwamba, pia Kampuni ya *Serengeti Breweries* wako tayari sasa hivi na wameomba *TFF* waandae programu ya kupeleka timu yetu Belgium ama Denmark kwa ajili ya mazoezi. Kwa hiyo, tunaamini kwa kipindi cha miezi mitatu hii pamoja na ligi ya ndani ambayo inachezwa, lakini bado kuna muda ambapo timu yetu itapata mafunzo ili iweze kufanya vizuri katika mechi iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali baada ya kuona kwamba sisi kama Serikali peke yetu hatuwezi kwenda, tuliunda Kamati na Kamati hii inaongozwa na Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Mohammed Dewji ambaye yeye katika msafara wa timu hizi zinazokwenda kucheza haijawahi kukosa kwenda hata siku moja, hata leo kama mnavyomwona ndiye ameongozana na timu na amerudia nayo ikiwa na ushindi.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza ile Kamati. Kamati hii ina watu 12 wafanyabiashara madhubuti kabisa akiwemo mwanamke mmoja mashuhuri sana na ambaye anatusaidia Sala Masasi. Ni mama shupavu, ni mama ambaye anajua kutafuta fedha na ni mama ambaye yuko mstari kuhakikisha kwamba Timu ya Taifa inafika katika ngazi nzuri. Naomba tumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Sala Masasi leo hatakuwepo, lakini naye pia katika misafara huwa hakosi, hata walipokwenda Msumbiji alikwenda, lakini kwa sababu ya shughuli nyingi leo hakuweza kuwa pamoja na sisi. Tunao wengi katika Kamati hiyo, lakini walijiteua wawili. Lakini naomba nimtaje mwingine ambaye alikwenda na msafara huu, ni Mheshimiwa Dr. Dau - *Managing Director* wa *NSSF*. Yeye aliongozana na wachezaji, naye yupo katika msafara huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kitu kimoja cha mwisho tu kwamba kumbe mkijipanga vizuri inawezekana. Lakini nataka niseme kitu kimoja kikubwa kwamba haya yote mnayoyaona ni ile nia ya kukifungua kitabu cha Ilani ya Uchaguzi ya CCM ukurasa wa 116. Kitabu kile kinaelezea kwamba Serikali ya Awamu ya Nne na Ilani ya Chama cha Mapinduzi itahakikisha kwamba inaibua vipaji na kuendeleza vipaji na kuhakikisha kwamba michezo inakuwa ni sehemu ya maendeleo katika nchi yetu. *(Vigelegele/Vifijo).*

Kwa hiyo, hili ni suala la utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu na mimi napenda nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa hili. Lakini kubwa ya yote kila mahali unapoona pana mwelekeo, basi kuna kiongozi juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa chachu ya furaha ya Watanzania. Michezo ni amani, michezo ni uzalendo, michezo ni upendo na michezo ni umoja. Jana au juzi usiku Watanzania wengine hawakulala. Mimi katika maisha yangu sijawahi kupata simu nilizopata zaidi 200 mpaka betri ya simu iliisha. Nikaichanji tena, watu wanavyopongeza, wengine wamepagawa kwa sababu ya kupenda michezo. *(Vigelegele na Vifijo)*

Kwa hiyo, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, hasa alipoamua kwamba lazima tupate mtaalam anayeweza kufundisha soka. Akasema mwenyewe kwamba tutaajiri makocha wenye uwezo na kweli kwa juhudi zake tulimpata Maximo. Lakini hakuishia hapo tu. Ni kwamba, kocha mmoja hatoshi akasema tufanye kama wenzetu wanavyofanya katika dunia.

Mheshimiwa Spika, katika Dunia ni kwamba kuna kocha msaidizi ambaye ni mzalendo mwenzetu Ali Bushiri na kwa bahati nzuri Ali Bushiri mimi nilipokuwa kocha wa Taifa yeye alikuwa golikipa wangu wa Timu ya Taifa. Huyu Ali Bushiri mimi nilipokuwa kocha mwaka 1980 nilipoipeleka timu kwenye *Finalize Africa Cup* nilikuwa naye golikipa wangu. Kwa hiyo, tuna msaidizi mahiri ambaye anaiga mbinu ili hata Maximo akiondoka tunaye mtu wa kuiga na wengine na wengine. *(Vigelegele/Vifijo)*

Mheshimiwa Spika, lakini tumeajiri makocha wengine wawili. Tunaye kocha wa viungo, huyo ni kijana mzuri anaitwa Itamar naye anatoka Brazil ana *Masters* kwenye *Physical Education*. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, tunaye kocha wa vijana. Tulisema kwamba tuanze kwenye wadogo, anaitwa Tinoco, naye pia ameongozana na timu naye anatoka Brazil. Lakini

zote hizi ni juhudi za Mheshimiwa wetu Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo, naomba nimpongeze sana na sisi tumuunge mkono na Watanzania wote tuunge mkono katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe utangulizi huo ili Mheshimiwa Waziri Mkuu azidi kuendelea. Nawashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye angehitimisha, sio vizuri aseme halafu tena ndiyo wakapeane mikono, itakuwa ni kinyume. Kwa hiyo, sasa Katibu kwa ule utaratibu kwamba Naibu Waziri atampa nafasi kiongozi wa msafara ama yeyote yule awataje kwa majina ili wapeana mkono kwanza kila mmoja.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba katika msafara tulikuwa na Mheshimiwa Mahammod Thabit Kombo - Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kutoka Zanzibar. Nitamwomba yeye kama kiongozi wa msafara aweze kuwatambulisha wachezaji wake na kama ana mambo mengine, basi ataendelea. Karibu Mheshimiwa Thabiti Kombo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - ZANZIBAR (MHE. THABITI KOMBO):** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, Wabunge wa wananchi na wale wote wa kuteuliwa, naomba kwa heshima na taadhima kuiwasilisha mbele yenu kwa pamoja timu ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imevunja rekodi ya miaka 30 katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mashujaa hawa kwani sisi wenyewe tunaamini kwamba ni mashujaa kutokana na kuvunja rekodi hiyo. Pili, kwa nafasi ya heshima na taadhima ambayo mmetupa nyinyi leo kupitia kwako Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sote kwa pamoja kuweza kuingia katika Bunge hili kukaa pamoja nanyi, hiyo ni heshima kubwa sana ambayo wanapewa mashujaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nishukuru sana kwa dhati kwa niaba ya timu nzima kwa bahati hii niliyopata mimi kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchaguliwa na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mfumo wake wa kudumisha Muungano kwamba mimi niwe ndiyo kiongozi wa msafara huu na pia naomba niwashukuruni sana kwamba bahati hiyo mmenipa na mimi nimekuja na bahati hiyo nyingine ya kwamba tumekuja na ushindi. *(Makofi)*

La mwisho kabisa, Mheshimiwa Spika, kabla hatujaondoka tulibahatika kupata ujumbe maalum kutoka kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na ujumbe wake kwa bahati nzuri ulikuwa na maneno machache sana. Alitoa maneno mawili tu alisema: “Nipeni Raha:” Magazeti yakaandika jamani nipe raha.

Mheshimiwa Spika, sasa maneno hayo mawili kupitia kwako sisi tunaomba na kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ujumbe wetu urudishwe kwake kwamba tumemletea raha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama kiongozi wa msafara tumekuwa muda wote pamoja na viongozi wenzangu na huu ni ushindi wa pamoja, na sitomtendea haki ikiwa mimi nitataja wachezaji wote na viongozi wote, kocha Marcio Maximo ambaye tulikuwa naye karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, nakuomba tena uniruhusu nafasi hii nimkaribishe kocha wetu aliyetuletea ushindi Maxio Maximo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ruksa Kocha Maximo.

*(Hapa Kocha Maximo aliwatambulisha wachezaji)*

**MR. MARCIO MAXIMO:** First of all, I would like to say that we are very proud to be with you here because for us it is not just a coach job it is a Taifa job. (Applause).

I think that all segments of this country work for it, not only coach players, directors, Government, responses, federation or people, but everyone in Tanzania. So, they take their own responsibility to grow. As I said, we are team work, everybody here have his/her own responsibility, everybody did, you will do, and everybody will do more. Because we just begin like all the time I talk. Because we are just beginning as I always say, we will never promise nothing. You ask us to work and we promise you that we will fight until last minute. you promise work, we promise fight until last minute. *(Applause)*

I would like to introduce my colleagues. We have our Manager upstairs, are our keeper met Manager Fred Tambati, our duty manager and Technical staff, Mr. Migoye. And down here are our players as follows: Mr. Ali Mustafa - our goalkeeper, Mr. Amir Mafah, Mr. Ibrahim Mwaipopo, Mr. Salvatory Ntebe, Mr. Abdullaham, Mr. Shaaban Nditi, Mr. Erasto Nyoni, Mr. Salum Sued, Mr. Nizar Khalfan, Mr. Joseph Kaniki and Mr. Shadrack Nsajigwa. Others are my staff Mr. Ally Bushiri, Mr. Itamar, Mr. Marcos Tinoco, Mr. Vincent Barnabas, Mr. Dahni Mlwanda, Mr. Said Maulid, Mr. Ivo Mapunda, Mr. Nadir Kanavalu, Mr. Haruna Moshi, Mr. Henry Joseph, Dr. Shed and Mr. Malegesi. *(Applause)*

*(Hapa Wachezaji walipeana mkono na Mheshimiwa Waziri Mkuu)*

And for finally, I would like to say that we don't do nothing, if we don't play ask me to work. Our sponsors Serengeti, *NMB, MTL*, Mohammed Dewji, Dr Dau, the Government supported us since the first minute of our federation. *(Applause)*

And I would like to express my appreciation to Tanzanians because when I took to the street after loosing the first match still everyone encouraged and supported us. *(Applause)*

And lastly I would like express my sincerely appreciation to our President Jakaya Mrisho Kikwete and Minister Muhammed Seif Khatib - Minister for Information and Culture, Deputy Minister - Joel Bendera and everybody who work with us to reach our goals. Ahsante sana. Tupo pamoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mr. Maximo will you shake hands now with two leaders.

*(Hapa Coach Marcio Maximo alipeana mkono na Viongozi)*

**SPIKA:** Kiongozi wa msafara umalizie sasa kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO–ZANZIBAR (MHE. THABITI KOMBO):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nimeambiwa kwamba Vyombo vya Habari vimekuwa vikitoa majina mbalimbali ya mfungaji, lakini mfungaji aliyefunga goli anaitwa Erasto Nyoni na nitamwomba asimame ili aonekane.

*(Hapa mfungaji wa goli Ndugu Erasto Nyoni alisimama)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO – ZANZIBAR (MHE. THABITI KOMBO):** Ule ulikuwa ndiyo mchezo wake wa kwanza *official game* katika Timu ya Taifa. Mchezo kabla ya hapo alicheza *friendly* na ile timu ya Zambia. Lakini *officially* mchezo ule ndiyo ulikuwa wa mwanzo kwa yeye na hilo lilikuwa ndilo goli lake la mwanzo katika Timu ya Taifa ya Jamhuri Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tutajie nafasi yake katika timu anacheza nafasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO – ZANZIBAR (MHE. THABITI KOMBO):** Yeye ni beki.

**SPIKA:** Mnaona! mafunzo hayo! Beki ndiye aliyefunga goli!!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO – ZANZIBAR (MHE. THABITI KOMBO):** Alitoka nyuma akaja kufunga mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, labda kwa kuwapa raha zaidi ya hilo suala liloulizwa ni kwamba wakati amekwenda mbele alikuwa anatafuta mtu wa kumpasia akawa hajamwona. Kwa hiyo, alichofanya, yeye akasema ninawasubiri, lakini hakuna mtu

aliyetokeza, kwa hiyo, akamsubiri golikipa ndiye aliyekuja akaupenya mpira juu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba tutoe shukrani zetu kwa dhati kwa wafuatao bila kuwasahau Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, ambaye ndiye aliyeniteua mimi rasmi kuwa kiongozi wa timu hii, pamoja na Manaibu wake Mawaziri wawili ambao tumekuwa nao muda wote tukishirikiana Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Daniel Nsanzungwanko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia tutoe shukrani zetu za dhati kwa Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Andrew Chenge na Naibu Waziri - Mheshimiwa Dr. Maua Daftari pamoja na Naibu Waziri - Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga. Shukrani zetu za dhati ziwafikie kwa sababu ndiyo walioshughulikia usafiri wa ndege ya Serikali ya Foka 50 kwa ajili ya kwenda huko na kurudi. Safari yetu nzima ilikuwa ni ya masaa 16.

Tulisimama katika nchi tatu, tukianzia Bujumbura, Burundi, tulipotoka hapo tulikwenda Kinshasa, tulipotoka Kinshasa, tulikwenda Libervial Gabon na baadaye hapo ndiyo tufika Burkina Faso katika Mji unaitwa Oagadougou, wenyewe wanaita Oaga kule. Kwa hiyo, safari yetu kwa ujumla ilikuwa ni ya masaa 16 ya kwenda na masaa 16 ya kurudi. Kwa hiyo, tulipoteza siku moja karibu na nusu katika kusafiri tu.

Mheshimiwa Spika, wa mwisho kabisa wa kuwashukuru bila ya kuwasahau waliokwishatajwa ambao ni wafadhili wote kwa jumla ni ma-*pilot* wawili ambao wamekuwa wakishirikiana na *co-pilot* wao pamoja na *cruel* wote ambao muda wote walikuwa pamoja na sisi; na la mwisho kubwa walilolifanya zaidi kwenye uwanja wa mpira walivaa jezi za Tanzania na wakawa ndiyo wapiga kelele wakubwa sana katika kushangilia. Naomba ma-*pilot* pamoja na *cruel* msimame ili waonekane. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea maombi ya baadhi yetu kutaka kuchangia. Nadhani hakuna haja. Akishasema Kiongozi wetu wa Shughuli za Serikali humu Bungeni Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani itatosha. Ila kutakuwa na dakika moja tu ya shukrani kutoka Mheshimiwa Mohamed Dewji aliyefuatana na wachezaji. Kwa sababu baada ya kusema Waziri Mkuu, timu haiwezi kuwa bubu. Nadhani baadhi ya maneno atakayosema nayo yatakuwa ni mazuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mohamed Dewji nitampa dakika mbili aweze kushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Vigelegele/Vifijo)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kama ninajiandaa kujibu hoja hivi. Kwanza, napenda kutumia nafasi hii kupongeza sana utaratibu huu wa kuja kuipongeza Timu, hapa tumefanya jambo zuri sana.

Lakini la pili, niwaambie tu, yule aliyesema nipe raha niliongea naye jana usiku, Mheshimiwa Rais na amefurahi sana. *(Makofi/Wimbo)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walianza kuimba wimbo wa mpeni raha Kikwete)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Rais anawapongeza sana. Lakini nina hakika nitakuwa ninazungumza kwa niaba ya Watanzania kuwaambia kwamba Watanzania wote tumefurahia sana sana. Lile goli moja lilisaidia kujenga mshikamano na umoja ndani ya nchi yetu kwa hali ya juu sana. Maana baada ya lile goli nchi nzima ilirindima kwa furaha na vigelegele. Ni kielelezo sahihi kama alivyosema Naibu Waziri - Mheshimiwa Joel Bendera ni uamuzi wa Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake kuweka umuhimu wa michezo, sasa unabainika. *(Makofi)*

Lakini vilevile uamuzi wa Rais wenyewe kulivalia njuga suala hili na kulisimamia, vilevile maana yake sasa inaonekana. Inaonekana kwa sababu michezo hii inajenga umoja wa Kitaifa kuliko kitu kingine chochote. Kwa hiyo, napenda sana kuipongeza timu hii kwa kazi nzuri waliyoifanyia nchi yetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

La pili, nimpongeze kocha Bwana Maximo, tumekusikia hapa na kazi yako tumeiona. Hongera sana Maximo. Kazi bado mpaka tucheze na Msumbiji halafu baadaye tukifanikiwa twende Ghana.

Sasa mimi nataka kuwapa changamoto hapa Bwana Maximo na timu yako kwamba mkichukua ushindi Ghana tutakuja tena kuwapongezeni kwa hali ya juu sana ndani ya Bunge hili. Sisi tunaamini kwamba uwezo wa kwenda kushinda Ghana mnao.

Mheshimiwa Spika, nimeona timu ya Msumbiji juzi ikicheza, nadhani hata Msumbiji tunaweza tukawashinda, mnao uwezo huo. Kwa hiyo, tunaomba mjitahidi muendelee kujiandaa vizuri mkijua kwamba kazi iliyoko mbele ni ya kuchukua huo ushindi. Tafadhalini sana msituangushe. *(Makofi)*

La tatu, jana usiku baada ya kujulikana kwamba mtakuja hapa Bungeni, baadhi ya watu walitupigia simu wakitoa michango. Lakini vilevile Bunge letu hapa leo asubuhi limeamua kwa kauli moja kwamba wenyewe watawapa zawadi na zawadi hii inakwenda kwa wachezaji wenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatangazia kwamba Waheshimiwa Wabunge wanatoa Sh. 33,895,000/=. Ninarudia. Inakwenda kwa wachezaji wenyewe na kocha wao. *(Makofi)*

Lakini vilevile Wizara ya Miundombinu na Mashirika yake wameandaa shilingi milioni 70. Walionipigia simu mmoja ni Mheshimiwa Nimrod Mkono atatoa Shilingi milioni 20, wa pili ni A to Z kile kiwanda kinachotengeneza vyandurua kule Arusha watatoa shilingi Shilingi milioni 17. Kampuni ya *OIL COM* itatoa shilingi milioni 10 na Kampuni ya *Export Trading* itatoa Shilingi milioni tano. Michango hii inaendelea katika baadhi ya Mashirika ya Serikali na tuna hakika tutafikisha kitu kikubwa cha kuwaonyesha furaha yetu na kuwatia moyo ili mkafanye vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema tumefanya maamuzi mazuri sana. Tumewapa vijana wetu heshima wanayostahili na heshima hiyo iko hapa ndani ya Bunge letu. Hongereni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. Kwa kuwa inawezekana tukapitiliza kidogo dakika mbili, tatu, namwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu aweze kusimama na kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 21 inayozingatia muda ili tumalize shughuli hii vizuri bila kuathiri Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILD S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 124, naomba Kutengua Kanuni ya 21 fasili ya (3) ili kuwezesha Bunge letu liendelee mpaka tutakapomaliza shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni ya 21 ilikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Mohamed Dewji nilikuwa napenda kusema kwamba, jana usiku Waheshimiwa Wabunge tulipoanza kuchangachanga lengo letu lilikuwa ni wachezaji na kocha. Kwa Sh.33,000,000/= tulizochanga sitazamii mchezaji kupata chini ya shilingi milioni moja. Naomba niliweke wazi hili. Kusije kukatokea hapa gharama sijui nani, sijui nani aah!!!! Kila mchezaji wa timu yetu kwa shilingi milioni 33, ni lazima apate sio chini ya shilingi milioni moja.

Naomba sana Mheshimiwa Bendera, tafadhali msimamie hilo. Hayo ndio utashi wa Wabunge. Sasa hizo nyingine alizozitangaza Waziri Mkuu basi mtajuana utaratibu wake.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Na tupate ripoti.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nasema tu kwamba hata nilizotangaza shilingi milioni 47 zenyewe ni hivyo hivyo kwenda kwa wachezaji na kocha. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Lazima kutakuwa na itifaki, Mwalimu na Mwalimu Bushir msaidizi watapata zaidi pamoja na wasaidizi Atamar na Tinoco. Ndiyo, mwalimu hawezi kupata sawa sawa na mchezaji na hasa kwa sababu Bingo imeongezeka sasa ni kubwa zaidi inaelekea kwenye shilingi milioni 70 na kitu sasa naona mambo ni mazuri. Ila ningeomba tu *TFF* fedha hizi ni nyingi sana kwa vijana wetu, shilingi milioni 100, inaweza kuwafikisha kila mmoja kupata pengine shilingi milioni tatu. Sasa bado kazi inaendelea. Kwa hiyo, lazima TFF waweze kusimamia vizuri na hususan kuweza kuwa na akaunti na kadhalika. Tunataka tufike Ghana jamani! Kwa hiyo, isianze tena kijana amepata Shilingi milioni tatu anaonekana katika kilabu za usiku, anakoga watu na vitu vya namna hiyo. Niliona niweke tahadhari hiyo.

Baada ya tahadhari hiyo naomba sasa Mheshimiwa Mohamed Dewji kama mwenzetu ambaye amekuwa akiandamana na timu atoe maneno fulani ya shukrani. Karibuni Mheshimiwa Dewji.

**MHE. MOHAMED G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa leo ni siku ya kwanza kwangu kuongea kwenye Bunge hili Tukufu. Napenda kutoa shukrani kwa wananchi wa Singida kunichagua na kunipa kura nyingi sana na nawaahidi sitawaangusha kamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Amekuwa nasi tangu mwanzo, ametulea ametusaidia amejitolea kwa hali na mali. Kwa hilo nasema "*Thank You Mr. President*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge kwa kutupa heshima kubwa, kutualika hapa Bungeni. Nasema ahsanteni sana. Tatu, napenda kutoa shukrani kwa Wizara ya Michezo, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Nswanzugwanko, Mheshimiwa Mahmud Kombo, Mkuu wa msafara, nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Nne, napenda kutoa shukrani kwa wadhamini, *Serengeti Breweries, NMB,MTL*.

Tano, napenda kutoa shukrani kwa *Tanzania Football Federation. President* Tenga, Magori tuko bega kwa bega ahsante sana. Sita, kwenye Kamati ya Ushindi nitawataja Dr. Dau, Malinzi, Mama Masasi, Shabri Haji, nasema ahsanteni kwa ushirikiano wenu. Saba, napenda kutoa shukrani kwa Kocha Maximo na wasaidizi wake Atamar, Tinoco, Ali Bushir, Dr. Keep Manager ahsanteni sana. *(Makofi)*

Nane, napenda kutoa shukrani kwa wachezaji, hawa ni majasiri, wapiganaji. Kwa wachezaji nasema *go, Tanzania go? (Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** *Go!!*

**MHE. MOHAMED G. DEWJI:** Tisa, nawashukuru *last but not least* wananchi. Wametuombea, wameonyesha upendo mkubwa, sijawahi kuona uzalendo kama huu

Tanzania na wana muziki, Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars, *J.K. Boys* nasema ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha Shughuli za Bunge, sasa nitawaomba wageni wetu waweze kutoka ili tuhitimishe shughuli za mchana huu. *Sergeant-at-arm* angalia utaratibu ili waweze kutoka.

*(Hapa Wachezaji wa Taifa Stars Waliondoka Ukumbini)*

*(Saa 07.08 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa. 11.00 jioni Bunge lilirudia.)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuwashukuru kwa jinsi tulivyowapokea vijana wetu wa timu ya Taifa ya Soka. Nimearifiwa wamekwishawasili Dar es Salaam kwa mapokezi makubwa. *(Makofi)*

La, pili nilikuwa nataka nitoe vidokezo vingine kuhusu tukio hilo kwa ajili ya kumbukumbu tu. Kwanza katika Timu hiyo vijana tisa ni vijana wanaosoma Shule za Sekondari. Kwa hiyo, ina maana kuna timu endelevu ya baadaye sio watu waliochoka ama vipi, tisa ni vijana wadogo wapo Sekondari na wanne wao wapo Sekondari ya Makongo. Pia, baada ya moto mliouwasha wa kuchangia nchi nzima imesisimka na ninafurahi kuwaambia sasa kwamba michango iliyopatikana na ile iliyoahidiwa imefikia sasa shilingi milioni 320. Nilioupata sasa hivi kutoka kwa Mkurugenzi wa *TIOT*, orodha itapatikana baadaye, lakini huyu ametuomba tutangaze, nadhani sasa hivi anaangalia TV, nadhani Bwana Meley alikuwa amekusudia kutoa shilingi milioni 3.0 lakini baada ya ushindi ameamua kutoa milioni 10 na amewakabidhi fedha hizi taslimu *Dar es Salaam Airport. (Makofi)*

Ametuomba tutambue mchango huu kama kuwahamasisha na Watanzania wengine ambao watakuwa bado wanapenda kuchangia. Ofisi ya Habari, Utamaduni na Michezo inaendelea kupokea na kuratibu michango. Kama ulivyosema mapema, ninayo orodha ya wachangiaji 72 na nilikwishawataja kwa mpangilio. Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa John Cheyo. Tutaanza sasa na Mheshimiwa Mongella.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2006, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia Hoja za Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Hoja ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, nami naomba nijumuike kwa kutoa rambirambi kwa wale ambao wamepata maafa katika basi lile lililokuwa linakwenda Mwanza na rambirambi hizi ziwafikie wote waliohusika na familia zao. Ningeomba pia nichukue dakika moja kuwashukuru wale wote ambao walituma salamu za rambirambi kwa sisi wananchi wa Ukerewe wakati tumempoteza Mwenyekiti wetu Edward China Tegile ambaye alikuwa ni Mtanzania hodari na mpenda Chama cha Mapinduzi amekulia katika chama mpaka mwisho wa uhai wake na kuungana na suala hilo, napenda pia kwa namna ya pekee nifikishe shukrani za wale wote waliokuja kutuhani na pole za wananchi wa Ukerewe kwa wale ambao walipata maafa wakati wanakuja kutuhani ambao ni Mheshimiwa Diallo, Mheshimiwa Hewa, DC Wilaya ya Ukerewe ambaye nitahama naye kwenda Tunduru, Mwenyekiti wa *Council* Wilaya ya Ukerewe, Katibu wa Chama wa Mkoa wa Mwanza na Mwenyekiti wa Chama Mkoa wa Kagera na Meneja wa *Monarch Hotel Mwanza* na Manahodha wawili waliokuwemo katika chombo hicho.

Tunamshukuru Mungu kwamba alinusuru roho zao na tutaendelea kuomba wakati wote maafa yanapotokea angalau kuwe na namna ya kuokoa maisha ya wananchi. Sitaki kuchukua muda mrefu nataka sasa niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, bajeti ni matokeo ya Mpango. Mimi kama Mwalimu, nasema mwanafunzi ukimwona amemaliza udaktari ni matokeo ya *curriculum*. Kwa hiyo, pesa tunazozipanga hapa ni pesa zinazopaswa kwenda kutekeleza mpango tulionao. Kwa hiyo, changamoto iliyo mbele yetu nadhani ni kuangalia jinsi bajeti na mpango wetu vinavyoendana kutaka kukidhi mahitaji yetu. Sasa katika kufanya hivyo, mimi nataka niseme wazi kwamba Bajeti hii si nyepesi. Atakayesema bajeti hii itapokelewa kwa vigelevigele kama ya mwaka 2006 ambayo tulikuwa tumepunguza kodi atakuwa ni mwongo. Watu wanalalamika juu ya mafuta, watu wanalalamika hasa mafuta ya taa na ni kawaida tunapokuwa na Bajeti. Kodi ikiongezeka lazima kuwe na malalamiko. Lakini sisi tunaoongoza wananchi tunataka tuseme nini?

Mimi nitasema kwa kifupi sana. Bajeti imeonyesha kwamba tuko katika hali ngumu ya uchumi na hali hii lazima tuidhibiti haraka. Namna yoyote ile tutakayoifanya kutakuwa na ukali kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, kama tunaongoza na ni viongozi thabiti ni lazima tuwe tayari kwenda kueleza Bajeti hii kwa wananchi ili waweze kuielewa na wakati huo huo tukiwa na dhamana kama wasimamizi wa Serikali turudi tusimamie mapato yatakayotokana na Bajeti hii. Mimi ndivyo naona mantiki ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tumesema tufunge mikanda na Watanzania sio mara ya kwanza. Wakati wa vita ya Idd Amin tulifunga mikanda kwa miezi 18 na tulifunga na tukaendelea kufunga kwa sababu baada ya vita ndiyo makali ya vita yakaanza kujionyesha tukaendelea kufunga mkanda. Kwa hiyo, nadhani kilichopo sasa hivi ni

Serikali iwe wazi tu kwamba tupo katika hatua za kufunga mkanda. Mimi kama Mwakilishi wa wananchi nina haya ya kusema:-

Mheshimiwa Spika, nitakuwa tayari kuelezea juu ya Bajeti hii na makali yake, lakini tukubaliane na Serikali kwamba nidhamu iwepo ndani ya utekelezaji wa Serikali ya kutueleza hatua kwa hatua baada ya miezi mitatu, si vibaya kwa mfano tukaambiwa mafuta kodi tuliyoipiga tumepata kiasi hiki na kiasi hiki kimepelekwa kwenye barabara ya Geita, barabara ya Kigoma, imepelekwa kwenye Gati ya Mafia na imepelekwa kwenye vifaa vya majini vikiwemo vya kuokolea maisha ya wananchi. Mimi kwangu hilo ndiyo la muhimu. *(Makofi)*

Kwangu hilo ndilo la muhimu. Kwa vyovyote vile, hata Serikali za nchi nyingine, kila akitaja Waziri hapa tumesaidiwa na Finland, makofi, tumesaidiwa na nchi, makofi; maana yake wale watu wanafunga mkanda kwa ajili ya maendeleo yao, lakini huwa wanaongeza ziada kwa ajili yetu sisi. Kwa hiyo, itaonekana ni kitu cha ajabu tusikubali kufunga mikanda lakini itaonekana ni ajabu zaidi wananchi wafunge mikanda sisi Wabunge tusiiulize Serikali zile pesa zimekwenda wapi. Mimi nadhani hilo ndilo la msingi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, najua hilo litapita. Tumeifanyia kazi, wote tumeizungumza kwa makini na ikishapita mimi kwa kweli naomba Waheshimiwa Wabunge tuulize maswali ya kudumu. Pesa ziko wapi? Nayasema haya kwa sababu kama mtakumbuka Rais alikuwa mkali katika kusoma Ripoti ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini na sisi huko tulipo tumeona ubadhirifu unaofanyika na kazi hafifu zinazofanyika ambazo huwa hazisaidii ufungaji ule wa mkanda. Sasa hivi tuwe wakali zaidi. Tuisaidie Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama linajengwa darasa, lijengwe darasa kweli! Kama inatengenezwa barabara itengenezwe barabara kweli. Katika Bajeti hii bei za mafuta ya taa, zitasumbua wengi. Katika Jimbo langu, litatusumbua kweli kwa mapato ya Wilaya kwa sababu tunatumia mafuta ya taa kuvua dagaa, tunatumia mafuta ya taa kuwasha nyumbani, mafuta ya taa ndiyo msingi wa kazi tunazozifanya. Lakini leo mimi Serikali ikiniahidi ya kwamba huo mkanda wafunge tu wenyeji wa Ukerewe tutakuja kuwaonyesha matokeo yake baada ya kufanya kazi kwa muda huu wa mwaka mmoja. Mimi Bajeti hii sina matatizo nayo. Serikali lazima itoze kodi. Ugomvi wangu ni pesa ziende wapi? Ndiyo ugomvi wangu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziende wapi? Ningeomba pia Serikali itusaidie. Kuna maeneo ukiwekeza tu umepata. Ukiangalia Bajeti hii imetueleza ya kwamba asilimia 48 ya Mapato imetokana na dhahabu, asilimia nane imetokana na samaki na sio samaki wengine isipokuwa ni samaki wale wanaotoka Ziwa Victoria ikiwemo na Ukerewe.

Sasa swali, wataendelea kuvua, wataendelea kuchimba dhahabu, kigugumizi kinatoka wapi kutengeneza barabara zinazokwenda kwenye dhahabu? Kigugumizi kinatoka wapi kununua *speed boat* ya kuokoa maisha ya wale walioko majini? Kigugumizi kinatoka wapi kusadia wale wote walio katika msururu mzima wa kuhakikisha ya kwamba tuna pato la kutosha? Naweza kutaja Mafia, Zanzibar,

ningeweza kutaja Tunduru, mahali pote kule ukiweza kuangalia kwa mfano Kigoma sasa hivi na rutuba iliyopo utavuna harana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani suala la pili sio kusimamia tu matumizi suala la pili ni kuhakikisha ya kwamba tuchague maeneo yatakayotunusuru haraka ili hata kama wananchi wamefunga mkanda waweze kupata kupumua kwa sababu ya kuongezeka kwa pato la haraka ili tusiendelee kuwa tunafunga mkanda mpaka tukakatika viuno. *(Kicheko/Makofi)*

Jambo lingine ambalo mimi ningependa niliseme ni saula la maisha ya watu. Nisipolisema hili nitakuwa sijasema. Usalama wa watu ndani ya vyombo vya kusafiria ni hatari. Ukiangalia kama Singida, watu wameungua tukiwa hapa, hakuna gari la zimamoto. Hivi ni pesa ngapi kununua gari la zimamoto, tukahakikisha kila Mji Mkuu angalau una gari la zimamoto?

Hiyo ndiyo inatia uchungu ninapoona vitu hivi vinatokea watu wanapoteza maisha kwa sababu hakuna vyombo vya kuokolea. Ningeomba tubane mikanda tutoe kodi, lakini wananchi waweze kunufaika na kuhakikishwa kwamba maisha yao ni salama.

Mheshimiwa Spika, ningependa niongeze kwamba, Bajeti hii ni kama ndani ya nyumba, ni kuamua. Ndani ya nyumba mnaweza kuamua tunajenga nyumba, tutakula maharage. Lakini mume wangu tukifunga mkanda mwenzangu analala Bar, sitamuelewa! *(Makofi)*

Lakini tukifunga mkanda, alikuwa anakunywa bia tatu akaanza kunywa moja mwishowe akaacha mpaka tukapaua nyumba nitampongeza. Kwa hiyo, mimi Serikali yangu naiona hivyo ya kwamba tuwakubalie Bajeti hii. Lakini waende, tufunge nao mikanda, tukianzia pia ndani ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna pesa huwa zinakwenda haraka haraka karibu na mwisho tunapokaribia kuja kwenye Bajeti. Kila Idara ya Serikali Serikali ina kazi na kutumia pesa ili tuje hapa, wanasema tunamalizia zile pesa. Zikome, zisiliwe haraka haraka. Tuna miradi haijakamilika, kwa hiyo, utaratibu utafutwe, Idara ambayo haijatumia isimamishe zile pesa ziweze kuwekwa ili ziweze kuendeleza miradi na tukamilishe miradi ambayo tumeiweka hasa ya barabara ambayo imetamkwa kwenye Ilani ya Uchaguzi tuanzie hapo bila kupangua mipango yetu ambayo tumeshaipanga.

Ningependa niseme wanaolipa kodi ni wachache, *TRA* kama nitakosea watanisahihisha. Walipa kodi wazito katika nchi hii ndiyo wanaolipa kodi ile yenye kishindo. Lakini wafanyabiashara wangapi ambao wangeweza kuchangia hiyo ili tusipate tena kubana wale ambao wananunua kikoroboi cha mafuta ya taa. Sasa itabidi tufanye hivyo. Lakini lazima katika kipindi hiki cha mwaka mmoja tuwasake hao na tuzuie hii *fast truck* kwa sababu mvuvi wa samaki hapiti *fast truck* anakwenda wapi? *(Kicheko)*

Tuzime hiyo, tusimame *seriously* tuiunge mkono Serikali yetu tufunge mkanda na tuhakikishe ya kwamba kila baada ya muda sisi kama watu ambao tumepewa dhamana ya kusimamia tuletewe taarifa ya jinsi tulivyopata pesa na jinsi pesa hizo zilivyoendelea. Naomba niipongeze Serikali, imefanya mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, unajua kuna wakati tunasahau? Ni Serikali hii ambayo imekazana kupata Sekondari za Kata wakishirikiana na wananchi na sasa tuna matumaini ya kwamba hata mtoto wa mkulima ataibuka kutokana na hizo Sekondari za Kata. Mimi nimefurahi vilevile kwamba *Chemistry, Physics* na *Biology* havibabaishwi. Kwa hiyo, ni kwa sababu za Sekondari za Kata. *(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, sikuwa nimesikia kengele ya kwanza, kwa hiyo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tahadhari tu kuhusu ili neno "kukazana", halipendezi sana. Lakini nashukuru kwa mchango wako Mheshimiwa Dr. Mongella na nakutakia safari njema kwenda Afrika Kusini kuongoza Bunge lile la Afrika. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa atafuatiwa na Mheshimiwa William Shellukindo. *(Kicheko)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya pili, katika hii Bajeti ya pili tangu uchaguzi. Awali, napenda nitoe shukrani za dhati kwa wananchi wa Karatu kwa sababu bila wao nisengekuwa na hii ridhaa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nawashukuru sana wananchi wa Karatu kwa kunichagua kwa kipindi kingine tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili nisisahau, naomba niseme toka mwanzo kwamba hoja hii sitaiunga mkono, kama kutakuwa na mabadiliko ninaweza nikafikiria katika maeneo nitakayozungumzia. Lakini vinginevyo kwa kweli sitaiunga mkono. Najua hata ikipita, historia itajua kwamba kuna waliokataa kuiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze tu na eneo ambalo linanifanya nisiunge mkono hoja na kwa hili naomba nipige magoti sana kwa Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na ombi la Mheshimiwa Rais wa Bunge wa Afrika la kufunga mikanda, nadhani eneo la mafuta na hasa eneo la mafuta ya taa ni eneo ambalo tunaweza kusamehe tukalirekebisha katika Bunge hili na Bajeti hiyo isiathirike sana na Waziri akaongeza kianzio kingine na mwananchi wa kawaida akapata ahueni. Hili linawezekana tukiwa na nia njema na tukipenda.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwanza mafuta ya taa. Hivi sasa mwananchi wa kawaida na sio tu wa vijijini hata wa mijini, ni hivi karibuni tumeweka utaratibu kwamba mkaa upatikane kwa utaratibu kidogo mgumu na sababu tunazielewa. Lakini matokeo yake ni kwamba gunia la mkaa ni Sh. 20,000/= mpaka Sh. 25,000/= kwa sasa.

Mwananchi wa kawaida ndiyo alikuwa tegemeo lake mkaa. Walipotoka hapo wanashindwa, hawana Sh. 25,000/= wanakimbia kwenye mafuta ya taa pamoja na majiko ya mchina. Leo tunapandisha tena ushuru tunaweka tozo kwenye mafuta ya taa, huyu mwananchi atakimbilia wapi? Kula lazima ale, lakini mjini hakuna hata miti ya kusema atakwenda kuiba kwenda kukata hata haizuru akamatwe akubali kufungwa lakini ameokoa maisha yake, hakuna miti! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tena, kila kitu hata hao watoto tunaowajengea shule, asilimia 90 ya Watanzania walio vijijini watoto hawa usiku wanasoma kwa kutumia mafuta ya taa. Tunataka watoto wetu waende Sekondari, watakwenda na nini? Tunatoa kwa mkono mmoja, tunanyang'anya kwa mkono mwingine.

Mheshimiwa Spika, ukipandisha mafuta na hapa naongelea yote, ukipandisha mafuta ya Diesel na ya Petrol maana yake mabasi yote sasa nauli itapanda.

Mheshimiwa Spika, ni nadharia ya kawaida ya uchumi, labda tu uzuie kwa mabavu wenye mabasi tuwakataze wasipandishe nayo ni kuwaonea wale wenye mabasi, malori nayo hivyo hivyo. Lakini ikipanda sio nauli tu na mazao yale yote yatakayosafirishwa. Kwa hiyo na chakula nacho kitapanda juu na nguo nazo bei zitapanda, hata kibiriti hata chumvi, hata vile vitu vidogo vyote hivi, vitu ndivyo vinavyomgusa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, huyu mwananchi ndiyo MKUKUTA ndiyo unajaribu kumnyanyua, lakini wakati tunataka kumnyanyua kwa MKUKUTA tunamkandamiza chini kwa njia hii nyingine. Napiga magoti Mheshimiwa Waziri awe tayari. Njia zipo tukiwa na nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesema njia rahisi na Waziri kivuli wa Fedha alieleza hata kwenye posho tu kwa mujibu wa sheria, Sheria zetu sasa zinataka posho zote za Semina na nini zinazotolewa na mwajiri zikatwe kodi. Hata kwenye posho tu, tukikubaliana kwenye posho tu tutapata fedha za kutosha kufidia fedha za mafuta ya taa. Anza na posho yangu, kuna Waziri ananiambia nianze na ya kwangu, nakuruhusu anza na ya kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni ajabu kama mimi nataka kutetea halafu mimi napata posho halafu huyu mwananchi wa kawaida anaumia kiasi hiki. Samaki, ni eneo lingine ambalo tunaweza kabisa bila gharama kubwa. Meli tunaambiwa ziko ngapi? Serikali yenyewe imetuambia ziko 193 na takwimu ya Serikali inatumbia, sasa tukazane tukusanye yale mapato ambayo hatuyakusanyi tufidie kutoka kwenye mapato tunayopata kwenye samaki angalau tuondoe mafuta ya taa, mafuta ya *diesel* tuweze kusaidia kunyanyua uchumi angalau wa yule mtu wa chini. *(Makofi)*

Tunazungumzia umaskini wa kipato na bahati mbaya kwenye hali hii sasa kwa mafuta, yule mtu wa chini ambaye kipato chake kiko chini ya dola moja kwa siku, kwa maana ya chini ya shilingi 1,300 kwa siku na huyu 1,300 tena ana unafuu mkubwa, wengi wao hata hiyo 1,300 kwa siku hawana, bado unakwenda kumtoza badala ya kutafuta

hivyo vianzio vingine ambavyo hata ukivitoza wale wanaotozwa hiyo hawatapata athari kubwa. Naomba nipige magoti tena Mheshimiwa Waziri, Serikali hii tunajua ni sikivu, tunaomba isikie kilio cha Watanzania kiwango hiki kiondolewe katika mafuta. *(Makofi)*

Mwaka 2006 au mwaka 2005 tuliondoa kutoka kwenye simu na simu tunatumia ni sisi wakubwa. Leo hii namgusa mdogo wa kawaida wa chini, tunashindwa nini kuondoa mafuta ya taa wakati tuliweza kuondoa kodi za simu ndani ya ukumbi huu wakati wa Bunge? Wala tusitumie kigezo kwamba wakati wa Bajeti hatuwezi kubadilisha *figures* zilizowekwa. Tunao uwezo! Tuna-*presidency* ilishatokea na tunaomba sasa hili tulifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie tu kwa kifupi hasa kwenye miji, usafiri wao wa kawaida wa haraka ni teksi. Anataka kuwahi mahali, ni teksi. Lakini unapopandisha ada kutoka Sh. 20,000/= hadi Sh. 80,000/= kwa kweli wale watu wote tumewaondolea pale. Angalau hiyo ninaweza nikavumilia Sh. 80,000/= unalipa mara moja japo ni kwa kila mwaka. Kila mwaka inaweza kuumiza, lakini angalau inavumilika. Lakini athari yake ni kwamba tunawanyima haki wale watu wa kawaida. Ninaomba sana, kadiri inavyowezekana, haya maeneo yaangaliwe upya katika kipindi hiki kabla hatujafikia kwenye Muswada wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, aliyenitangulia amezungumzia kufunga mikanda na mimi sina tatizo kufunga mikanda kwa jambo ambalo ni kweli kuna sababu ya kufunga mkanda. Wakati wa vita vya Idd Amin tulifunga mikanda, hatukulalamika, bahati mbaya tuliambiwa miezi kumi na nane. Miezi kumi na nane ikapita miaka kumi na nane. Sijui sasa ni karne ya kumi na nane na karne ya kumi na nane hatutakuwepo*! (Kicheko/ Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa, lakini katika suala hili sioni sababu ya kufunga mikanda kwa sababu Waziri wa Fedha Kivuli alionyesha mabilioni ambayo yapo nje tumeyaacha. Sio kwa sababu ya tatizo lilelo la kweli na tutapenda Waziri atuambie baadaye kama yale yaliainishwa na Kambi ya Upinzani ambayo kwa bahati mbaya tena hatuna wataalam.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina wataalam chungu nzima, wamekuwa na muda wa mwaka mzima kuandaa Bajeti, sisi tulikuwa na siku tatu tu. Kama kwa siku tatu tunaweza kufika trilioni karibu 8.0, ni 7.0. Je, kwa muda wote wa maandalizi ya Bajeti ya Serikali na wataalam wote tumeshindwa nini kuweza kupata maeneo ambayo hayana athari kwa Mtanzania wa kawaida.? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, kwa bahati mbaya na bahati hii mwanzoni sikutaka kuizungumzia pamoja na kwamba kwenye taarifa zetu tumeweza kutoa maeneo fulani ambayo tulifikiri labda ilikuwa ni maeneo ambayo kuna watu wana nia mbaya, lakini sasa ni jana tu nimepokea kutoka kwenye *E-mail* yangu na kwa bahati nzuri Bunge hili tulipitisha Sheria kwamba *E-mail* siku hizi inaweza kupokelewa kama ushahidi hata Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa imezungusha kwanye *E-mail* na imekwenda kwa watu wengi. Imekwenda kwa *World Bank,* Wafadhili wetu walioko Balozi za Ndani zilizopo hapa, zimekwenda *IMF* na watu wengine mbalimbali. Hii ni *E-mail* niliyoipokea jana na iko kwa watu mbalimbali na kuna hata Wabunge hapa ambao wamepata.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi zinatia uchungu na ndiyo maana naungana na mwenzangu kwamba kufunga mikanda ni lazima kuwe na maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii kama Waziri atataka nitamkabidhi, lakini najua anayo na anayo kwa sababu sehemu nyingine hata yeye kwenye magazeti amenukuliwa akikiri kwamba ni kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ubadhilifu wa *Debt Service Account* ndani ya Benki Kuu ni suala ambalo Waziri amenukuliwa na Magazeti kwamba lipo na sasa limezungushwa kwa wafadhili, jambo ambalo linaweza kuharibu hata jina la nchi. Tungependa Waziri atuhakikishie, haya yaliyoko kwenye *document* atujibu yote kikamilifu. Mimi sitaki kuyataja kwa majina, ni ya aibu, wanaotajwa ni majina mazito, ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa Waziri atupe majibu ya kina na ikiwezekana atueleze maeneo yafuatayo:-

Benki Kuu, *Twin Tower* inadhaniwa kwamba ujenzi ni mara nne zaidi kuliko ujenzi Mji wa London, Mji wa New York, Mji wa Tokyo. Ni kitu gani kimetokea? Hatupendi katika hili kupata majibu ya kisiasa, tunataka majibu ya kitaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Meremereta, tumejibiwa hapa Meremeta inafilisika, imekwenda mwaka jana *off shore*, tunaambiwa. Taarifa hii inaonyesha Meremeta imeuzwa kwenda kwa *Land Gold*. Mwaka jana hatukuambiwa hiyo taarifa. Taarifa hii inazungumza na imekwenda kwa hao *World Bank, IMF* na kadhalika. Inaonyesha kuna watu ambao ni vigogo ndio wanaomiliki hizo hisa huko huko ilikokwenda ile Meremeta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Julius Nyerere aliunda Kampuni ya Meremeta kusaidia kwenda katika Kampuni yetu ya Nyumbu, tutengeneze magari, leo iko kule *off shore*. Watanzania hawaelewi hata *off shore* ni nini!

Mheshimiwa Spika, tunataka maelezo ya kina. Hatutaki safari hii majibu ya kutubabaisha, tunataka maelezo ya kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mengi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, hii *e-mail* inatoka wapi? Kila kitu kiwe na chanzo kilicho bayana! Inataja mambo mazito ya ajabu ajabu na wala hutuambiwi inatoka kwa nani, unasema inatembea. Inatembea, inatoka wapi? Hatuwezi kuchukua

*document* ambayo inatembea tembea tu. Yanatembea mengi pamoja na matusi! Hebu tufafanulie! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante! Nilikuwa nalinda kwa sababu mengine niliogopa kuyataja ili tufanyie kazi. Lakini, nitataja hapa.

Kwanza, aliyezungusha *e-mail* anatumia Jina la Peter na barua pepe yake ni pjunior1980@yahoo.com. Kwa hiyo, katika *system* ya *internet* unaweza ukafuatilia ni nani. Lakini, imepelekwa kwa *J. Adams, World Bank Organization, Africa Secretariat, DFID* na kadhalika. Ni majina mengi, kwa hiyo, itanichukulia muda wangu mrefu. Lakini, inasema *"The Governer of the Bank of Tanzania, Daudi Balali,* ndio maana nimesema majina mengine naogopa hata kuyataja na ikamhusisha kwamba hapa kuna *deal* imefanyika, ndio kitu kinachonishitua na ndio maana tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie kama ni kweli Gavana wa Benki anahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli kwamba tukubali kufunga mikanda? Watanzania tufunge mikanda wakati kuna fedha zetu zinatumika, *USD 8,628* kwa s*quare metre* moja wakati Tanzania wataalamu wanasema na hapa wanasema, *the Tanzania Engineers' Board, Architects' Board and Contractors' Board* walikataa hata hizo *quotation,* lakini hawakusikilizwa. Kwa hiyo, hata vyombo vyetu vya ndani vilifanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizi ni taarifa ambazo zinatutia wasi wasi. Tungependa Waziri atueleze hii iliyoko kwenye hii taarifa ni kitu gani kimetokea, ukweli ni upi na kitu gani kimefanyika na sasa tunaweza kufanya nini!

Mheshimiwa Spika, kwenye *Foreign Debt Service Account* ambayo Waziri mwenyewe amenukuliwa na amekubali kwamba ni kweli *IMF* imetaka uchunguzi ufanyike, hili Bunge ndio kazi yake kusimamia Fedha za Tanzania. *IMF* hawakuchaguliwa na Watanzania. Wabunge sisi ndio tuliochaguliwa na Watanzania kusimamia rasilimali na mali zote zilizoko ndani ya nchi hii. Haiwezekani Wabunge tukasubiri eti *IMF* ije ifanye uchunguzi, ndio sisi tuambiwe kuhusu hela zetu ambazo zimetumika vibaya. Kuna mabilioni ya fedha yanayotajwa kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Ya kwanza, ya pili? Ya pili! Mheshimiwa Spika, nashukuru! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana! Sasa ni zamu ya Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hizi mbili; hoja ya Waziri wa Fedha na hoja ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutamka kabisa kwamba mimi naunga mkono hoja hizo. Napenda kuwapongeza sana Mawaziri hao wawili kwa kuwasilisha

hoja zao hizi kwa ufanisi mzuri na kuzifanya zieleweke vizuri na ndio maana hata michango vile vile inakuwa na nafasi ya kuweza kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia maeneo machache tu. Nitatumia muda kidogo kuzungumzia hili suala la kodi. Katika nchi yoyote ile ambayo ina utawala wa kisasa, kodi inatozwa, lazima itozwe kwa raia wake, vinginevyo hakuna huo utawala. Huo ndio msingi wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kodi ni wajibu wa kila raia mwema katika nchi yake na lazima ilipwe, hiyo tunakubaliana. Labda tunachotofautiana ni wapi itozwe na kwa kiasi gani. Labda ukichukua historia kidogo, sisi siyo wa kwanza kutoza kodi. Uingereza ilianza kutoza kodi mwaka 1799 mpaka 1816 wakati wa vita na *Napoleone,* kulipia hivyo vita. Kodi ilikuwa haipendwi wakati huo. Marekani walianza kutoza kodi mwaka 1861 hadi 1865 kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe *(Civil Wars)* na haikupendwa. Imechukua nchi hizi mbili miaka 50 raia kuweza kukubali kulipa kodi. Kwa hiyo hata ukwepaji wa kodi si wa leo, wala si wa kesho, upo na utaendelea kuwepo. Lakini, suala la kuelimisha ulipaji wa kodi, nadhani ni muhimu sana. Hilo lingefanywa kwamba raia mwema anawajibika kulipa kodi. Lakini kama alivyozungumza Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella na kodi hizo ziende kutekeleza yale ambayo ni ya manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Uingereza katika miaka hiyo 50 baada ya kufanikiwa, mwaka 1874 Waingereza walikubali kulipa kodi. Kwa hiyo, wamechukua kama jukumu na mtu akikwepa kulipa kodi, watu wanashangaa kwa nini akwepe kodi, siyo raia mwema. Marekani, mwaka 1913 ndipo kodi ya mapato ikakubalika rasmi na ikaingizwa katika Katiba. Kwa hiyo, ni jukumu la kila raia kwa mujibu wa Katiba kuwajibika kulipa kodi. Lakini, kodi hizo lazima zifanye mambo yale yanayokubalika na kwa upande wetu yanakubalika kwa sababu ni haya ndiyo yanatusaidia kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sitegemei kwamba mwana-CCM atakuwa ni wa kwanza kukataa maendeleo haya ya kodi. Mengine tunaweza kuyazungumza, lakini tupewe eneo ambalo halitakuwa na athari vile vile. Mimi nafarijika sana kwa sababu nilivyotazama jinsi kodi ilivyo, ukiangalia sehemu kubwa sasa hivi kwa mfano, katika hizi trilioni 6, trilioni 3.5 ni kodi zetu wenyewe, trilioni 2.5 ndio msaada. Mimi nadhani hatua nzuri sana. Sasa kama unataka kujitegemea na uimarishe demokrasia yako, huwezi kutegemea nchi nyingine, lazima utakwepo ugumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii mimi ninavyoiona ni kwamba inakwenda vile vile kusaidia maeneo mengine ya kuweka mazingira ambayo yanasaidia wananchi kuzalisha zaidi na kuweza kuchangia katika ulipaji wa kodi. Mimi nadhani ukiitazama kwa juu juu unaweza kusema kuna watu wanaoumia zaidi. Mimi kwenye Jimbo langu nina wakulima wa nyanya. Unapopandisha nauli, naye atapandisha bei ya nyanya, ana-*balance* hiyo. Sasa, isije ikaonekana kwamba hii kodi inambana mtu mmoja au mapato yake yanakwenda kwa mtu mmoja tu. Yule mlima vitunguu na mapeasi kule Lushoto, itabidi aongeze bei yake maana gharama ya usafirishaji imekuwa kubwa, ndio biashara inavyokwenda hivyo! *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani tunapozungumza, tusije tukaweka mahali ambapo hatusaidii wananchi kuelewa. Kwa mfano mimi nimeshangaa kusoma gazeti la leo lenye kichwa cha habari kuwa Wenyeviti wa Vyama vitatu vya siasa wanataka kuzunguka nchini kuhamasisha wananchi waielewe vibaya hoja yetu ya kodi hii. Kodi ni muhimu ilipwe, hatuna mjomba wa kutulipia sisi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TRA* inafanya kazi vizuri sana, inakusanya mapato. Lakini, ningependa kuwashauri kwamba pale ambapo kuna ukwepaji dhahiri, kwa kweli tusiugeuze kwenye mchezo wa kuigiza. Kwa mfano, juzi nilitizama mchezo mmoja wa kuigiza, mtu mmoja anapewa bei mbili, moja isiyo na risiti, nyingine yenye risiti. Ile haisaidii, mimi nadhani mtu akikamatwa apelekwe mahakamani na huyo angekuwa kielelezo kuwa huyu ameuza bila risiti ili akwepe kodi. Lile igizo linazidi kuhamasisha watu kwamba kumbe kuna uwezekano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Bumbuli hawajui kwamba kuna risiti mbili, kuna risiti yenye kodi na kuna risiti isiyokuwa na kodi. Sasa, ukiipiga hiyo sana, inatoa zaidi maarifa kwamba kumbe unaweza kukwepa. Mimi nadhani, wachukue hatua, kama kuna ukwepaji unaonekana wazi wazi, basi mtu apelekwe mahakamani. Kwa mfano, Wamachinga wanatumiwa sana kukwepa kodi, Wamachinga, ndio! Mimi siamini kwamba redio tatu, nne, tano za shilingi 60,000 kila moja, huo ni mtaji wa Mmachinga, mimi siamini na sitapenda kuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuchunguze, wanatumiwa na wafanyabiashara wakubwa kwenda kuuza mitaani bila risiti ili kukwepa kodi. Lifanyiwe kazi hili! Wamachinga wanatoka jasho la bure kuwaneemesha watu wengine wenye maduka, wakubwa hawa! Huo ni mwanya mwingine, *TRA* wachukue hatua za kuwafikisha watu hao mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kupunguzia wafanyakazi kodi. Katika nchi yetu, wanaolipa kodi kwa uhakika ni wafanyakazi. Halafu, mfumo wetu una matatizo, labda ifike wakati tuuangalie. Kwa sababu mfanyakazi hapokei mshahara wake kwanza, unakatwa kodi huko, halafu ndio anapewa kilichobaki. Lakini, mfanyabiashara, baada ya kupata mapato yake, anaondoa gharama zake, halafu kinachobaki ndio analipa kodi. Sasa, ifike wakati tumuulize na mfanyakazi naye, matumizi yako ni yapi, tuyaondoe kwanza ndio ulipe kodi. Sijui kama mmeona *logic* hii! Halafu kwenye gharama hizo za makampuni na yanayofanya biashara kubwa, zinaingiza pamoja na gharama za harusi za watoto wa Wakurugenzi, zinaingizwa kama matumizi ya Bodi za Wakurugenzi. Harusi za watoto zinaingia humo ndani. Kwa hiyo, mimi nadhani tukiangalia yote haya tunaweza kufika mahali, ukakuta kila mtu analipa kodi ile ambayo anastahili kuilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni uwezeshaji wananchi. Uwezeshaji ambao sisi kwetu una matumaini makubwa kwa watu wengi ni kwenye kilimo, uwezeshaji, mitaji pamoja na mikopo. Mikopo iliyopo inatia woga wakulima hasa wakulima wadogo kuweza kuichukua kwa sababu ya namna zao lenyewe

lilivyo. Kwa mfano mimi natoka eneo linalolima chai, nina kata 12, kata 10 zinalima zao la chai. Chai toka uipande mpaka uanze kuvuna ni miaka miwili na nusu mpaka mitatu. Je, mkopo huo utazingatia haya, kwamba sina mapato kwa miaka miwili na nusu au kwa miaka mitatu? Kwa hiyo, kama hatutalitizama hili, tutafika mahali kwa kweli tunamkuta yule ambaye tunamtegemea zaidi, hana njia ya kujiendeleza yeye mwenyewe na vile vile kuendelea na kulipa kodi ile ambayo inastahili ailipe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuieleza Serikali kwamba mimi niko katika eneo la chai na nailelewa vizuri sana. Wakulima wa chai hawana mwelekeo wowote wa kuongeza maeneo ya chai. Hawana kabisa, kwa sababu gani! Hawa wanaongozwa na wenye hisa huko nje. Ukiongeza zaidi, bei itapungua, maana yake chai itakuwa nyingi. Kwa hiyo, wanabaki hapo hapo, hakuna kuongeza. Lakini sisi tuna upungufu wa uzalishaji wa chai. Kama ikija kulimwa kwa *quarter* kwa viwango fulani, sisi tutakuwa nyuma sana.

Sasa, mimi nadhani tukajitahidi kuwawezesha hao wakulima wadogo hao waongeze ukubwa wa maeneo ya chai. Wale wakubwa kama nyie hamuamini, nendeni mkatizame kwa miaka hii 10 wameongeza eneo kiasi gani? Wamebakia pale pale ili kuhakikisha kwamba bei inazidi kuongezeka kwa kupunguza uzalishaji ambapo sisi kwa kweli uzalishaji wa chai ni uchumi wenyewe, ndio maisha ya mkulima mdogo wa chai.

Kwa hiyo, hili litazamwe na mikopo iweze kupangwa kuweza kusaidia maeneo haya ambayo yakiongeza uzalishaji yatatusaidia. Kwa mfano, tukitizama kitabu hiki cha Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, chai imekwenda ikisuasua kwa sababu kama kuna ukame, eneo ni dogo, kwa hiyo, hata mazao yanakuwa ni madogo, kwenye *table* ile ukurasa wa 95.

Mheshimiwa Spika, mimi naona niishie hapa, lakini, naunga mkono hoja hii, sisi ni Serikali, lazima Serikali ijiendeshe yenyewe! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa William Shellukindo, ahsante sana! Kabla sijamwita Mheshimiwa John Cheyo, natamka tu majina yanayofuata kwa Waheshimiwa kuweza kujiandaa.

Baada ya Mheshimiwa John Cheyo, nitamwita Mheshimiwa Hasnain Dewji, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga. Kwa hiyo wajiandae. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, naomba nifanye mambo ya utu uzima kwa kusifu Bunge hili kwa jinsi lilivyowapokea vijana wetu *Taifa Stars* na yote yale ambayo yamefanyika na hii ni kwa uongozi wako Mheshimiwa Spika. Hili ni jambo la kujivunia kwa sisi Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili la utu uzima ni kwamba wakati Mheshimiwa Celina Kombani akiwa anajibu swali hapa, amewahakikishia watu wa Bariadi kwamba Daraja la

Simiu litajengwa na fedha zipo tayari. Mimi nasema nashukuru sana kwamba Mheshimiwa Rais amekuwa muungwana kuweza kutimiza ahadi yake hiyo. *(Makofi)*

Mimi nawahakikishia kuwa tunangojea sana hilo Daraja na siyo Daraja tu, ni matumaini yangu kwamba Daraja likisha kuwa Daraja, halina maana, nategemea kwamba kutakuwa pia na barabara inayounganisha hilo Daraja ikipitia Lagangabilili mpaka ifike Bariadi na nyingine ikitoka pale Gambasingo ifike mpaka Gwamapalala. Tukifanya hivyo, ndio itakuwa tumetimiza ahadi vizuri zaidi na mimi, kama hilo daraja litamalizika, nitatoa ng'ombe wawili ili wote tuweze kusherehekea ushindi na ukombozi mpya katika Wilaya ya Bariadi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bajeti, nitachukua tu mfano wa Bariadi. Mimi nilikuwa na matumaini makubwa sana baada ya kuona mambo yaliyotokea kwa mwaka uliopita kwamba Bajeti hii ingeweza kuleta unafuu kwa watu wangu wale walionituma hapa hususan kwa mambo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka ambao unamalizika sasa, Bariadi tumejenga *Secondary Schools 28* mpya ukilinganisha na *Secondary Schools* 12 ambazo zilizokuwepo mwaka 2005. Lakini, hizi *Secondary Schools* tumezijenga kwa kuwachangisha watu kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, wengine wamechukuliwa sufuria zao za chakula, wengine wamechukuliwa baiskeli zao, wengine wamewekwa ndani, yaani ni ghasia za kila aina. Kwa hiyo, ndio kusema watu wamejenga hizi shule siyo kwa mchango wa hiari, ni kwa kiboko, ni kwa lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilichokuwa nategemea kwenye Bajeti hii, ni kwamba ningepata unafuu nitakaporudi kule Bariadi niwaambie sasa wananchi ahueni, sasa afadhali Bajeti hii imeleta kwamba kutakuwa na madarasa yatakayojengwa na Serikali na Serikali itatuunga mkono. Nitaeleza baadae, sijaona hili katika Bajeti hii ambayo sasa hivi tunaizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia nilikuwa nategemea kwa kuwa Bariadi tunapata mazao makubwa sana kwa mfano Pamba ambayo inaleta *Foregn Exchange,* kwamba sasa Bajeti hii ingeweza kuniambia, Ng'wasuale itaunganishwa kwa barabara na Bariadi. Ningeambiwa kwamba Mahembe sasa tutaweza kupita hata wakati wa masika, na sehemu zingine. Hakuna barabara za vijijini, nimeangalia katika Bajeti hii na nitaeleza hapo baadae kwamba sioni chochote ambacho tunampa mkulima. Bajeti imekuwa kwamba tunatoza kodi nyingi, tunatoza kodi ya mafuta ya taa. Sasa na wewe chukua hii, sioni katika Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeangalia pia upande wa Bariadi na wengine wataangalia wenyewe. Ni afadhali kidogo hapa kwenye maji. Halafu pia nimeangalia kwenye afya, bado namba kama kwa Bariadi haziridhishi. Kilimo hivyo hivyo! Sisi ni wakulima wa Pamba, nilikuwa nategemea mwaka huu na bado hapa nitalizungumza hili zaidi kama nikipata nafasi kwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Lakini, haiwezekani kwamba wengine wakawa watazamaji na wengine wakawa wanafaidika na kodi.

Hatuwezi kukubali kwamba Mikoa ambayo inalima sijui mahindi iwe inapata ruzuku ya dawa na sisi ambao tunalima Pamba inayoleta *Foreign Exchange,* hatupati chochote. Tunataka wakulima washikwe mkono kwa shilingi 15 kwa kila kilo wanayotoa kwa ajili ya pembejeo, angalu na Serikali iseme tutatoa shilingi 5 na wenyewe wakatoa shilingi 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo itakuwa angalau Serikali imeonyesha kwamba imepandisha kodi hapa, tumefanya hivi na wewe shika angalau shilingi 5 kwa kilo ili kuweza kuwa kama mchango kwa ajili ya pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali halisi ambayo ninaiona sasa kwamba kama tutaendelea na mtindo huu wa kuvichangisha wananchi kwa bei ambazo zinapita hata bei za Pamba, hali hii haiwezi ikakubalika. Kwa mfano, mwaka jana tumepata kama kilo milioni 40 za Pamba ambazo ni karibu shilingi bilioni 12 kwa bei ya shilingi 300 kwa kilo. Mwaka juzi tumepata kama milioni 80 ambayo ni sawa sawa na shilingi bilioni 24 kwa bei ya shilingi 300 kwa kilo. Lakini tumechanga zaidi ya bilioni 7 kwa ajili ya *Secondary Schools*. Sasa shilingi bilioni 7 kwa ajili ya shule ni asilimia 30 kwa mapato ya mwaka 2005 na ni asilimia karibu nusu kwa sababu bei ya Pamba ilikuwa imeteremka chini. Hali hii hairuhusiwi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kwamba maana ya Bajeti ni kugawana mzigo kidogo kidogo. Tungependa kufika Bariadi ambapo kama tunaamua kwamba kama tunachangia *Secondary Schools*, basi Serikali ihakikishe kuwa angalau mtu anayepata dola moja kwa siku, hachangii zaidi ya shilingi 5 kwa mwaka mzima. Kama shilingi 5 haitoshi, vingine visubiri. Lakini mimi naona kama Bariadi tuko watu zaidi ya 300,000 ambao tunaweza kutoa kodi shilingi bilioni 1.5, mimi naona inatosha kabisa kuweza kufanya maendeleo katika sehemu yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nasema hatujapata chochote ambacho tunaona kinaweza kusaidia Bariadi na sioni kwa nini basi nisimame hapa kwa nguvu zote niseme kwamba, mimi naunga mkono Bajeti hii. Nitawaambia nini watu wa Bariadi kama mambo yote haya niliyoweza kuorodhesha hapa, siyaoni ndani ya Bajeti hii? Hilo la kwanza! Daraja, litatuwezesha tu kidogo! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naona sishangai kwa nini hatuwapi watu wa kawaida chochote. Muundo wa Bajeti yetu, kusema kweli ni wa ajabu sana! Nimeangalia tu kwa takwimu, kwa mfano nikichukua upande wa Sekta ya Elimu kwamba Bajeti imetoa trilioni moja. Lakini ukiangalia katika miradi ya maendeleo ambapo ndio ningekuta kwamba tutajenga madarasa kadhaa ya *Secondary Schools*. Nimekuta la kujenga pale ni kwamba tutafuatilia kujenga madarasa 10,000, tutafuatilia kujenga nyumba za walimu 800, tutafuatilia. Sijaona kauli ya Serikali ya kusema kwamba tutajenga na hela ziPo hapa! Ukiangalia zile takwimu utaona kwamba kumetolewa shilingi trilioni moja, miradi ni shilingi bilioni 110 tu ambayo ni asilimia 10. Kwa hiyo, ndio maana hakuna chochote ambacho tunawapelekea wananchi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Kilimo, zimetengwa shilingi bilioni 379, miradi ambayo imeandikwa humu ni shilingi bilioni 60 tu, asilimia 15. Afadhali Maji, sijui Waziri ni nani kule! Afadhali ya Maji kumetengwa shilingi bilioni 309, angalau miradi ni 224 ambayo ni asilimia 72 ya fedha hizo, afadhali. Zimetengwa kwa Afya, shilingi bilioni 589, 180 ndio miradi iliyoorodheshwa hapa ambayo ni asilimia 30. Zimetengwa kwa Miundombinu shilingi bilioni 773, miradi ni bilioni 378 ambayo ni sawa sawa na asilimia 48. Kwa *sample* hii tu wengine mtaangalia ninyi wenyewe. Sioni basi ni kitu gani haya mabilioni yanayotajwa yanakwenmda wapi, kama hayaendi katika miradi ambayo tunaweza kuiona?

Mheshimiwa Spika, mimi nasema, kama tutaendelea na utaratibu huu, tunawaambia wananchi tunapandisha mafuta ya taa, tunapandisha petroli, tunapandisha sijui, daladala, tunapandisha kila kitu, lakini hawapati chochote ambacho wanaweza kukiona.

Mimi nina hakika Serikali iliyochaguliwa kwa ajili ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania pamoja na mimi na pamoja na Watanzania ambao wako nyuma, kwa hali ya namna hii, maneno hayo hayana *support* ya *figures* za Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri ni lazima. Sasa nitatoa ushauri, tatizo ni nini! Kwanza, mimi naona tatizo katika upangaji wote wa Bajeti hii, Wazungu wanasema, *It is ambition without resource.* Wewe una ari, lakini huna pesa ya ku-*support* ari yako. Sasa hali ya namna hii ndiyo imetufanya sisi Kambi ya Upinzani angalau tuwaamshe, jamani angalieni hapa! Hapa labda tunaweza tukapata chochote. Zamani mlikuwa mnatuambia ninyi mnasema tu tuletee hiki, tuletee hiki. Zamani mlikuwa mnatuambia ninyi mnatuambia tu *wishes wishes* tu, mnasema tu tuletee tuletee hiki. Mimi nina hakika kuna haja ya Serikali hii kufikiri tena namna tunavyofanya Bajeti yetu. Mimi naona huu utaratibu wa miaka hadi miaka, mimi naona ni kama vile *copy and paste,* basi. Kwa hali kama hii hatuwezi. *We have a revolutional President,* lakini *we have a Conservative System* ya kutengeneza utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali kama hii, hatuwezi tukafika. Kama sasa hivi tuna-*constrain* wafanyakazi, hebu mimi nashauri kwamba labda tutengeneze ofisi maalumu na hii Ofisi iwe *an Independent Office* kwa ajili ya Bajeti. Bajeti siyo chama, Bajeti ni yetu sisi wote. Unapopewa ushindi na wananchi, wanakuambia nenda ukashirikiane kisheria. *This is a Legal Matter,* ndani ya *Constituon* ndio Bunge hili tumepewa Mamlaka ya kuweza kuiangalia Serikali. Lakini, kuangalia Serikali *it is a Budgetary Oversight*, maana yake hapa ndio tumefika tunapozungumza haya mambo. Sasa mimi nasema kama kuna *constraints* juu ya watu ndani ya Serikali kwa ajili ya *Budgeting,* mimi nashauri labda tutengeneze *Budget Office* iliyo *Independent, Commissioner* aliye *Independent.* Sasa hivi naona *pressure* ya wanasiasa ni nyingi mno. Kila ukitengeneza hivi, *profession* wanasema hapana, nataka iwe hapa. Hali ya namna hii ndio tunajiweka mahali ambapo hatufiki popote.

Mheshimiwa Spika, la pili, kama tukitengeneza Bajeti, ni lazima iwe Bajeti iheshimike. Leo hapa tutatumia hela za wananchi zaidi ya miezi mitatu tuko hapa wote

tunapiga maneno, na mimi ni mmojawapo. Sasa, baada ya kupiga maneno hapa, tunakuja kusikia tena ripoti kutoka kwa Waziri wa Fedha kwamba mimi mlinipa madaraka ya kuweza kuhamisha fedha, leo nimehamisha hapa, nimehamisha hapa. Ulituweka hapa kufanya nini kama tuna Bajeti ambayo inaweza ikahamishwa hamishwa jinsi mtu ambavyo anaona kama inafaa. *We need to have a budget* ambayo ni *performong.* Mimi naona Bajeti iliyopo sasa, tuna matatizo kwa sababu muundo na taswira juu ya Bajeti haijawa sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu ni tegemezi. Utegemezi huu kusema kweli lazima nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wafadhili wa nchi hii na hawa wafadhili hata leo wamenipa fursa ya kuweza kuzungumza na Mabalozi ambao wamekuja hapa kama alivyosema Mheshimiwa Spika. Kweli, kwa mtindo uliopo sasa ambapo ukiangalia hata ile *trend,* watu wanaotoa *Basket Fund*, watu wanaotoa *direct to projects* na watu wanaotupa katika *General Budget Support,* kusema kweli pesa imekuwa nyingi ya wafadhili na inakuja. Lakini, zaidi nawasifu wale ambao wanatuamini kiasi cha kwamba wewe chukua hizi fedha nenda ukatumie. Mimi naona Bunge hili limepewa jukumu kubwa sana, limeaminiwa sana kwamba tukiwapa Watanzania fedha bila kuwafuata fuata kwa njia ya *Budget Support*, Miradi yao ni *predictable*. Kwa hiyo, fedha zake zinajulikana, ziko wapi na zinakuja *on time* kwamba hawa wataziangalia hizo *time.* Hili nataka kutoa hapa kazio kwamba Bunge hili sasa hivi lazima liamke. Bunge hili sasa hivi lianze ku-*demand accountability* kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuhakikishe kwamba Serikali inawajibika ipasavyo kwa fedha ambayo sisi tunatoa ambayo *domestic revenue* na kwa fedha ambayo inatolewa na wafadhili. Wafadhili kukupa hela tu halafu na kuachia kusema kweli ni jambo ambalo ni la kujisifu. Lakini wewe unapewa hizi fedha halafu kesho unapata *CAG Report* hatukuweza ku-*reconcile* kati ya mikopo na sijui mapato. Hali kama hii inadhalilisha Taifa letu. Unapoambiwa leo *CAG Report* inasema kuna ubadhilifu hapa na haya mimi nayaona kama Mwenyekiti wa *PAC* hali hii inawafanya wafadhili wasituamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii siwezi kutamka kwamba naunga mkono Bajeti hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo. Sahihisho kidogo hapa baada ya Mheshimiwa Hasnain Dewji nilikuwa naomba radhi nimuwezeshe Mheshimiwa Ahmed Shabiby kama nilivyotangaza asubuhi mama yake ni mgonjwa sana pale Gairo na inabidi kuondoka asubuhi. Kwa hiyo, nikivuta muda tunaweza kufika muda ambao asichangie. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Dewji atakuja Mheshimiwa Ahmed Shabiby na ndiyo tutaendelea sasa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja hizi mbili zilizokuwepo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nawapongeza Timu ya Taifa kwa kufanya vizuri sana na kupata ushindi na nawaombea ushindi dhidi ya timu ya Msumbiji

wataupata *Inshallah.* Vile vile nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kilwa Kusini kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili nikiwa ni mwakilishi wao nawaambia nitawawakilisha vizuri sana hapa Bungeni. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nataka niunge mkono hoja hii mia kwa mia kwani haina matatizo. Mimi nina maswali mawili, matatu ya kuzungumzia. Kwanza nataka niipongeze Wizara kwa kuwa na *Cash Management Unit Budget*. Hii itasaidia sana katika kupunguza riba. Ninavyoiona mimi itakuja na itasaidia sana katika kupunguza riba nchini ambazo mabenki yetu yanatoza riba kubwa na wanakuwa na kauli ya kusema kwamba *risk free* kuwekeza kwenye *treasury bill* ni *risk free*.

Sasa hivi kwa kuwa Serikali haitatilia mkazo sana kwenye *treasury bills* za *bonds,* zile fedha katika mabenki yetu tutakuwa na fedha nyingi ambazo watu wengi wanaweza kukopa hizo fedha. Mzunguko wa fedha utakuwa mkubwa na biashara zitazidi kushamiri. Watu wa benki hawawezi kuweka fedha ndani ya benki zisifanye kazi, itabidi iwakopeshe. Tuna matatizo makubwa katika uwekezaji. Tupo sisi wawekezaji wa ndani na wako wawekezaji wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hili wale wawekezaji wa nje wanakuja na fedha kutoka nje takribani asilimia 4 au 5 ya *interest rate* wanatozwa kule kwao, huyu wa ndani anatozwa asilimia 20 au zaidi. Hii inakuwa kama timu moja inacheza pekupeku na timu nyingine ina viatu. Sisi wa ndani hatuwezi kucheza vizuri, nchi hii haiwezi kuendelea hata kidogo kama tutafanya hivyo. Wenzetu wanapata ahueni, wanapata *interest rate* ndogo huko kwao wanakuja kuwekeza huku. Sisi wa ndani tunakuwa hatuwezi kuwa kwenye *fair competition* na wao. Kwa kuwa Wizara imeliona hili kutokubali *treasury bills* hizi mimi naishukuru sana, naipongeza sana Wizara kwa kulifanya hili hata zile riba kubwa ambazo Serikali inalipa itakuwa ahueni na kipato cha Serikali kwa namna nyingine kitaongezeka hapa.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka nichangie hapa ni kuhusu jimboni kwangu. Kilwa kuna hazina kubwa ya *gypsum*. Hizi ni malighafi ambazo zinakwenda kwenye viwanda vya saruji. Cha kushangaza Kampuni ya *Wazo Hill* inaagiza *Gypsum* kutoka nje. Mwaka jana mwezi Novemba, *Gypsum* tani 40,000 zilikuja zenye thamani ya dola milioni 4.8 za Kimarekani na mwaka huu wana mpango wa kuagiza tani 20,000 zenye thamani ya dola milioni 2.4 jumla ni milioni 7.4 fedha za kigeni. Hapa Waziri ametuambia Serikali inatafuta fedha za kigeni kwa nguvu, lazima tuwe na fedha za kutuwezesha kwa miezi mitano. *Gypsum* ya Kilwa ina ubora, ina *standard,* ina *calcium contents* ambazo ni 95% mpaka 103%. Ile iliyoagizwa ina *contents* iliyoagizwa, ina *contents 75 to 78%* bado *gypsum* yetu ni mali na ni bora. Hiyo hiyo kampuni ilikuwa inanunua kwa muda huu wote, *gypsum* ya Kilwa ilikuwa inanunuliwa, cha kushangaza tu hapa katikati wamekuja hawapati kununua *gypsum* ya kwetu. Wananchi wangu wanapata taabu, migodi yote imesimama tuna tatizo kabisa hapo tunaharibu hela zetu za kigeni, tunazi-*support* kampuni za nje, hatujui hiyo kampuni ya wazo inahusiana na kampuni mama gani ya nje, kwa nini fedha hizi zinatoka hapa nchini kwenda kununulia malighafi na mali sisi tunazo. *(Makofi)*

Nataka niliongelee hili linaniuma kabisa dola milioni 7 ni hela nyingi sana. Utafiti umefanywa, *gypsum* ina ubora mzuri sana, kwa nini wawekezaji wasitumie asilimia 80 ya malighafi iliyopo ndani ya nchi? Hili kwa kuwa limegusa, nimeona niliongelee hapa kwa sababu wananchi wangu linawakosesha ajira, Serikali inawatumia fedha nyingi sana za kigeni kutokana na tatizo hili. Naiomba Serikali iangalie kwa makini kwa tatizo hili kwa nini tunaruhusu kampuni hizi kubwa  kuagiza malighafi ambayo iko hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu nataka niongelee kuhusu Songosongo. Songosongo ni kisiwa kidogo ambacho kina hazina kubwa ya gesi asilia. Gesi hii ilikuwa ni mkombozi kwa nchi nzima kwa mwaka jana wakati tulikuwa na tatizo la ukame, Songosongo imeikomboa nchi nzima kwa kutumia gesi yake lakini tuna matatizo na wawekezaji wa Songosongo. Nataka niliongelee hili ili Wizara itambue. Nalifanyia kazi na nimelivalia njuga sasa hivi yapata mwaka mmoja na nusu. Tumekaa Halmashauri tumepanga, tumewaandikia kwamba watuwezeshe kwenye fedha za *development level*. Tumewaandikia wametujibu jibu siyo zuri la mkato, *we are not entitled to pay any tax in this country*.

Mheshimiwa Spika, majibu hayo yamenishangaza sana kama wao wana Mkataba na Serikali lakini sisi tuna mambo yetu pale, tuna sheria zetu pale Kilwa, tumezipanga sheria kwa kuwa hali zetu siyo nzuri, Songosongo ni kisiwa hakioti kitu pale, samaki sasa hivi hawapo wako bahari kuu, wako mbali, wananchi taabani, tuna wakazi 5,000 kaya karibu 600 ziko hoi bin taabani, wanaona uwekezaji uko pale, mwekezaji bilioni 2 za sekondari zimetutoa jasho kuziomba tu hizo. Hatuna uhusiano mzuri kabisa na wawekezaji, hili naomba niliongelee, siwapuuzi wawekezaji wengine lakini mimi mwekezaji wangu nina taabu naye kabisa. Hakuna uhusiano wowote hata kuombana chumvi pale Songosongo jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kengele ya pili ilie nasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuendelea. Kwanza kabisa napenda kuzipongeza hotuba zote mbili za Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na hotuba ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua lengo la hotuba ya Bajeti ni kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi unapanda na tunatekeleza yale yote ambayo yamo katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ambacho kwa sasa hivi ndiyo kinachoongoza nchi.

Lakini mimi kwa upande wangu hakuna kitu cha kupinga isipokuwa ni katika kutoa ushauri. Hasa nikianzia katika upande wa ushuru magari *(Road license)*. Samahani kwanza napenda kuzungumza kwamba mimi ni mdau kwa upande wa mafuta na magari. Kwa upande wa *Road License* napenda kuzungumzia hapa penye *cc*  kuanzia *cc 1500* kushuka chini kuwa ni shilingi 80,000 na kuanzia *cc 1500* kwenda *cc 5,000* ni shilingi 230,000 hapa kwa vyovyote vile tunaweka mianya ya kukwepa ushuru. Kuna gari watu wananunua shilingi 00,000 zipo mitaani kwa ajili ya kujisogeza lakini zina *cc 1600, cc 1800.* Leo tena akaongeze kulipa *Road License* shilingi 230,000.

Kwa mfano, pale kama jimboni kwangu sasa hivi pamoja na kuwa ni tarafa lakini ina *tax* kama 30 hivi. Lakini nina imani kabisa kama watawekewa alipe shilingi 230,000 lazima atakuwa tu anakwepa. Kwa hiyo, siku *TRA* akitoka Kilosa Wilayani mpaka aje afike pale jimboni ni kilomita 180 anaficha ile gari. Siku akitoka gari inatolewa. Kwa hiyo, watu wataendelea kukwepa. Kwa hiyo, hili lengo la kukusanya hizi fedha nina wasiwasi kwamba halitatimia.

Mimi ushauri wangu labda kuanzia *cc 2000* kuja chini ambazo ndiyo *balloon* na hizi *Mark II* ndogo ndogo kwa sababu *balloon* ina *cc 1600* na *cc 1800* sasa ukiiwekea kiwango cha shilingi 230,000 ni kikubwa mno. Kwa hiyo, labda kwa ushauri wangu itoke *cc 2000* kuja chini ziwe shilingi 80,000 na kuanzia *cc 2000* kwenda *cc 5000* hata ikiwa shilingi 230,000 inakuwa siyo mbaya. Halafu kwa upande wa mafuta hapa lipo tatizo kubwa sana na hili tatizo halijaanza leo liko siku nyingi sana na linafahamika hata ukimwuliza mtu yeyote mwenye *petrol station* Tanzania hii hili tatizo analifahamu. Sasa kwa mfano dizeli sasa hivi itakuwa ushuru wake ukichanga *excise duty* na *lottery* itakuwa 512, *petrol* itakuwa shilingi 515 kwa hiyo ukitoa tofauti ya *diesel* na mafuta ya taa ambayo ukitoa 512 ukitoa ushuru wa mafuta ya taa shilingi 56 utapata hapa ni shilingi 456 tofauti ya *diesel* na *kerosene*.

Sasa hivi Mkoa wa Pwani kuna vituo kila kona na viko porini na vyote nyuma vina magodauni na yale magodauni yana matanki ya kutosha laki mbili, laki tatu mpaka laki sita. Gari zote Tanzania haiwezi ikaenda nchi yeyote au Mkoa wowote bila kupita Mkoa wa Pwani. Kwani *semi trailer* imepakia lita 35,000 zinatolewa lita 7,000 za dizeli inawekwa mafuta ya taa lita 7,000 inaitwa chakachua hii. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kwa siku moja maana yake akishatoa ile dizeli akiweka mafuta ya taa ina maana tayari mafuta ya taa yameshafanywa malighafi na tayari ameshakwepa ushuru wa dizeli kwa sababu badala ya dizeli amefanya mafuta ya taa kuwa dizeli na karibu vituo vyote vile ni vingi ni vichache sana ambavyo havifanyi hiyo kazi. Sasa tukitaka tulete mafuta Dodoma lazima uwe na gari nyingine ndogo ilifate lile lori tena kwa simu mpaka ifike ukizubaa kidogo tu ukiona hupati simu lazima utume ndugu yangu mwingine Dar es Salaam asogee aangalie vipi hapo. *(Makofi)*

Sasa kwa siku moja Dar es Salaam zinapakiwa zaidi ya lita milioni moja na chakachua inayofanywa pale kuchanganya wanaiba zaidi ya lita 300,000 kwenda mbele. Sasa tufanye tu *maximum* ya lita 250,000 wakiiba kwa siku lita 250,000 ya mafuta ya taa ukifanya iwe dizeli kwa ushuru wa shilingi 456 ambayo ni tofauti na mafuta ya taa hapa kwa siku moja *TRA* inapoteza shilingi 114,000,000 kwa siku na kwa mwezi inapoteza shilingi 3,420,000,000 kwa na mwaka inapoteza shilingi bilioni 41 hiyo baki ya wale wenye vituo ambao siyo waaminifu ambao wanaweza wakachukua mafuta ya taa tena wakachanganya kwenye vituo hiyo tofauti. *(Makofi)*

Tukumbuke kwamba mafuta ya taa kwa kweli hayakupanda sana ushuru ni shilingi 4 tu pamoja na kuwa wenzetu wengi waliotangulia wanalalamika lakini bado. Lakini mimi wasiwasi wangu ni kwamba tofauti kubwa ya mafuta ya taa na dizeli

isipoangaliwa na *TRA* wasipofanya mipango ya kushughulikia wao wenyewe kwa kutegemea kwamba kuna vyombo vingine vinawasaidia, watakuwa wanakosesha mapato Serikali.

Kwa hiyo, mimi nafikiri tofauti ya mafuta ya taa na dizeli na petroli kama isipoangaliwa kwa makini na isiposimamiwa badala ya kuwa inasaidia wananchi wadogo bado itatumika kama kuwa malighafi kwa ajili ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ushauri wangu sitaki kupoteza muda kwa sababu suala hili linafahamika siku nyingi na lipo muda mrefu katika Mkoa wa Pwani kwa kubadilisha mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa. Kwa hiyo, naomba vyombo husika viliangalie kwa makini ili kuondoa usumbufu na uharibifu kwa magari pamoja na kutokwepa ushuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia hoja ya Bajeti ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabla sijaendelea kuchangia hoja hii naomba niseme naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukubaliane kwamba Bajeti hii ina mambo matatu muhimu. Katika hizi hoja, kuna hoja ya Serikali ambayo wanaitetea kwa maana ya vigezo walivyoweka kwa ajili ya Bajeti ya mwaka 2007/2008. Hoja ya pili ni hoja ya Kambi ya Upinzani ambayo na wao watapinga Bajeti hii kwa vigezo walivyokuwa navyo. Lakini hoja ya tatu ni wananchi wenyewe ambao sisi wananchi tunawasemea hapa na kuwatetea. Lakini tukubali vile vile kwamba wananchi wana haki katika mambo yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwananchi anataka barabara nzuri ni haki yake, mwananchi anataka mtoto wake akasome ni haki yake, mwananchi anataka apate matibabu mazuri ni haki yake, mwananchi anahitaji vitu vyote ambayo vitamwezesha yeye kuishi maisha mazuri, ni hizi zote ni gharama ambazo kwamba Serikali inabidi izitafute na kuanza kuzitumia kwa ajili ya maslahi yao. *(Makofi)*

Lakini tukubaliane pamoja na wananchi kwamba na sisi kama wananchi tuna haki vile vile na tuna wajibu wa kusaidia mapato ya nchi hii yainuke. Niwaombe tu wananchi wafanye jambo moja kubwa tu ambalo litaiwezesha Serikali kukosa mapato yake. Wananchi wawe na utaratibu wa kununua bidhaa zote ambazo zinazalishwa hapa Tanzania kwa kitendo hicho tu peke yake kitaongeza mapato ya nchi hii. Lakini tukiwa na utaratibu wa kununua bidhaa nyingine ambazo zinatoka nje ya nchi pamoja na kwamba zina kodi kubwa bado hatusaidii mapato ya nchi hii. Kwa hilo dogo tu la wananchi kununua bidhaa zinazotengenezwa katika nchi hii zitaisaidia kuongeza mapato ya nchi hii kwa maana ya viwanda vyetu vitaongeza uzalishaji na hatimaye kodi zaidi zitalipwa Serikalini na hatimaye kodi zile zitarudi tena kwa wananchi kuwasaidia mambo yote ambayo wao wana haki ya kuwa nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa Serikali inazungumzia utaratibu mzima wa jinsi ya kupata mapato ili yaweze kutumiwa katika Serikali kwa manufaa yao wananchi wenyewe. Lakini kubwa ambalo limechukua kipaumbele kwa wananchi ni bei ya mafuta kama ilivyoongelewa na walitangulia kusema. Kitakachomuhusu mwananchi wa chini ni mafuta ni sawa na mwenzangu aliyetangulia alisema kwamba bei ya mafuta ya taa haikupanda sana ni shilingi 4 na mimi niseme *advantage* na *disadvantage* ya mafuta ya taa katika ushuru pamoja na kwamba ushuru wa mafuta ya taa umeongezeka kwa shilingi 4, wasiwasi mkubwa wa Serikali wa kupunguza bei ya mafuta ya taa ni kama alivyozungumza Mheshimiwa Ahmed Shabiby ni suala zima la kuchanganya mafuta ya taa na mafuta ya dizeli na petroli. *(Makofi)*

Lakini sasa tukubaliane kila mmoja abebe mzigo wake. Serikali ina vyombo vya kusimamia shughuli kama hizi za kudhibiti uhalibifu huu unaojitokeza wa kukwepa kodi katika ushuru wa mafuta. Serikali isimamie basi kwa kudhibiti uchanganyaji wa mafuta ya taa na bidhaa nyingine za mafuta ya petroli na dizeli ndiyo kazi yao. Hivi ni kitu gani itakachoweza kushindwa Serikali kama iko *serious* kweli kweli kusimamia uchanganyaji wa mafuta ya taa na petroli na dizeli kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanaofanya biashara ili kukwepa kodi wasiweze kufanya hivyo? Hiyo ni kazi ya Serikali, haina mjadala kwamba lazima wasimamie suala hilo maana ndiyo kazi ambayo Serikali inayo na vyombo vyote wanavyo na sheria tumepitisha na adhabu tumezipitisha hapa kwa hakika wanatakiwa wasimamie hilo. Lakini vile vile basi tumsaidie mwananchi tunaposema kwamba mwananchi aamue nishati mbadala kwa lengo la kwamba hatuharibu mazingira tumpe *option* aone kwamba nikitumia mafuta ya taa mimi nitaachana na kuni. Nikitumia mafuta ya taa nitaachana na mkaa. Lazima tumpe nafasi hiyo ya *option*. Lakini mafuta ya taa haya ambayo yamepanda kwa shilingi 4 yatakapomfikia mlaji yatapanda zaidi ya shilingi 4 kwa sababu ya gharama ya usafiri kwa kupanda dizeli na petroli. *(Makofi)*

Sasa hii ni *logic* inaeleweka, lakini mimi naishauri Serikali, lengo Serikali inataka ipate kodi yake, sasa tunafanyaje, mimi niishauri Serikali nafahamu kwamba mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayoagizwa hapa nchini kwa mwezi ni tani 120,000 matumizi ya mafuta ya taa ni asilimia 12 mpaka asilimia 16. Kwa maana hiyo mafuta ya taa yanayoingizwa hapa nchini kwa matumizi ya kila mwezi ni kati ya tani 15,000 na tani 20,000 wastani. Hii Serikali inategemea kupata kwa tani 15,000 ni shilingi milioni 810 mpaka bilioni 1.1 ndio mategemeo ya Serikali kwa kila mwezi tuweke wastani wa kati ya shilingi bilioni moja kutoka kwenye mafuta ya taa peke yake kwa maana ya kwamba matumizi ya mafuta ya taa ni kati ya tani 12 mpaka 16. *(Makofi)*

Lakini mimi niseme Serikali ipunguze bei ya mafuta ya taa. Kama hoja yake ni kwamba ipate ushuru wakipunguza bei ya mafuta ya taa, ina maana mafuta ya taa yatanunuliwa kwa wingi na wananchi ili wapate nishati mbadala waachane na kuni, waachane na mkaa kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, watumie mafuta ya taa kwa vile ni bei rahisi. Ikishakuwa bei ya mafuta ya taa ni rahisi wingi wa mafuta ya taa utatumika kwa maana ya *volume* ya mafuta ya taa yataongezeka. Lakini itakuja kufidiwa na kodi ambayo itashushwa *volume* itazidi mara mbili au mara tatu kwa hiyo, itafidia kodi ile ile ya shilingi 56 tukiipunguza kwa shilingi labda 20 *volume* itaongezeka lakini na kodi

itakayokusanywa ni ndogo lakini volume ni kubwa hatimaye watafika pale pale kwa ile kodi ambayo wameikadiria Serikali kuipata kwa mafuta ya taa kwa bei ya shilingi 54 au 56.

Sasa mimi niiombe Serikali punguzeni bei ya mafuta ya taa, *demand* ya mafuta ya taa itakuwa kubwa. Ikiongezeka *volume,* ushuru utaongezeka kwa kiwango kidogo kidogo na itapita kile kiwango ambacho Serikali wamepanga hiyo ni njia mojawapo ya kuwasaidia wananchi katika masuala mazima ya nishati. Tunajua mafuta ya taa yanavyowagusa wananchi moja kwa moja mpaka vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi najaribu kuishauri Serikali suala zima la kutafuta mapato mengine bila ya kuwaumiza wananchi katika mapato mengine. Tulitoa ushauri hapa Bungeni jinsi gani ya kuongeza mapato, pamoja na kwamba Serikali imeona kwamba labda wakati siyo muafaka, lakini nasema hakuna wakati muafaka wa kukusanya kodi, wakati sababu za kukusanya kodi zile zipo.

Mheshimiwa Spika, tulishauri hapa kwamba sasa magari yanayoingia nchini tutumie utaratibu wa *cc capacity* ya injini, wameweka katika vigezo vya *road lisense*. Lakini kwa nini wasiweke kwenye magari, kwa sababu tukiweka hii katika utaratibu wa magari ni urahisi wa kupata kodi haraka, kwa sababu hakuna mwananchi anayetaka gari yake ikae bandarini kwa siku nyingi, wataingiza gari zao kwa haraka, gari inafika nchini amekwishajua kodi atakayolipa. Kwa hiyo, Serikali itakuwa na mapato ya kila kwa maana ya urasimu kupungua katika kuingiza magari.

Vile vile tulishauri kwamba ukaguzi wa magari unaofanywa nje, unaitia hasara Serikali. Tukasema kwa nini *inspection* isifanywe hapa nchini. Lakini vile vile kwa utaratibu mwingine wa kukusanya mapato ni lazima sasa kila mwaka magari yakaguliwe. Katika kukaguliwa magari kwa utaratibu wa kitaalamu kama zile zinazoingia nchini kwa kuweka mitambo ya kukagua magari, Serikali itakuwa inaongeza mapato kila mwaka kwa magari yote ambayo yanakaguliwa hapa nchini kwa ajili ya wewe kuweza kupata *road lisense.* Hupati *road license* mpaka gari yako ikaguliwe na ukikagua gari yako kuna gharama ambazo ni lazima ulipie, hayo ni mapato ambayo yataingia Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tushukuru vile vile kwamba sasa tumekuwa siyo tegemezi sana kwa Bajeti yetu kutoka asilimia 50 mpaka sasa hivi tumefikia asilimia 39. Tuipongeze Serikali kwa hatua hiyo ambayo imefikia. *(Makofi)*

Lakini suala la kutafuta vyanzo vingine vya mapato ni lazima *TRA* na wataalamu wengine waumize vichwa hatimaye kuhakikisha kwamba ziko kodi nyingi ambazo bado hazikusanywi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima sasa la MKUKUTA na MKURABITA ambayo Bajeti imeizungumzia. Lakini tukubaliane pesa nyingi sasa hivi za Bajeti zinakwenda katika Halmashauri za Wilaya, *concern* yetu kubwa ni utaratibu wa kusimamia hizi fedha zinazokwenda Wilayani kwamba hatuna wataalamu wa kutosha kuweza kusimamia fedha nyingi kama hizi. Panapotokea uharibifu wa hizi fedha

tunaiomba Serikali tunapowabaini wale Watendaji ambao ni wabadhirifu, isiwe sasa utaratibu huku Serikali huku juu wanaanza kuwalinda kwa sababu huyu ni mjomba wake, huyu ni shangazi yake au huyu ni rafiki yake na kuanza kupeleka zawadi huku juu Wizarani kwa sababu asiweze kuchukuliwa hatua. Hii inatusumbua na tunashindwa kabisa kuelewa kwa nini Serikali haichukui hatua wakati imethibitika kwamba huyu amefanya ubadhirifu wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunajenga Sekondari, wakati tunajenga shule za msingi mabati yanaibiwa, nondo zinaibiwa na ushahidi unapatikana, watu wanasimamishwa, lakini hakuna hatua za kuchukuliwa kwamba huyu amefanya kosa, tunatafuta ushahidi kwamba wapi ameiba, wakati yeye ndiye Mkuu wa Idara nani tumkamate. Yeye ndiyo awajibike kwanza lakini huku juu tafadhalini sana msiwalinde kama hawa ili kunusuru fedha hizi nyingi za Bajeti zinazokwenda katika Halmashauri ziweze kufanya kazi yake kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka kusema kwamba Bajeti hii katika mfumuko wa bei, kwa safari hii kwa vile tumepata mvua za kutosha, bei ya chakula itapungua lakini bado nasema kuna bidhaa ambazo siyo za chakula bado mfumuko wake wa bei ni mkubwa na hilo litachangia zaidi kupanda kwa sababu ya bei ya mafuta. Serikali itafute njia mbadala ya kuweza kuwanusuru hawa watu wa chini na narudia wale wa chini wapate nishati mbadala. Hiyo ndiyo hoja yangu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nakushukuru kwa kunipa nafasi na niseme tena naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008. Awali ya yote vile vile niwashukuru wananchi wa Jimbo la Tabora ambao wameniwezesha kuwa mwakilishi wao katika Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja katika uchangiaji. Hoja yangu ya kwanza ni kwamba nchi yetu inanunua sana kuliko inavyouza nje. Matokeo yake tunapata matatizo katika *exchange rate,* dawa rahisi ni kuongeza mazao tunayouza nje. Tatizo ni mazao gani tunaweza kuyaongeza haraka? Mazao asilia ni pamba, korosho, chai, kahawa na kadhalika. Haya hatuyawezi kuyaongeza haraka. Tunaweza kudhamiria kuyaongeza lakini itatuchukua muda mrefu mpaka kupata kiwango kikubwa cha kuweza kuuza nje. Nafasi nzuri tuliyonayo ni kuongeza huduma kama vile za usafiri, kati ya *Dar es Salaam port* na nchi jirani na vile vile kukuza huduma katika utalii. Tukiongeza huduma katika utalii, watalii watakuja wengi, tutapata haraka fedha za kigeni, na tukiongeza matumizi mazuri ya *location* ya Tanzania ya kijiografia tutaongeza haraka mapato ya fedha za kigeni kwa matumizi mazuri ya bandari yetu ya Dar es Salaam.

Hivi sasa bandari yetu ya Dar es Salaam ambayo uwezo wake ni takribani tani milioni tano, matumizi yake ni kati ya tani milioni mbili mpaka milioni tatu. Kwa hiyo, kuna tani milioni mbili za ukubwa wa bandari ya Dar es Salaam hazitumiwi ipasavyo.

Tatizo ni miundombinu ya kutoka *Dar es Salaam port* kwenda Rwanda, Uganda, na Burundi na kwa maana hiyo kwenda Zaire. Bajeti inazungumzia juu ya kutengeneza miundombinu. Lakini na mimi nasisitiza miundombinu, ila tumekuwa tunazungumza miundombinu kwa ujumla. Hapa kuna haja ya kuwa na uhakika wa kuangalia ni miundombinu gani ambayo inaweza kutuletea *quick wins* katika uchumi wetu. Miundombinu mmojawapo na wa haraka sana ni Reli ya Kati ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati ya Tanzania ikitengenezwa vizuri itakuwa mkombozi wa nchi hii kiuchumi na sasa hivi tuone aibu kwamba hatuitumii reli ile kikamilifu. Tuweke mkazo, reli ifanye kazi ili iweze kutuletea matokeo mazuri ya kiuchumi. Sambamba na hilo tutengeneze barabara ya kudumu kutoka Manyoni, sasa imeshafika Manyoni iende moja kwa moja Tabora mpaka Kigoma. Huko itafika mpaka Burundi, Zaire na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, miundombinu itaokoa uchumi wa nchi hii na kwa kuongeza sehemu za mizigo itakayosafirishwa. Kama hatuna fedha za kutengeneza miundombinu hii, Serikali ruhusu ijengwe barabara hiyo ya kutoka Manyoni mpaka Kigoma kwa kutumia utaratibu wa *Build Operate and Transfer (BOT)*.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo nataka kukazia, kusisitiza samahani. Ni suala zima ambalo linazungumziwa kuhusiana na mauzo ya *Treasury Bills* pamoja na *Government Bonds.* Mauzo ya *Treasury Bills* na *Government Bonds* yanafanyika kwa utaratibu wa kwamba ni *monetary* ya *policy tool.* Uuzaji wa *Treasury Bills* na *Bonds* ni utaratibu wa *monetary policy.* Ni chombo ambacho Benki Kuu ya nchi inatumia katika kufanya mambo mawili makubwa.

La kwanza ni kuweza kupata *bench mark* ya *interest rates structure* katika uchumi na la pili inaisaidia Serikali kutumia *Central Bank* kuondoa *excess liquidity* ambayo iko katika uchumi. Pesa zinazopatikana na uuzaji wa *Treasury Bonds* pamoja na *Treasury Bills* ni matokeo tu ya *monetary policy action.* Tatizo letu liko katika matumizi ya fedha tunapozikusanya kupitia *Treasury Bills* pamoja *Bonds,* tunazifanyia nini.

Mheshimiwa Spika, hapa nataka nisisitize tuwe na uamuzi wa makusudi kwa sababu Serikali ina upungufu wa fedha kutoka katika vyanzo vyake vya kodi tutumie chanzo hiki cha *Government Bonds* ambazo tutazikusanya kwa makusudi baada ya kuelewa tuna mahitaji gani hasa katika miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ukishajua unataka kutengeneza barabara hii na hii na hii huna fedha, fedha zinaweza kupatikana humu humu ndani kwa kuuza *Bonds* za muda mrefu kwa miaka 10 mpaka miaka 15 na kuzitekeleza katika miradi maalum ya miundombinu iliyokusudia kufanywa. Hilo linawezekana tulifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine ambalo ningependa nilizungumzie kwa mkazo zaidi, nalo ni kuifanya Dar es Salaam kwa maana hiyo Tanzania tuwe na *free port.* Tuna kila sababu ya kuifanya Dar es Salaam kuwa *free port* na tukafaidika sana. Watu wa Malawi, Zambia, Zaire, Rwanda na Burundi na sisi wenyewe kama Tanzania tukiifanya *Tanzania free port* tutanunua vitu vingi vya nje hapa hapa. Wawekezaji wenye makampuni huko nje ambao vitu vyao vinahitajika na hawa ambao wako *land locked*

kuwekeza hapa. Sisi kazi yetu ni kusafirisha na kupata fedha. Tuna tatizo gani la kufanya hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ni matokeo ya mpango, suala ni kwamba je, mipango yetu ni mizuri. Mpaka sasa hivi tunafanya vizuri. Lakini nasema tungeweza kufanya vizuri zaidi, kwa kubadilisha muundo wa utaratibu wetu hasa wa chombo kinachopanga. Mpaka sasa hivi tunatumia Wizara yetu ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, nashauri Serikali ifikirie uwezekano wa kuanzisha Tume ya Mipango ambayo Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, itakuwa ndiyo sekretarieti, Mwenyekiti wa Tume ya Mipango atakuwa ama Rais au Waziri Mkuu. Wako baadhi ya Mawaziri watakuwa Wajumbe wa Tume hii lakini kubwa zaidi ni kwamba Tume hii itakuwa na wataalamu hususan ambao wamebobea na ndiyo watakaokuwa wanaleta mawazo ya ziada katika hiyo Tume.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na mipango mizuri Bajeti ni matokeo yake. Tukiwa hatuna mipango mizuri ndiyo tunaanza kuhangaika kila mwaka tunapanga lakini hatuendi mbele. Hii inaonyeshwa na tarakimu za ukuaji wa uchumi wetu kama ilivyotolewa katika kitabu cha Mipango. Uchumi wetu utakuwa kwa asilimia 7.3 mwaka wa 2007 utakwenda kwenye asilimia 7.7 mwaka 2008, utakwenda 7.9% mwaka 2009. Tunapofikia mwaka 2010 ndiyo utafikia asilimia 8.1. Ukuaji wa uchumi wetu katika asilimia hizi hautatutoa katika umaskini. Hizi *figures* zinaonyesha kwamba *business as usual* hakuna *changes* hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani ni kwamba mwaka 2007 asilimia 7.3, mwaka 2008 asilimia 7.7 na mwaka 2009 ni asilimia 7.9 ni *business as usual, we are not serious.* Ili nchi yetu iweze kuendelea vizuri na tuondokane katika umaskini, tunahitaji kufikia *rate* ya kati ya asilimia 8 mpaka asilimia 10 ya ukuaji wa uchumi. Tunafanya nini ndiyo maana nimesema tuanzishe Tume ya Mipango ambayo itatuambia tufanye nini na watakaokuwa katika Tume hii ni watu wazito ni Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri waandamizi pamoja na watu waliobobea katika masuala ya uchumi, tutakwenda tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna haja ya kutumia rasilimali zetu vizuri. Sasa hivi tuna gesi asilia. Gesi asilia inaweza ikazalisha umeme, lakini vile vile inaweza ikatengenezwa mbolea. Kwa kuwa tuna mikakati mizuri tumeshajiwekea kuzalisha umeme sasa hivi ambayo inatutoa wasiwasi wa kukosa umeme, tunaweza tukauza umeme wa ziada nchi jirani. Tunangoja nini kufanya maamuzi ya kukaribisha wawekezaji wakubwa waje kutumia gesi asilia, watengeneze umeme tuuze nje na gesi nyingine tutengenezee mbolea hapa nchini kwa ajili ya kufufua kilimo.

Mheshimiwa Spika, nimeuzungumzia utalii, tatizo letu kubwa katika utalii ni kutumia *package tours.* Tusimamie vizuri utalii wetu utatukomboa, tuondokane na suala la *package tours* waje kulipia hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwindaji wa utalii ni eneo ambalo lina matatizo na ni eneo nyeti, lakini linapendwa sana. Linaweza kutuletea fedha za kutosha. *Export Processing Zone* zinaanzishwa na Serikali kwa maana ya kuanzisha maeneo ya kuweza kutengeneza

vitu na ku-*export.* Lakini katika mwaka huu nilikuwa napitia Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, wamepewa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kutengeneza *Export Processing Zone, are we serious?* Kwa maana ya kukuza *exports* ambazo ndiyo mkombozi wa nchi hii. Hapo napo tunahitaji kuangalia vizuri kama tunataka kukuza *export* tuwekeze katika haya maeneo *in the real sense of the world.* Siyo tuwe tunacheza cheza tuna-*scrach the surface* tuweke pesa za kutosha ili tutengeneze *Export Processing Zone* za maana kama tunataka zitukomboe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie, kwa kusisitiza umuhimu wa kuwa na Benki ya kukopesha kwa muda mrefu. Hatuwezi kuendelea kama hatuna benki ya kukopesha kwa muda mrefu, kwa maana ya viwanda, kilimo na sekta nyingine muhimu nchini. Tuliambiwa mwaka jana kwamba kuna mpango wa kuibadilisha *TIB* iwe benki ya kukopesha kwa muda mrefu. Mpaka leo mpango huo haujakamilika. Kuna nini? Naiomba Serikali itilie mkazo jambo hili ili tuweze kujikomboa katika maeneo ya kuwekeza kwa muda mrefu kwa njia ya mikopo ya muda mrefu. *(Makofi)*

Sambamba na hili, ni suala zima la mikopo ya nyumba, sekta ya ujenzi ni sekta muhimu ambayo inaingiliana na sekta nyingine kwa kiasi kikubwa. Ukijenga nyumba utahitaji simenti, mabati, misumari, mbao na utahitaji kila kitu. Kwa kuitengenezea mazingira mazuri sekta ya ujenzi tutaamsha uchumi mzima ambao sasa hivi unasinzia sinzia kwa sababu viwanda vingi na watu wengi watapata soko, watu wa simenti wapata soko, watu wa kokoto watapata soko na vibarua na mafundi watapata kazi. Tunazungumza juu ya ajira, ajira ziko katika *construction sector* kwa maana ya nyumba na kwa maana ya barabara. Tukiwekeza huko tutainua uchumi wetu kwa haraka kuliko vile tunavyofikiria na hizi *rates* za 7.7%, 7.3%, 7.9% za ukuaji wa Pato la Taifa, tunaondokana nazo kwa haraka zaidi na tutaanza kupaa kwenye 8%, 10% na uchumi wetu utakuwa mzuri na tutaondokana na umaskini. *(Makofi)*

Katika kitabu cha Mipango kinasema *target* yetu ya *inflation* mwaka kesho ni 4.5%. Asilimia 4.5 haiwezi kufikiwa kwa *policies* za kupandisha mafuta. Kupandisha bei ya mafuta halafu unasema unataka *inflation* iwe kwenye 4.5% wakati sasa hivi iko kwenye 6%, unapandisha mafuta ambayo yanagusa kila sekta ya uchumi halafu tunasema *target* yetu ya *inflation* ibaki kwenye 4.5% ni kujidanganya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuangalie tunaweza kufanya nini ili ile *target* ya 4.5% ya *inflation rate* maana yake ndiyo iko katika kitabu cha Serikali. *Policies* zetu *are not consistent. Objective* yetu ya *inflation* ni 4.5%, lakini *our policies* zinakwenda kinyume. Kwa hiyo, hilo tunahitaji kurudi kwenye *drawing board* na kuangalia je, kweli tutafikia 4.5%? *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuzungumza na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa muda huu ili niweze kuchangia katika Bajeti hizi mbili ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze kwa jitihada ambazo umeonyesha za kuweza kuhamasisha timu yetu ya mpira ya Taifa kuingia hapa Bungeni, shabaha ikiwa ni kuhamasisha na kukuza michezo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wawili waliotoa mipango yao na Bajeti ya mwaka huu wa 2007/2008 na lazima tuseme kitu kimoja ambacho mimi nimekiona kwamba kumekuwepo na uwiano mzuri na mtiririko mzuri kati ya Bajeti ya Mipango na Bajeti ya Fedha, yaliyozungumzwa katika Mipango unayaona katika

Mheshimiwa Spika, nataka niseme mambo machache, kwanza *observation* yangu inaonyesha katika Bajeti zote mbili mambo yafuatayo:-

Kwanza uchumi wetu unakua kwa kasi ndogo zaidi ya mahitaji yetu. Uchumi wetu unakua kwa kasi ndogo zaidi ya mahitaji yetu ni jambo la hatari hili. Mahitaji yetu yanafikia zaidi ya shilingi trilioni 12, uwezo wetu wa ndani ni nusu ya hapo, trilioni 6, hapo inatuonyesha kwamba hatuna njia zaidi ya njia mbili. Kwanza, kupunguza mahitaji yetu ili yawiane na uwezo wetu. Lakini la pili ni kutafuta misaada kutoka nje ili angalau tuweze kukidhi kiwango kikubwa zaidi cha mahitaji yetu. Tunahitaji fedha.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo yapo katika Bajeti katika sehemu ya Mipango yaliyojitokeza, yanayoonyesha sababu inayofanya mambo haya mengi au uchumi wetu kushuka. Kwanza kumekuwa na kushuka vile vile kwa biashara yetu ya nje. Kwa hiyo, kuna matatizo katika *balance of trade to balance of payment.* Hili siyo jambo zuri. Tuna maonyesho ya biashara kila mwaka ya Saba Saba, kila mwaka. Lazima tuangalie sasa Saba Saba hii inatusaidia nini, maonyesho haya yanatusaidia nini hasa katika kuwezesha Taifa letu kuuza bidhaa nje ya nchi, kama maonyesho haya yanatupa mwelekeo tofauti basi lazima tuangalie kama kweli haya tunayaendesha vizuri. Kama matokeo ya maonyesho ya Kimataifa yanafanya Tanzania iweze kuingiza bidhaa nyingi zaidi nchini badala ya kuuza nje ya nchi lazima tujiulize kama ndiyo shabaha ya maonyesho yetu ya Kitaifa. Kwa sababu maana yake ni kwamba maonyesho hayo yanachangia kufanya hali yetu ile ya *balance of trade* na *balance of payment* iwe mbaya na hilo siyo jambo zuri. Tuangalie na tujirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika upande huo pia wa Mipango tumeona kwamba uchumi unadidimia. Lakini huwezi ukaimarisha uchumi wako bila kuimarisha mambo makubwa na muhimu sana. Ni kweli tumefanya vizuri kuongeza na kuweka kipaumbele katika elimu. Lakini miundombinu ina matatizo makubwa, miundombinu bila kuifanyia kazi tukairekebisha uchumi utaendelea kudorora na hapa inabidi niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tuliona athari za mvua zilizonyesha. Katika sehemu nyingi Serikali ilijitahidi, barabara nyingi zikawa zimetengenezwa. Lakini mvua kubwa zilizokuja zimeharibu kwa kiasi kikubwa miundombinu. Tumekaa katika Bunge hapa, tukaomba mpango maalumu, fedha maalumu, fungu maalumu ili kufanya marekebisho ya miundombinu iliyoharibika. Fedha tulizokuwa tumekusudia kuzipata hazikuweza

kupatikana kwa sababu uwezo wetu ulikuwa ni mdogo. Lakini bado tunahitaji miundombinu. Lazima tuangalie upo wapi kwa mfano mkakati wa kuimarisha na kuboresha bandari zetu. Bandari ya Tanga, Bagamoyo, Dar es Salaam na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, tunaposema tunataka kujenga na kuwa na mikakati ya kuboresha miundombinu na hivyo kuboresha bandari zetu maana yake tunahitaji fedha. Tukisema kwamba tunahitaji kujenga reli, kutoka Tanga kwenda Arusha hadi Musoma ni mkakati mzuri wa kuimarisha miundombinu lakini maana yake na tafsiri yake ni kwamba tunahitaji fedha. Tunaweza tukawa na mkakati lakini hautatekelezeka kama hatutakuwa tumepata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipoona hali ya barabara zetu imeharibika na fedha hatuna, ndipo tulipokaa chini tukasema tutafute fedha kutoka vyanzo vyetu vya ndani. Hapo ikalazimika kutoa mapendekezo ya kuongeza angalau bei ya petroli ili kutafuta fedha za ndani kutoka katika uwezo wetu sisi wenyewe. Sasa hili linaweza kuwa limefanyika na sehemu ya Kamati ya Bunge lakini Kamati ya Bunge inafanya kwa niaba ya Bunge Zima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mapendekezo yale ni sahihi kwa sababu wenzetu waliyakubali, waliyapendekeza wakapeleka Serikalini, Serikali ikayakubali. Kwa hiyo, ni mapendekezo yetu sisi wote Wabunge na Serikali. Hivyo mimi napata taabu sana niliposikia kauli kwenye magazeti wakisema kwamba eti Serikali inasema siyo sisi Serikali tuliyotaka kuongeza bei ya mafuta ni Wabunge. Hapo ile maana ya uwajibikaji wa pamoja *(collective responsibility)* inapotea. *(Makofi)*

Sisi lazima tusimame kidete na tuwajibike pamoja kwa sababu tunatafuta fedha ili kukamilisha mikakati ambayo tunaamini kabisa ndiyo itakayosaidia kujenga uchumi wa Taifa hili. Hali ya kilimo ni mbaya na taarifa zinaonyesha hapa kwamba hata uzalishaji umeshuka badala ya kuongezeka. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni kwamba mikakati yetu tulioianzisha ya kuboresha kilimo haijafanikiwa, haifanikiwi. Mikakati gani hapa? Tuna *National Irrigation Master Plan,* kama kweli mkakati huo ungekuwa unafanikiwa matokeo yake si kushuka kwa hali ya kilimo ingekuwa ni kuongezeka kwa uzalishaji wa hali ya kilimo. Lakini unapoona hata kilimo kinashuka na tuna mkakati unaoitwa *National Irrigation Master Plan then their something wrong.* Mimi nimeona kwa sababu katika jimbo langu kuna miradi miwili ya umwagiliaji, ina miaka sasa mwaka mmoja na nusu haitekelezeki, haijengwi, haimaliziki, matatizo fedha hakuna. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu mimi nimewashuhudia, nimewaona, lakini nataka niseme wana matatizo kweli. Vyombo vyao vya kufanyia kazi ni chakavu kupita kiasi, watawezaje kuchimba mabwawa hawa. Watawezaje kufanya kazi nzito hizo za *irrigation plans* bila kuwa na vifaa vya uhakika vya kufanyia kazi, vipo jimboni kwangu vimekaa, vina miezi 11 sasa havifanyi kazi, fedha hakuna na vifaa chakavu. Tuwasaidie, lakini tusaidie vile vile pamoja na kwamba tumeongeza Bajeti kidogo ya kilimo nadhani haitoshi. Tunahitaji kuandaa mkakati wa watendaji. Mheshimiwa Waziri ana mpango mzuri lakini je, tunampa fedha? Watendaji vijijini hakuna, hawatoshi, mabwana shamba. Mimi kama

Mbunge ni mkulima vile vile. Lakini utashangaa hata shambani kwa Mbunge, bwana shamba hajakanyaga pale.

Mheshimiwa Spika, mimi ninafuga pia, maana yake watendaji hawa hakuna. Sasa hata kama shamba la Mbunge, bwana shamba hajafika pale kwa zaidi ya miezi 12 je, kwa jirani zangu? Mimi ni kiongozi hajafika, je, kwa wale wengine ambao wanahitaji msaada zaidi? Matokeo yake kilimo kinaendelea kushuka, tuiwezeshe Wizara hii iweze kufanikiwa katika kupata vifaa na watendaji wa kutoa huduma. Lakini tunatoa mbolea *subsidies* lakini hizi mbolea kweli zinawafikia walengwa? Kwa kiwango kikubwa haziwafikii walengwa, tuwasaidie. Wapo watu wa kati wanakwenda kwa wakulima wetu wanawakopesha mbolea lakini wanawakata fedha wakati wa mauzo, wanakwenda kununua kutoka kwao na baada ya kununua mazao wanakata fedha walizowapa za mbolea, maana yake ni nini? Hawa watu tena wanafanya biashara hapa nchini maana yake wanapata *income* kutokana na mbolea waliopeleka kwa wakulima wetu badala ya kuchukuliwa ile ya *subside.* Hivi tunawakamata kodi wale? Si wanafanya biashara? Mheshimiwa Waziri watafute, wapo.

Mheshimiwa Spika, kitu kikubwa cha kuzingatia ni matumizi ya fedha zetu, tuna mikakati mizuri, usimamizi wa matumizi ya fedha. Ukienda kwenye Halmashauri ambapo sasa fedha nyingi zinakwenda utashangaa yaani Halmashauri ya Wilaya au ya Manispaa ina akaunti tofauti 35, *how do you manage your money?* Akaunti 30? Kila Idara ina akaunti yake na *signatories* wake. Hivi kweli *accounting system* za wapi hizo? Tunaweka *loopholes* za kuwafanya watu watumie fedha hizi bure tu bila sababu. Akaunti 30, *how do you manage to control the accounts? Impossible!* Kwa hiyo, fedha tunapeleka kule zinapotelea mbali tu hazifanyi kazi za maendeleo yaliyokusidiwa.

Lakini kingine kibaya ambacho nakiona ni mikataba, Wajerumani walipokuja Tanganyika kuna Mjerumani mmoja mjanja sana alikuja anaitwa Karl Peters. Karl Peters alikuwa hodari wa kutengeneza mikataba ya ulaghai, sasa Taifa hili limetawaliwa na mikataba ya Karl Peters. Ukienda sehemu mbalimbali kama kwenye Madini ni Karl Peters, ukienda popote pale ni Karl Peters tu hivi kweli tutafika? Hatutafika, Karl Peters wana mikataba ya uongo na udanganyifu lakini wanaondoka na fedha chungu mzima. *(Makofi)*

Hapa katika Bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri anatuambia bado kuna ule mkakati wa kulipia gharama za dharura za umeme *2.4 billions,* mikataba ile ni ya Karl Peters. *2.4 billion* hizi tungezisimamia vizuri tukaondokana na matatizo haya zingetusaidia sana wala tusingekuwa na sababu ya kupandisha bei ya petroli na kadhalika. leo sitazungumzia sana habari ya mafuta kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameyazungumzia kwa kiwango kikubwa sana. Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, amezungumzia vizuri sana, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, pia amezungumzia vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bila kusimamia vizuri fedha tunazozizalisha ndani na zile za wahisani kazi hii ya kuboresha uchumi wetu itakuwa na vipingamizi vikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia ada za leseni za magari, hata mimi nataka niseme kidogo kwamba viwango hivi hasa vya *cc* kati ya 1500 na 5000 ni kikubwa, 235,000/= ni kikubwa sana. Magari ndugu zangu siyo anasa, tunahitaji magari kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli muhimu za kiuchumi, ukusanyaji nataka niwahakikishieni kama wenzangu walivyosema ukusanyaji wa kodi, huu sasa utakuwa ni mgumu sana kwani kila mtu atajitahidi kuikwepa kodi hii. Tulitaka kuhakikisha kwamba watu wanalipa kodi kwa hiari, watu wameanza kubadilika, walikuwa wanakwenda kulipa *TRA* na walilipa kodi kwa hiari lakini si kodi ya viwango vikubwa kama hivi. Watu wataikwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba mimi ninasikitika sana kwamba sekta ya mafuta imeishinda Serikali. Wamesema katika taarifa yao kwamba makusanyo katika sekta hii yanakuwa magumu sana lakini washauri wa mafuta wapo hatuwatumii. Nawapongeza chombo kile kinachoitwa *EWURA* angalau ile *Regularity Authority* sasa inaongozwa na watu ambao nafahamu na ninawafahamu wana uwezo katika sekta hii ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na ikiwa muda utakuwa bado upo inavyoelekea basi atafuatia Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN AHMED SADDIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niwapongeze sana Mawaziri wote kwa hoja zao zote mbili yaani ya Mipango na ile ya Fedha na pia naomba kutamka kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu tunaweza tukasema iko *tight* lakini kuwa *tight* kwa Bajeti yetu kunategemea zaidi na mipango halisi ya nchi yetu. Nchi yetu ina mipango mizuri ya kuwasaidia wananchi wake na ndiyo maana Bajeti iko *tight* kwa sababu tunataka kupeleka maendeleo vijijini na mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianze na suala la Benki Kuu yaani *BOT*. *BOT* ni kiungo muhimu sana katika Taifa lolote lakini katika nchi yetu tegemeo la uchumi ni Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nilibahatika kutembelea majengo mengi ya *BOT,* tulianza na *Green Tower* tukaenda Zanzibar na baadaye tukaenda Mwanza. Naomba tuipongeze Serikali kwa uamuzi wa kujenga *Green Tower* katika jiji la Dar es salaam. *(Makofi)*

Naipongeza sana Serikali na viongozi wote walioshiriki kwani jengo lile ni jengo ambalo linakidhi mahitaji ya miaka 20 au 50 mbele, ni jengo ambalo litatuletea mambo mengi yanayohusu uchumi katika Taifa letu kwa miaka mingi ya mbele na pia ni heshima kwa Taifa letu lakini ni heshima katika mtandao wa sasa hivi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Spika, mimi ushauri wangu kwa *BOT* ni kwamba waangalie mipango mingine mizuri ya kujenga jengo kama lile katika Jiji la Mwanza, Mwanza tumefika *BOT* jengo lao bado halikidhi mahitaji ya Kanda ya Ziwa. Kanda ya Ziwa inachangia pato kubwa la Taifa. *(Makofi)*

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha akae na wenzetu wa *BOT* waangalie uwezekano wa kuiona Kanda ya Mwanza kwa maana ya kuwa na jengo la kisasa la *BOT* litakalokuwa linafanya kazi nyingi zitakazoweza kuimarisha uchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, *Green Tower* ya Dar es Salaam siyo mchezo, mimi nimetembelea jengo lile mara mbili kama Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, maelezo tuliyopewa yanakidhi mahitaji ya Taifa hili kwa miaka mingi mbele, narudia suala hili kwa hiyo, mimi naungana mkono kabisa na juhudi za Serikali za kujenga *Green Tower* na kuimarisha *BOT* naomba mkaze buti mbele kwa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niingie kwenye Bajeti au kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kabla ya yote naomba ku-*declare interest,* mimi ni mfanyabiashara, naelewa sana mambo ya magari na mambo ya mafuta lakini hapa naweka mbele maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la magari, ukurasa wa 55 tumezungumzia zaidi ushuru wa magari kwa maana ya *road licence* zile za kila mwaka. Mimi hoja yangu ni moja tu kwamba nakubaliana na *figure* zile kwa sababu hii ni *balance budget* hatuweza kubadili chochote tunachotaka Bajeti ikafanye kazi tuone mabadiliko ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mimi naungana na wenzangu kuhusu suala la *cc, cc 1500* ni kigari kidogo sana, leo Mtanzania anayepata ajira katikati ya jiji anayetoka *Mbezi Beach,* Kimara na maeneo mengine ndani ya Jiji ana *RAV 4* yake ina *cc 1950* au Vitara yenye *cc 1690* au *Baloon* yenye *cc 1600* atawajibika kulipa 230,000/= kila mwaka huku tunataka Watanzania wawe na maisha bora. Mimi naishauri Serikali kuanzia *cc 1500* mpaka *cc 2500* magari haya yanatumiwa na Watanzania wenye kipato cha chini na wengi wao wameajiriwa na Serikali, wengi wao ni watumishi na wafanyakazi. *(Makofi)*

Mtu ana *Pick Up* yake anachukua majani ya ng'ombe anakwenda kulisha mifugo yake *Pick Up* ina *cc 1800* mpaka 2400, mimi nashauri *cc* hizi tuzibadilishe kiwango cha shilingi 80,000/= kibaki lakini *cc* ziishie 2500, hapa tutawagusa Watanzania wenye kipato cha chini na wenye ajira ambao kila siku tunahamasisha wapate maendeleo. Sisi wenye ma-*VX* tutamudu hatuna matatizo lakini tuwalenge wale wakulima wa Turiani, Mvomero, Sumve na maeneo mengineyo. *(Makofi)*

*TRA* walichokifanya hapa ni kuangalia urahisi wa kukusanya, Taifa letu lina magari takribani 325,000, mwaka jana baada ya kukubaliana kwamba kila mtu ana–*renew* kwa 20,000 *TRA* wamekusanya zaidi ya shilingi bilioni 5 hadi mwezi huu wamevuka lengo la 75% au wamefika 75% wakaona wapite hapohapo, Bwana Kitilya iko janja sana hii, wakaona sasa waingie hapo wakusanye mapato zaidi, mimi sina tatizo, mapato yakusanywe lakini hoja yangu ni moja kwamba kwenye *cc* tuziangalie.

Hoja yangu ya pili ni kwamba fedha hizi zitakazokusanywa katika eneo hili ziende kwenye barabara liwe tamko la Wizara ya Fedha, *TRA* walete makusanyo yote yanayotokana na ada za leseni za magari kama ni shilingi bilioni 50 au 60 fedha hizi ziende kwenye barabara moja kwa moja bila kuingia kwenye mafungu mengine ya Serikali. Hilo ndilo wazo langu au ushauri wangu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye sekta ya mafuta kidogo tu, wenzangu wamezungumza sana mimi sina tatizo na hilo, mwezi Aprili, 2007 kwenye Bunge hili wakati tulipokuja na mjadala wa Mheshimiwa Andrew John Chenge kuhusu suala la barabara mmoja wa Waheshimiwa Wabunge waliochangia na kuiomba Serikali kwamba iongeze *road toll* mmojawapo alikuwa ni mimi na leo naunga mkono suala hili kwa sababu tunahitaji barabara vijijini, tunahitaji wakulima waweze kusafirisha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kutengeneza barabara mimi sina mjadala nalo na sina kipingamizi naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Tatizo ambalo naliona lipo kwenye mafuta ya taa, shilingi 4 hizi zitaleta usumbufu mkubwa kwa Watanzania wenye kipato cha chini. Mimi ushauri wangu ni kwamba shilingi 4 hizi tuzigawe ili Bajeti iendelee kuwa *balanced budget.* Shilingi moja iende kwenye petroli, shilingi moja iende kwenye dizeli, shilingi moja iende kwenye mafuta mazito, shilingi moja iende kwenye mafuta ya mitambo ya viwandani yaani *IDO.* Zile shilingi kwenye mafuta ya taa tuziondoe, mafuta ya taa yasibadilike yabaki bei ya zamani. Pale tumguse moja kwa moja yule mtu ambaye hata uwezo wa kupanda gari hana lakini mafuta ya taa anayahitaji, anawasha kibatari, anahitaji mafuta ya taa. Suala la kuchanganya hili ni kazi ya Serikali. Wenzangu waliotangulia wamezungumza ni kweli mchanganyiko huo upo unaharibu magari, na mitambo Serikali ifuatilie eneo la Mkoa wa Pwani hilo wenzangu wamelizungumza, mimi hoja yangu kubwa ni ushuru wa mafuta ya taa ikiwezekana tuuondoe na fedha hizi shilingi 4 ziende kwenye makundi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niingie kwenye viwanda vya nyama. Pale kwenye Jimbo la Mvomero kuna kiwanda cha kisasa cha kusindika nyama na katika nchi yetu kuna viwanda vingi, tatizo lililopo ni kwamba viwanda hivi vinasuasua kwa sababu nyama kutoka nje ya nchi imekuwa ni nyingi mno. Mimi ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba ili tuendelee kuvilinda viwanda vya nyama ambavyo sasa hivi vinaibuka na vinakuwa viwanda vingine vya wazalendo naomba ushuru wa nyama kutoka nje uongezwe ili tuvilinde viwanda vya ndani. Katika Wilaya ya Mvomero kuna wawekezaji wana kiwanda cha nyama na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye ziara yake mwaka huu tulitembea naye na kwa kweli tulifika mahali tukaona ni kiwanda cha kisasa

na maeneo mengine mengi katika nchi yetu kuna viwanda kwa mfano Sumbawanga na Mtibwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliangalie sana suala hilo ili tuendelee kuvilinda viwanda vyetu na Watanzania waendelee kupata ajira.

Suala lingine ambalo ningeomba Serikali iliharakishe ni suala la *mortgage finance,* bila ya kuwapa mikopo ya kununua au kujenga nyumba, Watanzania hatutawafikisha mahali popote, zipo sheria ambazo hazijafanya kazi, naomba zile sheria zifanye kazi na kama hazifanyi kazi basi sheria nyingine iletwe haraka Bungeni watu wapewe mikopo ya kujenga nyumba kuanzia miaka 20, 25 na hata 30 kama ilivyo katika ulimwengu huu katika Mataifa mengi duniani hapa kwetu inaonekana mabenki haya bado yanasubiri amri au agizo la Serikali. Mimi naishauri Serikali itoe maelekezo haraka na sheria zilizopo zifanye kazi, hilo peke yake litawasaidia watu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda naomba sasa niingie kwenye michezo. Katika michezo naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi alivyokuwa makini katika suala zima la michezo, nampongeza sana kwani hatua tuliyofikia ni kubwa sana, nchi yetu imeanza kupata heshima iliyokuwepo kwenye Taifa letu miaka ya nyuma. Michezo katika Taifa hili ni mingi kuna *basketall, netball, vollyeball* na michezo mingine ya jadi. Namwomba sasa Mheshimiwa Rais kupitia Wizara yake atoe kipaumbele kwa Wizara ili michezo mingine yote nayo iweze kusimamiwa na vile vyuo vya michezo navyo vipewe kipaumbele, michezo ichukue sura ya nchi, isiwe soka peke yake kwani soka peke yake anayekwenda uwanjani anaacha Bunge ni Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya tu, lakini ikiwa michezo mingine wengi tunaweza tukashiriki. Katika hili hili la michezo naomba na suala la michezo ya jadi nalo liangaliwe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia katika suala hili uwanja mpya wa Taifa yapo mawazo ya wanariadha wetu, kwa mfano Ndugu Filbert Bayi na Ndugu Suleiman Nyambui. Kuhusu uwanja ule kutokuwa na sifa ya riadha ya Kimataifa katika miaka ya nyuma wakati nipo Zanzibar Uwanja wa Amani ulikuwa na eneo la kukimbia, lakini uwanja wa Taifa huu mpya umekosa sifa, Wizara ipokee mawazo ya wadau akiwemo Ndugu Suleiman Nyambui na Ndugu Filbert Bayi, uwanja ule na sifa ya michezo yote katika Taifa kwani pato litaongezeka na mambo mengine yatakwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye Kilimo. Bajeti ya Kilimo inaridhisha kiasi siyo sana lakini bado mimi kama Mbunge nina matumaini kwamba hela za wafadhili zile za *SDP* zitaweza kutusukuma, huu ulikuwa ni mpango maalumu wa miaka saba, sasa tupo kama sikosei mwaka wa pili. Ninaomba sasa hivi tuwe makini katika suala hili kwa maana ya wananchi wanahitaji tena mbolea ya ruzuku, mbolea iliyotolewa mwaka jana imesaidia sana katika maeneo mengi hususani Mkoa wa Morogoro. Naomba Serikali itilie mkazo suala la mbolea ya ruzuku, wakulima wetu wapate mbolea ya ruzuku na pia suala zima la wataalamu wa kilimo wawezeshwe kwa maana ya nyenzo. Sasa hivi Mkoa wa Morogoro umeandaliwa kuwa Mkoa utakaoweza kulilisha Taifa hili kwa kiwango kikubwa na tupo kwenye mpango maalumu, katika hili nampongeza sana Mkuu wa Mkoa

wa Morogoro,Meja Jenerali Mstaafu Said Kalembo, yeye kama Meja Jenerali sisi makamanda tupo naye bega kwa bega na tunaungana naye katika mambo mbalimbali pamoja na hili la kilimo.

Mheshimiwa Spika, langu la mwisho ni barabara. Barabara bado ni tatizo, mwaka huu Bajeti inatia matumaini. Jana kulikuwa na Mwenge wa Uhuru ndani ya Jimbo langu tumeupokea kutoka mkoa wa Tanga, Wilaya ya Kilindi umeingia Mkoa wa Morogoro kuanzia Wilaya ya Mvomero, bila ya juhudi za pamoja kati ya sisi viongozi, Mkuu wa Mkoa na viongozi wengine Mwenge usingefika Manispaa ya Morogoro leo asubuhi. Barabara zimekufa vibaya sana lakini waswahili wanasema, mgeni njoo mwenyeji apone.Naona kengele imelia, baada ya kusema hayo natamka kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini na ninadhani tunaweza kupata muda kwa Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, kuwa msemaji wa mwisho kwa siku ya leo. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Kwanza nimpongeze Waziri wa Fedha kwa hotuba yake ambayo ni changamoto kwa Watanzania kwa kuchangisha fedha nyingi ambazo zitaleta maendeleo katika nchi kama zitatumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sina matatizo na kulipa kodi, kulipa kodi ni jukumu la kila raia mwema wa nchi hii, tumepata somo hapa Mheshimiwa mmoja Mbunge wa Tanga alitupa somo jinsi kodi inavyotozwa kutoka kule Marekani mpaka Uingereza kwa hiyo, tumekuwa wanafunzi wazuri na tumejua vizuri sana jukumu letu la kulipa kodi. Mimi sina matatizo na kulipa kodi. Lakini kodi inapokusanywa na hasa inapotoka kwa watu maskini kwa ajili ya maendeleo yao inatakiwa itumike vizuri na iende inavyotakiwa, hapo ndiyo tatizo. Lakini kwa mengine kulipa kodi hata kama zingekusanywa nyingi kwangu mimi naona ni faraja, ni nzuri kwa sababu zitatuletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mpangilio wa Rais wetu amesema kwamba tunataka kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania, ni kweli, tunataka Watanzania wapate maisha bora lakini watapata maisha bora kwa Bajeti hii? Je, kweli tumejiweka tayari kuleta maisha bora kwa Watanzania? Tutaweza kupata ajira kwa vijana wetu? Bajeti hii inalenga ku-*create employment* kwa vijana ambao tunataka wapate maisha bora. *(Makofi)*

Mimi nina wasiwasi, tunasema kilimo ni uti wa mgongo wa nchi hii, kilimo ndiko kwenye ajira kuliko chombo chochote katika nchi hii, kilimo ndiyo *survival* na ndiyo kwenye uhai wa nchi hii lakini ukiangalia Bajeti hii tumeweka kiasi gani katika kilimo, tumeweka kiasi kidogo sana. Ukiangalia wawekezaji ambao wamekuja Tanzania kuwekeza katika kilimo kati ya wawekezaji karibu 500 ni karibu 30 tu ndiyo wapo kwenye kilimo ambayo inaonyesha wazi kwamba hatuna msukumo katika kilimo na

kwenye kilimo ndiyo kijijini na ndiyo kwenye 80% ya wakazi wa nchi hii, ndiyo kwenye akina Masanja wanapokaa, na akipata mshahara wa shilingi 80,000 au 60,000 atampeleka mtoto wake shuleni, atapata chakula pia na ndipo atapata maisha yake na maisha bora yataanzia pale. Sijui maisha bora tutayapata wapi kama kilimo tutakifanya namna hiyo. *(Makofi)*

Mimi naamini katika kuwekeza katika miradi endelevu, miradi endelevu ambayo itaendelea kusaidia nchi hii itaendelea kuleta mapato katika nchi hii. Mimi kama nakumbuka Mbunge wa Same Mashariki aliwahi kusema migodi ni heri tuifunge kwa sababu siyo endelevu, kwa sababu siyo tija haituletei faida. Wenzetu wajanja wanatuchukulia kila kitu sisi hatupati kitu katika migodi na kwa kweli ile migodi tungeifunga mpaka watoto wetu wakasoma wakapata akili, wakaja kuianza, sisi hatujawa tayari kuiendeleza. Tungetafuta sehemu nyingine za kuwekeza. Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga amezungumza, tungewekeza katika Bandari ya Dar es Salaam, *hinderland* ya Dar es Salaam tuna Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi na Uganda. Wenzetu tunazungumzia wenzetu Singapore na hata Uarabuni wanatumia bandari na pesa za bandari ndiyo zinakuza nchi zile, nchi zile zimeweza kuwa tajiri na sasa zinakiburi cha kutoka kwa kutumia bandari tu sisi tunaangalia bandari ya Dar es Salaam kazi yetu ni kuleta makampuni mengi kazi yake mtu mdogo mmoja anakuja na kisanduku chake unaleta makampuni manne kum-*search* mpaka tunadhalilishana, tunajifanya hata hatuaminiami, tumejifanya Watanzania wote ni wezi hata tusachiwe watu 20 hii ni kudhalilishana. Ndiyo maana yake hata watu hawatuamini, hivi kweli wote sisi ni wezi?

Hivi kweli ambaye siyo mwizi ni mwekezaji tu ndiye anayeweza kupitisha kitu pale *Dar es Salaam Port* ambayo siyo mwizi? Hivi kweli Ndesamburo akipitisha kitu pale Dar es Salaam ni mwizi? Ya kuwa ni lazima apitie njia ngapi, yupo *Tusker* na mambo mengine mengi. Zamani tulikuwa na *uppers* na *customers* basi, hao wengine ni chakula tu, ni njaa tupu hii, tunatengenezea wenzetu chakula ya nini hii? Halafu ni mzigo kwa wenzetu, kuna *harbors* na kuna *customs*.

Mheshimiwa Spika, *customs* unapeleka *entry* yako kwa *custom* wanakukisia unapeleka *harbor* unatoa mzigo wako. Hawa wengine wote wa nini? Maana yake hata nchi za jirani wanakosa amani na imani na sisi ndiyo maana hawaleti mizigo yao hapa, *port* yetu imeshakuwa haina maana, mnasikia Dubai imeshakuwa kubwa na sasa hivi ni tishio inashindana na Amsterdam, Singapore walikuwa sawa na sisi walipopata uhuru lakini sasa hivi wako wapi na sisi? Ni tofauti kubwa, wana nini? Maana hata maji ya kunywa wana- *import* yaani hata maji ya kunywa hawana, kile kisiwa ni jiwe tu wanategemea bandari, sisi tuna bandari nzuri kuliko wao lakini tunashindwa kuitumia ile ni endelevu tunakwenda kwenye madini, ile bandari ni endelevu jamani wanaotaka kuwekeza waje kwenye bandari yetu na sasa tuanze kuweka imani kwa watu wetu wa Tanzania, tuondoe hawa *middlemen* tuwe na imani na Watanzania tusidhalilishane, siyo wote ni wezi katika nchi hii. Mtu aki- *make declaration* yake akasema ana mizigo yake basi aaminiwe ambaye ata–*make wrong declaration* akamatwe na afungwe maana yake ni mwongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani ile ni njia moja ambayo kama tukiweza kuitumia vizuri ingeweza kuiletea nchi hii mapato makubwa sana tungepata mapato makubwa ambayo tungeachana na mambo ya kutoza petroli na mafuta ya taa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu nyingine kama *TANESCO,* umeme hatuwezi kuendelea bila kutumia umeme, umeme ni sehemu moja ambayo ni ya lazima kama tunataka kuendelea kwenye viwanda na hata majumbani kwetu tunahitaji umeme, mashuleni kwetu tunataka watoto wetu wasome wanahitaji umeme ili waweze kusoma badala ya vibatari, leo hapa tunazungumzia vibatari kwa sababu umeme hakuna. Tulikuwa na matatizo makubwa ya umeme hapa tukaleta kampuni hata sijui kampuni ile ilikuwa inaitwa nini, ah!

Mheshimiwa Spika, *Netgroup Solution,* Watanzania wetu wasomi wakakataa, wakakataa mpaka wakakaa mlangoni wakapinga wale wazungu wasiingie pale kwa sababu walijua wale watakuja kuhujumu hapa lakini sisi viongozi tukawatoa kwa mitutu na tukawaingiza wale watu, ndiyo Watanzania viongozi tulivyo. Tukawaingiza wale watu kwa mtutu wa bunduki wakaja wakanyonya Mtera na wakachukua pesa zote wakaenda na Serikali ilikuwa inatoa ruzuku *TANESCO* wakapata pesa wakaondoka. Sasa tumeona makosa yetu tumeweka Mwafrika pale na sasa tumesema hata ruzuku tena hatutoi kule, jamani! Tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepigiwa kengele, lakini kwanza nizungumzie bia. Wote hapa jioni tukishachoka tunakunywa bia. Kila Bajeti lazima tuongeze bei ya bia wakati wengi wetu tunakunywa bia. Kila siku tunaongeza bei ya bia badala ya kuanzisha viwanda vingi Tanzania na Watanzania wapate kazi. Tuteremshe bei ya bia watu wengi wanywe bia. Halafu tupate fedha nyingi. Tuwe na Kiwanda cha Bia Mbeya, tuwe na kiwanda cha Bia Tanga, tuwe na Kiwanda cha Bia Moshi na tuwe na viwanda vya bia kila mahali. Halafu tuta-*create employment* na tutakuwa na watu wengi watakaopata kazi na Watanzania watakunywa pombe nzuri iliyochunjwa badala ya kunywa gongo.

Mzee kama mimi kuliko nikose bia yangu, afadhali mtoto wangu akose nyama, nitamkosesha kwa sababu lazima ninywe bia yangu. Kwa hiyo, tunawaua watoto wetu, kwashakoo tunaileta sisi kwa kupandisha bei ya bia. Tunawaua watoto wetu kwa kwashakoo na wengine wanakufa kwa kunywa gongo. Tuteremshe bei ya bia, hizi *breweries* ziwe nyingi na tutakusanya fedha nyingi zaidi. Huo ni ukweli kabisa nawaambia ndugu zangu, tusiogope hilo mkafikiri labda tutakosa mapato. Tutaongeza mapato mara mia moja kuliko tunayokusanya sasa. Kuna Mashirika mengine ambayo Serikali ina hisa ndani yake. Mashirika hayo huwa nashangaa *Board of Directors* wanaweza wakakaa wakaamua wanaenda kuchangia kwenye mashule, kwenye miradi. Hivi kweli zile fedha ni zao au ni zetu? Hawana sababu au hawana ruksa ya kuchangia zile fedha wakati zile fedha ni za Watanzania, zile fedha ziende *treasury, treasury* ndiyo ina majukumu ya kuweza kuzigawa. Unakuta Benki ya *NMB* wanatoka hapa wanakwenda shule fulani labda kuna mkubwa pale wanachangia kuijenga, hii maana yake nini? Wanaweza kuja kwangu pale CHADEMA wakachangia kweli, hawawezi! Kwa hiyo, hilo si sahihi. Hayo Makampuni ambayo Serikali ina-*share* ndani yake wanasichezee fedha zetu kwa kutoa michango ambayo si halali. Zile fedha ni zetu ziende

*Treasury* ndiyo wenye jukumu la kuweza kuamua kama ziende wapi, lakini sio wao wanachangia kufuata mtu fulani tumchangie hapana, hiyo siyo halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia mafuta na kila mmoja amezungumzia na mimi vile vile nizungumze kidogo juu ya mafuta. Mafuta tumepandisha bei, mafuta ni kama damu kwenye mwili wa binadamu. Ukiyagusa mafuta ni mfumo wa bei nchi nzima kwa sababu hakuna kinachotembea bila mafuta. Petroli ni kama dawa ndani ya mwili wa binadamu. Kwa hiyo, tumegusa pale mahali pabaya na kwa kweli mfumuko wa bei utakuwepo. Tutakusanya fedha kweli, lakini tumegusa mahali pabaya, patakuwa na mfumo mbaya na matatizo yatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, nisije nikagongewa tena kengele ya mwisho. Kwa hayo machache, naomba kusema siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Raynald Mrope bahati mbaya utakuwa na dakika kama 11 tu. Sasa labda nikupe dakika 10 halafu kesho uwe wa kwanza kumalizia dakika zako tano. Kama unaweza kumaliza vizuri, lakini una haki yako ya dakika 15. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuwa mzungumzaji wa mwisho kwa usiku huu wa leo. Sasa naomba niende moja kwa moja kwenda kuchangia. Bajeti hii ni ngumu na katika kuwa ngumu lazima tujifunge kibwebwe. Haisaidi kuipinga Bajeti wale wanaosema kwamba tutatembea, ndio mtafika mpaka *Atlantic* na hakuna lolote, mtakalofanya, mtarudi hapa hapa. Hii Bajeti kinachotakiwa ni utekelezaji mzuri katika maeneo yote na tukiyatekeleza vizuri mtaona yatafidia yale mapungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye Bajeti kama tunavyozungumza siku zote maana ndicho wanachotutuma wananchi. Sasa mimi walichonituma wananchi ni kwamba hata kama Bajeti hiyo ikiwa ndogo kasemee barabara ya Kusini. Dar es Salaam-Lindi mpaka Masasi haya ndiyo mambo mazito. Tunategemea mwisho wa Bajeti Waziri anayehusika au hata Waziri wa Fedha atueleze kwamba barabara hiyo tulioanza kuililia toka miaka yote itakamilika siku gani. Hata kama ni mwakani barabara hiyo itakamilika tuambieni kama ni mwaka 2009 tuambieni, kama ni mwaka 2010 nafikiri haifiki huko, tuambieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna shida sana na kile kipande cha kutoka Ndundu mpaka Somanga na Waziri asubuhi ya leo amejibu kwamba kuna *tender* itafunguliwa kesho. Mimi nataka kuwauliza kwa nini tumelala mno hata kujikuta katika hali hii. Wenzetu wa *CUF* walipokuwa wanatoka Tunduru walipatwa na dhoruba pale wakapigwa wakaibiwa na kuonja joto ya jiwe. Kipande hiki ni kibaya sana. Sasa kwa nini wasifanye kila jitihada kuhakikisha angalau panapitika, suala ni kwamba papitike. Lakini hali ilivyo sasa hivi mmesikia tungoje *tender,* tungoje wakati mwingine sijui itakuwa lini, kwa kweli watu wangu wamenituma kabisa na kuniambia jamani wanazidi kuchoka na wamechoshwa mno na hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miundombinu ikirekebishwa ndiyo tutaibua uchumi wa Kusini. Sasa niwaelezeni kwamba kuna dalili nyingi kwamba Mikoa ya Lindi na Mtwara ndiyo itakayoongoza katika uchumi wa siku zijazo. Leo hii tumegundua gesi ya *Mnazi Bay,* hapa tumekuwa tukifurahi na kwa kule nyumbani ndugu zetu wanasema kwa kuwa umeme unaonekana wa uhakika zaidi wanasema *kuchele* yaani kumekucha. Tulikuwa tunategemea katika kukucha huko sasa hivi umeme utakuwa unawaka Mtwara, Lindi, Newala, Chigungu, Nachingwea na kila mahali. Lakini niwaambieni ndugu zangu kutokana na utendaji tumepigishwa *break* kwa sababu kuna mambo kadhaa hayajakamilika. Ni mambo ya utendaji na sisi hatuoni sababu gani yasikamilike. Nitawapeni mfano, mwezi Oktoba, Novemba, wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alivyotembelea Mikoa hiyo na kuja kuiona hiyo gesi, Balozi wa Uholanzi alitoa *cheque* ya *Euro* milioni 28 kwa ajili ya kusaidia mradi huo ili kwamba umeme uenezwe vijijini. Hilo lilikuwa ni jambo la furaha na faraja kubwa sana kwa watu wengi wa Kusini. Sasa toka mwezi Oktoba mpaka juzi ndiyo barua rasmi imeandikwa ya kuomba zile fedha, *can you imagine*. Hivi ingekuwa sehemu nyingine mambo haya yangetokea? Toka mwezi Oktoba mpaka juzi ndiyo barua rasmi ya kuziomba fedha imetolewa. Sasa hapa wanaotengeneza sera Waziri, Makatibu Wakuu unakuta wala hawana habari, ni pale katikati utendaji ndiyo unaochelewesha. Sasa mimi ninawaomba sana kwa mfano, katika suala hili Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Fedha wametusaidia sana na Makatibu Wakuu wao, lakini jamani pale katikati wametukwamisha kabisa. Sasa sijui hawa watendaji wana lengo gani?

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba katika Bajeti hii wasimamie Mawaziri kuhakikishia mambo ya namna hii hayatokei tena. Tumegundua hiyo gesi inayoweza kutengeneza umeme kiasi cha megawati 28, hiyo ndiyo imetusumbua. Bahati nzuri tumegundua gesi yenye uwezo wa kutoa megawati 300 ambazo zinaweza kutosha zaidi ya nusu ya mahitaji katika gridi yetu ya Taifa. Jamani msilale hebu fuatilieni, tusije tukakuta kwenye Bajeti nyingine unakuta mradi huu haujatekelezwa. Tunataka mchangamke na ndiyo ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya muwe na moyo na hasa msisitize haya kwa watendaji wenu wa katikati wale Wakurugenzi, Makamishna wasilale, wakamilishe mipango haraka. Watakavyoikamilisha mipango hii, uchumi wa Kusini ndivyo utakavyoibuka na nchi hii ndiyo mtakavyoona jinsi itakavyoendelea. Tafadhalini. Lingine ni suala la wenzetu wa Wizara ya Maji na wao nawaona kidogo wanataka kutupeleka kule kule ambako tulikuwa tunasikitika sana juu ya mambo ya umeme kwamba wanakwenda taratibu mno. Jamani suala la maji Masasi mpaka leo bado kabisa. Mimi nimeangalia katika vitabu hivi toka mwanzo mpaka mwisho najikuna hivi sioni kitu, labda katika Bajeti watatueleza sawasawa. Kwa sababu ahadi ilitolewa toka Serikali ya Awamu ya Tatu kwamba maji yatapatikana Masasi kupitia Mradi wa Mbwiji. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naye aliahidi hivyo hivyo kwamba maji yatapatikana mengi sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, naweza kuendelea kidogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kama nilivyokuahidi utapata dakika zako tano kesho. Kwa sasa muda uliosalia hatuwezi tena kuendelea na Shughuli za Bunge. Naomba nitangaze tu kwa ajili ya mpangilio wa wasemaji wanne wa awali kesho asubuhi. Niseme tu jioni ya leo wameongea Waheshimiwa Wabunge 12. Watakaoongea kesho, akishamaliza Mheshimiwa Raynald Mrope, dakika zake tano ni Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Kidawa Saleh. Wanne wa kwanza hao kwa ajili ya kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 19 Juni, 2007 saa tatu asubuhi)*